SUPA JACKPOT
TZS. 1,062,078,169
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 3

**RAIS** Dk. Mwinyi akunwa ukusanyaji mapato Zanzibar




NGO 'yawatoa' kinamama kuwaingiza katika kilimo cha kisasa kwa ushindi

Na Thobias Mwanakatwe, Ikungi

KILIMO ni kiungo muhimu katika kuchagiza maendeleo na kuhakikisha uhakika wa chakula. Wakati kilimo kinabaki kuwa uti wa mgongo wa jamii nyingi barani Afrika, katika baadhi ya nchi kumejengwa mazoea kwamba kazi hiyo inafanywa na kada fulani pekee katika jamii.

Hapo ndipo Shirika la Farm Africa kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa linalohusika na masuala ya wanawake UN-Women, zimeamua kuwekeza kwa kada ya wanawake katika kilimo zao la alizeti.

Elibariki anaeleza kwamba, kupitia shirika hilo wameweza kuboresha Chama cha Ushirika cha Mnang'ana na vyama vilivyopo vijiji jirani, ikiwamo Amunyu ambako wamejifunza matumizi ya mbegu bora na namna ya upandaji, hali kadhalika matumizi sahihi ya pembejeo.

MAOFISA SERIKALI

Kwa upande wake, Mkuu wa Idara ya Kilimo Wilaya ya Ikungi, Gurisha Msemo, anasema mradi huu ambao unajulikana kama 'Tufikie usawa kijinsia wa kumuwezesha mwanamke, unatekelezwa katika vijiji vya Kipumbiko, Irisia, Munyu na Mnang'ana.

Nipashe
Ijumaa Desemba 30, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581175
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

UKURASA 13

# Askofu aibua hoja ukosoaji serikalini

UKURASA 2



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akihutubia katika maadhimisho ya Siku ya Shukrani na Furaha kwa Walipakodi Zanzibar kwa mwaka 2021/2022, Bodi ya Mapato jana. **PICHA: IKULU**

## Muhimbili yafafanua huduma kuhamishiwa tawi Mloganzila

UKURASA 2

## Vigogo wa mamlaka maji kortini madai ya ubadhirifu

UKURASA 3

**MICHEZO** SIMBA, PRISONS HATUMWI MTOTO UK. 32

**KATUNI** UK. 6




Mafundi wakiendelea na maboresho ya Bandari ya Tanga kwa kuongeza kina cha maji kutoka mita tatu hadi 13 na upana wa mita 73 kwenye njia ya kuingiza/kutokea meli kilomita 1.7. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Askofu aibua hoja ukosoaji serikalini

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Elimu Pentekoste Tanzania, Peter Konki amewataka wasaidizi wa Rais Samia Suluhu Hassan kuacha alichokiita kumtupia mishale kiongozi huyo, badala yake wamsaidie kutimiza majukumu yake.

Vilevile, Askofu Konki amesema ni vizuri wasaidizi wa Rais wakatoa nafasi kwa wananchi kuikosoa serikali.

Akizungumza jana wakati wa mkutano mkuu maalum wa 19 wa kanisa hilo uliofanyika mjini Babati, askofu huyo alisema wasaidizi wa Rais wanapaswa kubeba jukumu lao kwa uzito na si kumfanya Rais ashindwe kutimiza malengo yake.

Akifafanua hoja ya ukosoaji serikalini, Askofu Konki alikuwa na angalizo lake katika hilo, akisema kuwa kama kuna mtu anataka kuikosoa serikali, inabidi afanye hivyo kwa lugha yenye staha na siyo kutukana.

Alisema miongoni mwa majukumu makuu aliyonayo Rais ni kusimamia ujenzi wa miradi mikubwa ya kimkakati ikiwamo ya ujenzi wa Bwawa la Nyerere mkoani Pwani na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Msalato mkoani Dodoma.

"Wito wangu kwa wasaidizi wa Rais ni kwamba, wamsaidie Rais ili atimize malengo yake aliyojiwekea kwa ajili ya kuwatumikia Watanzania," alisema Askofu Konki.

Aliwataka wasaidizi wa Rais walioko mpaka ngazi za chini, kuwasaidia wananchi kufikisha mahitaji kwa Rais ili ayafanyie kazi.

Kuhusu ujenzi wa kanisa hilo unaoendelea mjini Babati, alisema mpaka sasa wameshatumia Sh. milioni 99 na jumla ya gharama yote itakayotumika ni Sh. milioni 800 hadi kukamilika kwake.

"Mradi huu wa ujenzi wa kanisa ukikamilika, utabadili mandhari ya Mji wa Babati kwa kuwa hakuna kanisa kubwa kama hilo," alisema.

Alibainisha kuwa hawana vitega uchumi vya kitaifa katika kutekeleza miradi ya maendeleo, hivyo wanategemea zaka.

Alifafanunua kuwa ili wajenge uchumi wa kanisa hilo, tayari wameshanunua ekari tatu kwenye eneo la Msalato mkoani Dodoma ambako watajenga Shule ya Sekondari.

Alisema "kanisa hilo tayari limenunua eneo la kujenga makao makuu yake mkoani Dodoma kwenye eneo la Ihumwa".

# Muhimbili yafafanua huduma kuhamishiwa tawi Mloganzila

**Na Christina Mwakangale**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH), imesema uamuzi wake wa kuendelea kuhamisha wagonjwa na baadhi ya kliniki kwenda Mlonganzila ni kupunguza msongamano.

Pia imesema hakuna tofauti ya huduma baina ya Muhimbili na Mloganzila kwa sababu wataalamu wamegawanywa kwa usawa na wengine wanahudumia kote kulingana na mahitaji na sio kwamba huduma za eneo jipya ni mbovu.

Ufafanuzi huo ulitolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Prof. Mohamed Janabi, wakati akizungumza na Nipashe kwa simu.

Nipashe ilitaka kupata ufafanuzi kuhusu uwapo wa malalamiko ya baadhi ya wagonjwa wanaohudhuria kliniki Muhimbili kuhamishiwa Mloganzila huku baadhi ya watu wakidai huduma za eneo jipya si nzuri ndiyo maana wanakilimbilia eneo la zamani.

Alisema tangu kuanzishwa kwa kliniki za magonjwa yasiyoambukiza yakiwamo kisukari, moyo na kiharusi, Mloganzila imesaidia kupunguza msongamano kwenye kliniki hizo MNH-Upanga, kutoka wagonjwa 2,000 hadi 1,600 kwa siku.

Prof. Janabi alisema jamii inapaswa kufahamu kwamba lengo la hospitali kuhamishia kliniki hizo Mloganzila ni kupanua wigo wa matibabu, huku wataalamu watoa huduma wakiwa ni wale wale waliokuwa wakitoa huduma MNH-Upanga.

"Dhana itabakia kuwa dhana lakini madaktari ni wale wale. Tumewahamisha wote kule (Mloganzila) na hatuwezi na magonjwa yote haya ya kulipuka kujazana Muhimbili Upanga. Hivi tulivyopeleka kule (Mloganzila), Muhimbili bado tunaona wagonjwa 1,600 kabla ilikuwa 2,000 kwa siku.

"Kasi ni kubwa zaidi madaktari wana vyumba kila daktari ana chumba, kina nafasi, kuna mashine za kisasa zaidi na kwa wodi ni kubwa zaidi na sehemu ya kufanyia mzaoezi, hakuna tofauti ya dhana hii hata waandishi mtusaidie, kwamba hospitali zote hizi," alisema Prof. Janabi.

Alisema Hospitali ya Mloganzila yenye vitanda takribani 600, imesaidia kupunguza idadi ya wagonjwa wanaolazwa Muhimbili kwa kuwa miundombinu ilizidiwa huku wagonjwa wakilazimika kulala wawili kwenye kitanda kimoja.

"Saratani, moyo, kiharusi na kisukari kliniki inafanyika Mloganzila. Mwitikio ni mzuri sasa hata wenzetu wa usafiri wa mwendokasi biashara yao, imeongezeka na wagonjwa wanashushiwa ndani ya eneo la hospitali," alisema Prof. Janabi.

Novemba Mosi, mwaka huu, MNH iliamua kuimarisha kliniki za magonjwa makubwa manne, yakiwamo ya moyo na magonjwa ya mfumo wa fahamu, kwenda MNH-Mloganzila, kwa kuwa kuna vifaa vya kisasa, wataalamu na eneo la kutosha kuwezesha watoa huduma kufanya kazi kwa ufanisi.

# IPP yang'ara katika tuzo Habari za Watoto

**Na Elizabeth Zaya**

WAANDISHI wa habari wa IPP Media kupitia gazeti la Nipashe na East Afrika Radio wametwaa tuzo za Uandishi wa Habari za Watoto za mwaka huu.

Tuzo hizo hutolewa na Jukwaa la Wahariri (TEF) kwa ushirikiano na Shirika la Kimataifa linalohudumia Watoto (UNICEF).

Walioshinda kwa Nipashe ni Marko Maduhu aliyeshinda Tuzo ya Mwandishi Bora wa Habari za Watoto kwa ujumla na Julieth Mkireri aliyenyakua Tuzo ya Habari za Watoto - Ndoa za Utotoni.

Mwingine wa IPP Media aliyeshinda ni Anna Sombida wa East Afrika Radio, aliyetwaa Tuzo ya Mwandaaji Bora wa Kipindi cha Radio - Habari za Watoto.

Tuzo hizo zilotolewa jana jijini Dar es Salaam, jumla ya waandishi wa habari 12 wakitunukiwa, huku Mshindi wa Jumla akiwa ni Faraja Masinde wa Mtanzania Digital.

Washindi wengine wa tuzo hizo ni Tumaini Msowoya wa gazeti la Mwananchi, Aidan Mhando wa Chanel Ten, Anold Kailembo wa Radio Kwizera, Shua Ndereka wa Mwiwata Radio, Vick Kimaro wa HabariLeo, Judith Ferdinard wa Majira, Sabina Martin wa Chai FM Radio na Stansilaus Lameck wa Blogu ya Dar 24.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mwenyekiti wa TEF, Deodatus Balile alisema kampeni ya kupinga ndoa za utotoni ni lazima iwe endelevu kwa kila mwandishi wa habari kuhakikisha anashiriki kikamilifu kuandika habari za kuelimisha jamii kupinga ndoa za utotoni ili kusaidia watoto kutimiza ndoto na malengo yao.

Aliishukuru UNICEF kwa kuendelea kuunga mkono jitihada za kupinga ukatili dhidi ya watoto nchini.

Mwakilishi wa UNICEF, Ousmane Niana, alipongeza TEF kwa kuunga mkono mapambano dhidi ya ukatili kwa kuandika habari za kupinga ukatili dhidi ya watoto na kuhakikisha wanapata haki zao za msingi.

Alisema kuna haja kuendelea kuhamasisha jamii kupinga vitendo vya ukatili kwa watoto ikiwamo kupinga ndoa za utotoni ili wasome na kufanikisha ndoto zao.

## HABARI KITAIFA

# Vigogo mamlaka ya maji kortini madai ubadhirifu




Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mpanda (MUWASA), Hussein Salum Nyemba na Kaimu Ofisa Usimamizi wa Fedha na Utawala wa Mamlaka hiyo, Justine Wambali, wakifikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Mpanda jana. **PICHA: NEEMA HUSSEIN**

**Na Neema Hussein,** MPANDA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Katavi imewafikisha mahakamani watumishi wawili wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mpanda (MUWASA) kwa mashtaka mawili, ikiwamo kuisababishia mamlaka hasara ya Sh. milioni 17.817.

Hatua hiyo imechukuliwa ikiwa ni siku 17 tangu Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa kuwatuhumu kwa hujuma za kiofisi na kuiagiza TAKUKURU mkoani hapa kuwachukulia hatua za kisheria.

Watumishi waliofikishwa mahakamani jana ni Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mpanda (MUWASA), Hussein Nyemba na Kaimu Ofisa Usimamizi wa Fedha na Utawala wa mamlaka hiyo, Justine Wambali.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Naibu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Katavi, Stuart Kiondo alisema mbali na shtaka hilo, pia wanakabiliwa na shtaka la matumizi mabaya ya madaraka. Alisema washtakiwa hao pia wanatuhumiwa kutumia madaraka yao vibaya, kuajiri watumishi wapya 37 bila ya baraka za kisheria kutoka Bodi ya MUWASA.

Kiondo alidai watuhumiwa hao waliofikishwa mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya, Mpanda Luoga, walitenda makosa hayo kati ya Novemba na Desemba Mosi mwaka huu.

Alidai hatua hizo zilikuwa kinyume cha kifungu cha 31 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa.

"Ofisa utumishi alikuwa ana uwezo wa kumshauri mkurugenzi wake kuhusiana na tukio hilo la ajira za watumishi 37," alidai Kiondo.

Baada ya kufikishwa mahakamani, washtakiwa hao walisomewa mashtaka yaliyodai kwamba walishindwa kutekeleza majukumu yao na kuisababishia MUWASA hasara.

Hata hivyo, washtakiwa wote wawili walikana mshtaka dhidi yao, Mkurugenzi Mtendaji wa MUWASA, Nyemba, akiachiwa kwa dhamana huku Kaimu Ofisa Usimamizi wa Fedha na Utawala, Wambali, akirudishwa rumande kutokana na kushindwa kutimiza masharti ya dhamana.

Masharti hayo yalijumuisha kuwapo mshtakiwa kuwasilisha dhamana ya mali isiyohamishika yenye thamani isiyopungua Sh. milioni tano, hali kadhalika awapo mdhamini mwengine anayeweka bondi mali isiyohamishika yenye thamani kama ya mshtakiwa.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Januari 17 mwakani itakapokuja kwa ajili ya washtakiwa kusomewa maelezo ya awali.

# Mwinyi akunwa ukusanyaji kodi ZRB

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema ameridhishwa na ukusanyaji wa kodi na mapato kutoka Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB).

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana katika kilele cha sherehe za mwezi wa shukurani na furaha kwa walipakodi, zilizofanyika Hoteli ya Golden Tulip, Zanzibar.

Sherehe hizo ziliambatana na utoaji wa zawadi kwa walipakodi bora huku Taasisi ya Zanzibar Petroleum ikiibuka na ushindi wa jumla katika tuzo hizo.

Alisema tangu kuanza kwa mwaka huu wa fedha katika kipindi cha miezi mitano, ZRB imekuwa na mafanikio makubwa na makusanyo ya kodi kutokana na kuongezeka. Katika kipindi cha Julai hadi Novemba, mwaka huu, ZRB imekusanya Sh. bilioni 236.39 wakati lengo lilikuwa kukusanya Sh. bilioni 238.5.

Rais alisema ukusanyaji huo wa mapato ni sawa na ongezeko la ukasanyaji wa asilimia 67.6 ikilinganishwa na makusanyo ya Sh. milioni 141 kwa kipindi cha Julai hadi Novemba, mwaka 2021.

Alisema mafanikio hayo yanatokana na kazi nzuri inayofanywa na ZRB pamoja na mwamko wa wananchi kulipa kodi.

"Penye kazi nzuri lazima tupongeze na tutoe sifa zinazostahiki. Tusiwe tu tunasema mambo yanapokuwa mabaya. Binafsi nilifika ZRB kipindi cha nyuma na kueleza kutoridhishwa na ukusanyaji wa kodi lakini leo (jana) nasema hadharani sasa naridhishwa na ukusanyaji wa kodi wa ZRB," alisema Dk. Mwinyi.

Kwa mafanikio yanayopatikana kutokana na ukusanyaji wa kodi, aliwapongeza wafanyakazi wa ZRB kwa jitihada wanazochukua ambazo zimeongeza ufanisi na kukua kwa kasi la ongezeko la ukusanyaji wa kodi.

Aliwataka watendaji hao kuendelea na jitihada za kukusanya kodi kwa mujibu wa sheria zilizoko na kuwashirikisha walipakodi kwa lengo la kutatua changamoto zilizoko ili kuongeza uwezo wa serikali katika kuwahudumia wananchi.

Aidha alisema pamoja na jitihada hizo za kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato lakini, sheria zilizoko pia zimechangia ukusanyaji wa mapato kwa sababu ukuaji huo wa uchumi ni matokeo ya mazingira mazuri yanayoendelea kujengwa na serikali kwa wawekezaji.

Alisema mwelekeo wa kukusanya mapato zaidi upo na kama ilivyoelezwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwamba ifikapo mwaka 2025 mapato yanayokusanya na ZRB na Mamalaka ya Mapato Tanzania (TRA) yafikie tirioli 1.5 kwa mwezi.

Dk Mwinyi alisema lengo la serikali ni kujenga utawala wa kodi utakaoiwezesha ZRB kukusanya mapato yote ya serikali yanayostahiki kwa kiwango cha juu zaidi kwa sababu serikali inaendelea kuimarisha mifumo ya kodi ili kuboresha ukusanyaji wa mapato.

Ili kufanikisha azma hiyo, aliwataka maaoisa masuhuli wote wa taasisi na idara za serikali ambazo zimepewa uwakala wa kuzuia kodi kutoka kwa wafanyabiashara waliopatiwa huduma, kuhakikisha wanazuia kodi hiyo na kuiwasilisha kwa wakati ZRB na TRA kama sheria inavyoeleza.

"Serikali haitosita kumchukulia hatua ofisa masuhuli yeyote ambaye ama hazuii kodi au hawasilishi kodi aliyoizuia kwa wakati na kwa ukamilifu," alisema.

Kamishna wa ZRB, Yussuf Mwenda, alisema katika kuongeza makusanyo ya kodi, ZRB kwa mwaka huu wa fedha, imepanga kukusanya Sh. bilioni 579 na ifikapo Juni, mwakani kufikia asilimia 100 ya ukusanyaji wa kodi.

Alisema usimamizi mzuri na ufanisi wa bodi ndio umesababisha makusanyo makubwa ya kodi na kuimarisha mifumo ya usimamizi wa kodi.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya, alisema bila kodi, maendeleo hayatapatikana, hivyo aliwasisitiza wananchi kuendelea kudai risiti kila wanapofanya ununuzi.

Alisema tayari Baraza la Wawakilishi limeshapitisha muswada wa sheria ya kubadilisha bodi ya mapato na kuwa Mamlaka ya Mapato Zanzibar baada ya Dk. Mwinyi kutia saini sheria hiyo. Alisema mabadiliko hayo yataleta ufanisi mkubwa katika ukusanyaji wa kodi.

Pia alisema mabadiliko hayo yataifanya mamlaka hiyo kuwa chombo kinachoaminika kwa jamii na kutoa huduma bora zaidi za mapato. Katika sherehe hizo, Dk. Mwinyi alitunukiwa tunzo ya mlipaji kodi mzuri.

## Re-Advertisement for
## A JOB VACANCY IN ARUSHA

A Printing Company operating from Arusha has retained us to help recruit a ***Sales & Business Promotion Manager*** for their operations in Arusha.

**Required qualifications are**:

- Good Academic Education with outstanding passes
- Recognized Relevant Professional training **especially** in Graphic Designing
- 3 – 5 years of working experience especially in the Printing Industry
- Valid driving licence

Attractive pay package including **performance-based sales bonus** will be offered.

**Please email your detailed CV together with certificates in PDF format before 10th January 2023 to:**

**Eugen@infojep.com**

17209402

HABARI KITAIFA

# Wizara yatoa kalenda masomo 2023

**Na Maulid Mmbaga**

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imetoa ratiba mpya kwa mwaka wa masomo 2023, huku ikiagiza kuzingatiwa kwa kalenda hiyo ili kupata matokeo chanya.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kamishna wa Elimu, Dk. Lyabwene Mtahabwa, kalenda hiyo imeandaliwa ili kuzingatia idadi sahihi ya siku za masomo na kutekeleza mtaala kwa ufanisi, kwa shule za awali, msingi na sekondari kwa mwaka wa masomo 2023.

Kalenda hiyo inaonyesha kwamba mhula wa kwanza utaanza Januari 9, 2023, ambao utaenda hadi kwenye likizo fupi inatakayoanzia Machi 31 hadi Aprili 11 na kwamba likizo ndefu itaanzia Mei 31 hadi Julai 3, mwakani.

"Muhula wa pili utaanzia Julai 3 utaenda hadi kwenye likizo fupi itakayoanza Septemba mosi hadi 18, tarehe hiyo watakaporudi wataendelea na masomo hadi Desemba 7 itakapoanza likizo ndefu hadi Januari 9," alisema.

"Kalenda hiyo inatakiwa ifuatwe na kuzingatiwa ipasavyo ili kupata matokeo chanya, siku za masomo kwa mwaka ni 194 na mashindano ya UMITASHUNTA yatafanyika Juni mbili hadi 13 na UMISENTA yataanza Juni 15 mpaka 26," aliongeza.

Pia alisema mashindano ya michezo ya shule za sekondari za Afrika Mashariki (FEASSSA) yatafanyika Agosti 18 hadi 28 na kwamba mwongozo huo utaanza kutumika kuanzia Januari Mosi, 2023.

Akizungumza na Nipashe jana, Halima Hussein, mkazi wa mkoani Dar es Salaam, alisema ratiba ya awali iliyokuwa ikitumika wakati wa janga la UVIKO-19 na sensa ilikuwa ikitoa muda mrefu wa kukaa nyumbani kwa wanafunzi jambo alilotaja kuwa lilikuwa linachangia kurudisha nyuma ufaulu wa wanafunzi.

Pia aliipongeza Wizara ya Elimu kwa kutoa ratiba na mwongozo ambao utawafanya wanafunzi kutumia muda mwingi wakiwa shuleni, akidai kwamba hiyo itasaidia kwa kiasi kikubwa kuongeza ufaulu kwa watoto wao.

Aidha, ikiwa zimebaki siku 10 shule kufunguliwa, Halima alibainisha kuwa kumekuwa na tatizo kubwa la kupanda kwa bei za vifaa vya wanafunzi, ikiwamo daftari, viatu na sare za shule akieleza kuwa hali hiyo itachangia kudhorotesha kasi ya wanafunzi kuwasili shule kwa wakati pindi shule zitakopofunguliwa.

"Watanzania wengi kipato chetu ni cha chini, sasa kipindi kama hiki wanapotupandishia bei sio sahihi kabisa, hii imekuwa ni kama mazoea ni jambo linalojirudia kila mwaka, wakati mwingine unashindwa unaona ni bora usubiri kipindi hiki kipite ndio uende kununua," alisema na kuongeza:

"Ni muhimu serikali ilitazame hili suala, ikiwezekana wapange bei elekezi kama wanavyofanya kwenye bidhaa zingine ili kuwe na uwiano na iwadhibiti na kuwachukulia hatua wafanyabiashara wanaopandisha bei kiholela katika kipindi hiki ambacho kuna uhitaji mkubwa wa vifaa hivi," alisema Halima.

Bakari Mashambo, mkazi wa Moshi Mkoani Kilimanjaro, alibainisha bei za vifaa vya shule uliyoko sokoni kwa sasa, alisema daftari walizokuwa wananunua Sh. 500 zimepanda hadi 800, walizokuwa wakinunua 1,500 zimepanda hadi 2,000, zilizokuwa zikiuzwa 2,500 sasa ni 3,000 na za 3,000 zimepanda hadi 3,500 kulingana na ukubwa, ikiwa ni ongezeko la wastani wa Sh. 300 hadi 500.

"Viatu tulivyokuwa tunanunua Sh. 25,000 vimepanda hadi 30,000, shati za shule zilikuwa 6,000 saivi ziko 8,000 mpaka 10,000, kaptura awali 10,000 sasa wanauza 13,500 hadi 15,000, suruali zilikuwa 15,000 zimepanda hadi 20,000," alisema Mashambo.

Naye Ally Masudi ambaye ni mfanyabiashara anayezunguka katika minada mbalimbali mkoani Dar es Salaam, akiuza vifaa tofauti vikiwamo vya shule, alisema bidhaa nyingi za shule katika kipindi hiki zinapanda bei kwasababu uhitaji wake ni mkubwa.

"Kule tunakokwenda kufungasha vinakuwa ni vichache na bei zinakuwa zimeongezeka kwasababu kila mtu anang'ang'ania apate, hivyo na sisi tunapokuja sokoni tunalazimika kuongeza kidogo ili tupate faida," alisema Masudi.

Kwa mujibu wa wizara ya elimu, takribani wanafunzi milioni moja wanatarajiwa kujiunga na kidato cha kwanza Januari 2023 na kwamba shule zitakapofunguliwa idadi ya wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha nne itakuwa zaidi ya milioni 2.7.



Mchungaji wa Kanisa la Waadventista Wasabato Mbezi Luis Dar es Salaam, Onesmo Dzombe, akizungumza jana, katika ibada maalum ya siku nne za maombi ya kumshukuru Mungu kumaliza mwaka salama. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mtoto aliwa na fisi akiogeshwa mtoni

**Na Rose Jacob,** MWANZA

MTOTO Emmanuel Michael (3), mkazi wa Kijiji cha Mwangika, Kwimba mkoani Mwanza, amefariki dunia kwa kuliwa na fisi wakati akiogeshwa mtoni na dada yake.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Wilbroad Mutafungwa, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo Desemba 27, mwaka huu, majira ya saa 12:00 jioni wakati mtoto huyo na wenzake wakiogeshwa kwenye mto na dada yao.

"Mtoto Emmanuel alikwenda mtoni akiwa na dada yake, Mary Michael (14) akiwa na ndugu zake wanne ambao walikuwa wakiogeshwa na binti huyo. Ghafla alitokea fisi mkubwa na kuanza kuwashambulia," alisema Mutafungwa.

Alisema, Mary alipambana na fisi huyo kwa ajili ya kuwaokoa wadogo zake lakini ilishindikana, maana mnyama huyo alimzidi nguvu ndipo akafanikiwa kumng'ata mkono wa kulia mtoto Emmanuel na kukimbia naye porini.

Aidha, Mutafungwa alisema Jeshi la Polisi mkoani Mwanza kwa kushirikiana na Idara ya Wanyamapori na wananchi, walifanya msako na kufanikiwa kupata mabaki ya viungo vya mtoto huyo na nguo alizokuwa amevaa.

"Jitihada za kumsaka fisi huyo zinaendelea ili asije kuleta madhara mengine kwa jamii ya maeneo hayo. Nawaomba wananchi kuchukua tahadhari ya kuweka uangalizi wa karibu kwa watoto, katika maeneo yote hatarishi ili kuwaepusha na vifo na hatari inayoweza kuepukika," alisema Mutafungwa.

# Mkurugenzi mahakamani madai ya kujipatia bil. 5.1/ kwa udanganyifu

**Na Grace Gurisha**

MKURUGENZI Mtendaji wa Kampuni ya JATU Public Ltd, Peter Gasaya (32), amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, kwa tuhuma za kujipatia Sh. billioni 5.1 kwa njia ya udanganyifu.

Gasaya anadaiwa kujipatia fedha hizo kutoka Chama cha Akiba cha Kuweka na Kukopa cha (SACCOS) cha JATU kwa madai kuwa ataizalishia faida.

Mkurugenzi huyo alifikishwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Mary Mrio, na kusomewa shitaka moja la kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na Wakili wa Serikali, Tumaini Mafuru.

Mafuru alidai kuwa kati ya Januari Mosi, 2020 na Desemba 31, 2021 mshtakiwa akiwa ndani ya jiji na mkoa wa Dar es Salaam kama mkurugenzi wa kampuni hiyo, alijipatia Sh 5,139,865,733 kwa njia ya udanganyifu kutoka JATU SACCOS.

Mshtakiwa anadaiwa alichukua fedha hizo kwa madai kuwa atazipanda na kuzalisha faida huku akijua si kweli.

Baada ya mshtakiwa kusomewa shtaka lake, alikana kuhusika na tuhuma hizo. Mafuru alidai upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika na kuomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Hakimu Mrio alisema mahakama hiyo haina mamlaka ya kutoa dhamana inayozidi Sh milioni 300 kwa hiyo mshtakiwa atapelekwa mahabusu. Kesi hiyo imeahirishwa hadi Januari 11, mwakani kwa ajili ya kutajwa na kuangalia hatua ya upelelezi ilipofikia.

# Bandari Tanga kuanza kuhudumia moja kwa moja meli kubwa Januari

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

UONGOZI wa Bandari ya Tanga umesema matumizi ya eneo jipya kwa meli kubwa za mizigo kushusha shehena moja kwa moja, unatarajiwa kuanza Januari, mwakani.

Hatua hiyo inatokana na upanuzi wa bandari hiyo umefikia asilimia 82.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi jijini hapa, Meneja wa Bandari ya Tanga, Masoud Mirisha, alisema mradi huo umegharimu zaidi ya Sh. bilioni 429.1 na ulianza Agosti 3, 2019 kwa lengo la kuongeza kina cha maji kutoka mita tatu hadi 13.

Sambamba na hilo, ujenzi huo umeongeza upana wa mita 73 kwenye njia ya kuingiza na kutokea meli kilomita 1.7, sehemu ya kugeuzia meli kutoka mita tatu hadi mita 13 yenye kipenyo cha mita 800.

Alisema awamu ya kwanza ya mradi ambayo ni manunuzi ya mitambo imekamilika kwa asilimia 100, na kwamba ya pili ilianza Septemba 2020 kwa miezi 22 kwa lengo la kuboresha magati mawili yenye urefu wa mita 450 kwa kuongeza mita 50 upande wa mashariki na mita 92 magharibi.

Mirisha alisema hadi sasa mkandarasi amekabidhi kipande chenye urefu wa mita 300 huku akiendelea kukamilisha kipande cha mita 150.

"Hii ni bandari kongwe kuliko zote nchini lakini meli zilikuwa zinakuja na mzigo umbali wa kilomita 1.7 kutoka kwenye gati kutokana na kina cha maji kuwa ni mita 3 hadi 3.5 hali ambayo haikuruhusu meli kubwa. Hii ilileta gharama mara mbili kuupakua na kuupakiza halafu kupakua tena," alisema.

Kuhusu matarajio baada ya mradi kukamilika ni uwezo wa bandari utaongezeka kutoka kuhudumia shehena tani 750,000 hadi milioni 3, kuongezeka kwa kodi, pato la mkoa na taifa kutokana na mizigo itakayosafirishwa kupitia bandari hilo.

Alisema kukamilika kwa mradi huo ni neema kwa mikoa ya Kanda ya Kaskazini na nchi jirani, lakini kwa uchumi wa mikoa wa Tanga pamoja na kuongeza fursa kwa wananchi kwa ujumla.

"Maboresho haya yatasaidia sana kupunguza gharama za uendeshaji wa bandari kuondokana na gharama mara mbili kwa kuwa mizigo itashushwa moja kwa moja eneo la bandari, pia tunatarajia kuongezeka kwa ufanisi katika utendaji wa bandari," alisema.

Kwa mujibu wa Meneja huyo, baadhi ya changamoto na mikakati ya kuzitatua ni uhaba wa eneo la kufanyia kazi ndani ya bandari ambayo Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) imeshaanza taratibu za kutwaa maeneo yaliyo karibu na kwamba taratibu zinaendelea.

Pia wanatarajia kutumia eneo la Mwambani lililoko kilomita saba kutoka bandarini kwa ajili ya eneo la kuhifadhi mizigo.

Naye Ofisa Masoko wa Bandari ya Tanga, Rose Tandiko, alisema wameandaa mkakati wa kuitangaza bandari hiyo ndani na nje ya nchi kwa kukutana na wafanyabiashara wakubwa na wamiliki wa meli kueleza faida za kutumia eneo hilo.

"Ili bandari hii ifanye kazi vizuri tunaiomba serikali itoe tamko kwamba mizigo fulani ipitishiwe hapa, mfano tuna mazao ya biashara kama kahawa iwapo itasema mazao haya yatapitia bandari fulani itasaidia sana, au mizigo inayokwenda Kanda ya Kaskazini ipitia hapa itainua bandari hii na kuchagiza uchumi wa maeneo haya," alisema.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Tanga, Pili Mnyema, alisema kwa kipindi cha Rais Samia Suluhu Hassan kumekuwa na mabadiliko makubwa ikiwamo kuharakisha maboresho ya bandari hiyo, ili ianze kazi ambayo itakwenda kuinua uchumi wa mikoa na kuongeza fursa kwa mwananchi mmoja mmoja.

"Kwa sasa treni inaweza kuingia moja kwa moja hadi ndani ya bandari, itarahisisha kazi ya utoaji shehena, niwahisi wafanyabiashara na wasafirishaji wa mizigo kutumia bandari yetu, hii ni fursa ya kukuza uchumi wa wananchi na mikoa ya kaskazini, lakini itapunguza gharama," alisema.

Moja wa wafanyakazi wa bandari hiyo, Mwanahamisi Msemo, alisema uwepo wa maboresho hayo kumemwezesha kufanyakazi na kupata kipato cha kumsaidia kuendesha maisha.

"Nimeanza kazi Januari hapa ninachokipata sio sawa na kukaa nyumbani, kuna watu wako nyumbani hawajui wakapate wapi kipato, ninachokipata kinanisaidia kulipa kodi, kulisha watoto na mahitaji mengine. Inanipunguzia kudharaulika kwamba mwanamke siingizi kipato chochote kwa familia," alisema.


## TANGAZO KWA UMMA KUHUSU MABADILIKO YA UWEKAJI WA MACHAPISHO YA UZALISHAJI NA YA MUDA WA TAREHE YA MATUMIZIYA BIDHAA ZETU

SERENGETI BREWERIES

Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) inatoa taarifa kwa umma, wateja na wadau wetu kwamba, tumefanya mabadiliko katika namna tunavyoweka chapisho za Uzalishaji na Muda wa Tarehe ya Matumizi ya bidhaa tunazozalisha.

Kwa sasa Kampuni ya Serengeti imeanza kutumia teknolojia ya chapisho za 'laser' kama mbadala wa chapisho ya taarifa za Uzalishaji na ile ya Muda wa Tarehe za Matumizi wa bidhaa zetu.

Teknolojia hii mpya ya Taarifa ya chapisho kwenye lebo za Uzalishaji na ya Muda wa Tarehe ya Matumizi kwa sasa utakuwa tofauti na ule wa awali ambapo taarifa hizi za Muda wa Tarehe ya Matumizi zilikuwa zikichapishwa moja kwa moja kwenye Chupa.

Mabadiliko haya ya chapisho ya Muda wa Tarehe ya Matumizi, utatoa taarifa za muda wa matumizi ya bidhaa zetu zikiwa zimechapishwa kwa uwazi kabisa katika lebo ya bidhaa husika hivyo kudumu muda wote wa matumizi wa bidhaa husika ikiwa sokoni kama inavyotakiwa na Mamlaka ya Udhibiti Viwango Nchini (TBS). TBS inahitaji taarifa hizi kuwekwa katika bidhaa zikiwa zinaonekana kwa urahisi na kubakia katika bidhaa muda wote wa matumizi yake ili kudhibiti viwango vya ubora. Teknolojia hii ya chapisho za 'Leser' ni maarufu katika kuweka chapisho na ina faida zifuatazo;

1. Haighushiki na haitumii wino
2. Ni ya kudumu na rahisi katika utambulishaji wa bidhaa
3. Ina ubora wa hali ya juu

Tumeanza kufanya mabadiliko haya katika chapa zetu pendwa za 'Serengeti Lager' na 'Serengeti Lite' na tutamaliza na chapa zetu zingine miezi ijayo. Ili kuepusha usumbufu, tafadhali kumbuka kuwa tutaendelea kutumia teknolojia zote mbili kwa sasa hadi tutakapobadilisha matumizi ya chapisho za teknolojia mpya ya Laser katika bidhaa zetu zote miezi michache ijayo.




Taarifa ya Muda wa Tarehe ya mwisho wa Matumizi kama ilivyo sasa




Taarifa ya Muda wa Tarehe ya Mwisho wa Matumizi kwa teknolojia mpya ya chapisho ya "leser"

Johnnie Walker Keep Walking · Smirnoff · Bongo Don Spirit · Captain Morgan · Guinness Made of More · Pilsner Lager · Cîroc · Serengeti Lite · Serengeti · Gordon's Shall We?

*Sherehekea Maisha Kila Siku Kila Mahali*

17210202

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Matukio ya kujiua, kuua yanaweza kudhibitiwa

**MATUKIO** ya watu kujiua au kuua wenzao yanaweza kudhibitiwa kama watafuata ushauri wa madaktari na wanasaikolojia.

Mengi ya matukio hayo yanaeleweka, husababishwa na hasira na mihemko ambayo kama itadhibitiwa mapema itapunguza madhara.

Elimu kwa jamii ni jambo muhimu kwa sababu itawafanya watu kuelewa vitu vya kuepuka wanapoona viashiria vyovyote vya vitendo vya mauaji.

Imeshauriwa pia watu wanapohisi hali isiyo ya kawaida kuondoka eneo ama mazingira yanayochochea kutenda mambo mabaya. Njia hiyo imetajwa kuwa dawa inayoweza kudhibiti ama kupunguza matukio ya watu kujiua au kuua.

Daktari Bingwa wa Binadamu, Idara ya Afya ya Akili kutoka Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya, Raymond Mgeni, anaeleza kuwa jamii inapaswa kudhibiti msukumo wa hasira unaochochewa na sababu yoyote, ikiwamo kuudhiwa ama kusingiziwa jambo lolote kwa sababu ni kati ya visababishi vya ongezeko la matukio ya mauaji nchini ni ukosefu wa kudhibiti hali hiyo.

Takwimu zilizotolewa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) mwaka juzi kuhusu haki za binadamu, zinaonesha kuwa watu wanne kati ya 10 waliojiua mwaka jana (2021), walikuwa ni vijana wenye umri kati ya miaka 15 hadi 35.

Ili kudhibiti matukio ya watu kujiua au kuua, jamii inapaswa ijenge mazoea na utaratibu wa kujifunza na kuwafundisha watoto. Kutoruhusu kuchukua hatua wapatwapo na msukumo huo na kuondoka eneo ama mazingira yanayowasababishia hasira.

Daktari anafafanua kuwa, matukio yanayoongezeka ya watu kujiua hutokana na kuchochewa na misukumo isiyodhibitiwa kutokana na hasira; ikiwamo mazingira yanayowazunguka na kusababisha mtu kuamua jambo bila kutarajia na kufahamu athari zake baadaye.

"Kuna wakati mwingine unaongea na mtu anakuudhi, kuna wengine hawana udhibiti, wengine wanaoudhiwa wanapoambiwa jambo ambalo hawajalitenda wanajikuta wakipatwa na hasira. Mwingine akipandwa na hasira anaweza kuchukua kitu ajichome au anywe sumu."

Hali hiyo pia inaweza kuchangia kisasi na matukio mengi. Watu walikuwa kwenye mazungumzo wakapishana kauli mmoja ananyanyua jiwe au chupa na kumrushia mwenzake. "Tuidhibiti hali hiyo na iwe ni utaratibu kwenye maisha yetu ya kila siku."

Ripoti ya LHRC kuhusu haki za binadamu kwa mwaka 2021/22, inazungumzia haki ya kuishi inavyokiukwa kutokana matukio kadhaa hasa ongezeko la mauaji yatokanayo na wivu wa kimapenzi.


Ripoti hiyo inasema, wanawake ndiyo waathiriwa wakuu wa matukio ya ukatili wa kijinsia, wanauawa na wapenzi wao kwa sababu ya wivu wa mapenzi, ingawa takwimu zinabainisha pia wanaume ambao wanaongoza kwa kuchukua maamuzi magumu ya kujiua.

Kadhalika, takwimu za Shirika la Afya Dunani (WHO), zinaonesha kwamba Watanzania milioni saba, wana tatizo la afya ya akili wengi wao wakiishi Dar es Salaam.

Pia kuna mtu mmoja hufariki dunia katika kila sekunde 40 kutokana na kujiua.

Aidha, takwimu za LHRC kuhusu haki za binadamu mwaka 2021, inabainisha kwamba watu wanne kati ya 10 waliojiua mwaka jana (2021) walikuwa ni vijana wenye umri kati ya miaka 15 hadi 35.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Beatrice Moses

## Muungwana Lazima Nilonge

# Mvua, jua zinavyowatesa abiria wa vituo vya daladala vya Dar

**MATESO** wanayokumbana nayo baadhi ya wakazi wa Dar es Salaam wanaotumia usafiri wa umma, iwe daladala au mwendo kasi ni mengi. Hii ni pamoja na kupambana kupata kiti, mlundikano wa abiria, lugha za maudhi kutoka kwa makondakta na yanayofanana nayo.

Wakazi hao pia hasa wanaotumia usafiri wa daladala wanakumbana na foleni, ambayo huwachelewesha kwenye shughuli zao za muhimu, wakati mwingine baadhi yao hulazimika kuamka mapema ili kufidia muda unaoliwa na foleni.

Pamoja na hayo, kuna kero nyingine kubwa ambayo inawakabili baadhi ya wasafiri hao wakiwamo wanafunzi wa ngazi zote na wagonjwa, ni kukosekana majengo ya vituo vya daladala na mwendo kasi katika baadhi ya maeneo.

Hali ya kukosekana miundombinu hiyo, watumiaji wa usafiri hujikuta katika wakati mgumu, maana wakati wa jua wanapokuwa wanasubiri magari linawachoma, pia wakati wa mvua nao ni mateso, maana hakuna mahali pa kujisitiri. Wanaweza kuwa salama bila kuloweshwa na mvua.

Hali hiyo kwa namna fulani inazua maswali mengi kwa mfano katika Barabara ya Morogoro, jijini Dar es Salaam ambako barabara ya mabasi ya mwendo kuna vituo maalum kuanzia Kivukoni au Gerezani hadi Kimara na baada ya hapo kuendelea mbele ya Stop Over Kimara, hakuna jengo la kituo hadi ukifika Mbezi Mwisho.

Hapo Mbezi Mwisho, mabasi ya mwendo kasi yanatumia kituo cha kawaida, japo ni wazi kuwa kuna gharama katika kujenga majengo ya vituo vya mabasi, kunaweka abiria salama dhidi ya mvua na jua. Ni mamlaka husika zikawathamini wasafiri, kama ilivyofanywa kwa wafanyakazi wa mwendo kasi kujengewa vibanda maalum.

Awali, wafanyakazi hao nao walisota kwa kuwa hakukuwapo majengo ya ofisi na walilazimika kutoa huduma za kukatisha tiketi kwenye jua na mvua. Serikali iliona mateso yao, ikajenga vibanda maalum ambavyo kwa hakika vinawasitiri sasa, abiria wengine nao waonewe huruma vituo vijengwe.

Kuna kitengo cha miundombinu ambacho pamoja na majukumu mengine, kinawajibika kutoa huduma za kitaalamu zinazohitajika kwa mamlaka za serikali za mitaa, katika kuendeleza miundombinu.

Vitengo vya miundombinu ndiyo vyenye majukumu kadhaa ikiwamo ya kuratibu utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni na Viwango katika nyanja za Barabara, Majengo, Upimaji, Ardhi na Mipangomiji.

Pia, inawajibika kuzijengea uwezo mamlaka za serikali za mitaa katika nyanja za barabara, majengo, upimaji, ardhi na mipangomiji na kuwasiliana, kuwa daraja kuunganisha baina ya mamlaka zinazohusika kwenye serikali kuu na mamlaka za serikali za mitaa juu, ya masuala ya ujenzi.

Kitengo hicho pia kinawajibika katika kushauri masuala ya barabara, ujenzi, viwanja na uboreshaji mifumo na kusimamia na kushauri juu ya kazi za ujenzi zinazotekelezwa ndani ya mkoa, pia kuzisaidia mamlaka za serikali za mitaa kutwaa ardhi, kwa ajili ya matumizi ya serikali kuu.

Nimelazimika kuitaja 'seksheni' hii ili kukumbusha jinsi gani ambavyo wakazi wa maeneo tofauti Dar es Salaam, wanavyoteseka hivyo ione umuhimu na ichukue hatua ya kuhakikisha, kuwa vituo pia vinajengwa, ili wananchi wapate huduma ya usafiri angalau vinavyojali afya zao, kwa namna fulani.

Nimetolea mfano barabara ya Morogoro, lakini ukweli ni kwamba, kwa sasa imekuwa desturi barabara zinajengwa mpya na hakuna majengo ya vituo vya kusitiri abira kwa jua wala mvua, ni kama vile havionekani kuwa ni muhimu kulinganishwa na madaraja au mirefeji .

## Bilioni 1.7/- kutatua kero uhaba wa maji vijiji vitano

**Na Gurian Adolf,** KALAMBO

ZAIDI ya wakazi 25,000 wa Kata ya Mbuluma wilayani Kalambo mkoani Rukwa wataondokana na adha ya kuamka usiku wa manani na kutembea umbali mrefu kutafuta maji baada ya serikali kutoa Sh. bilioni 1.7 kwa ajili ya mradi wa bwawa la maji kwenye Kijiji cha Kalemasha wilayani humo.

Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Kalambo ilibainisha hayo jana ilipofanya ziara kukagua maendeleo ya ujenzi wa mradi huo na kuridhika na kasi yake, ikieleza kuwa ukikamilika, utatoa huduma kwa wakazi wanaoishi kwenye vijiji vitano vya kata hiyo.

Akizungumza kwenye eneo la mradi huo, Mkuu wa Wilaya hiyo, Tano Mwera, alisema fedha zinazotumika kujenga mradi huo, zimetolewa na Mfuko wa Maji wa Taifa na kwamba awamu ya kwanza inahusisha ujenzi wa miundombinu ya maji itakayotoa huduma kwa wakazi wa vijiji vitano vya Kata ya Mbuluma.

"Ujenzi wa miundombinu ya bwawa unafanywa na Kampuni ya Chelesi General Entreprises Limited na gharama za mkataba ni Sh. bilioni 1,771 ambapo ujenzi wake unatarajia kukamilika Juni 30, 2023," alifafanua Mwera.

Awali akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi huo, Kaimu Meneja wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) wilayani Kalambo, Francis Mpunda, alibainisha kuwa mpaka sasa Sh. milioni 192.062 zimetumika.

Aliutaja mradi huo kuwa ni wa ukombozi kwa wakazi wa vijiji hivyo wanaokabiliwa na adha ya uhaba wa maji kwa muda mrefu.

Kaimu Mkurugenzi huyo alisema wana jukumu la kumsimamia mkandarasi ili atekeleze mradi huo kwa wakati, kwa thamani halisi ya fedha na kwa ubora wa hali ya juu ili mradi ulete tija kwa wananchi na utumike kwa muda mrefu na tatizo la maji ilibaki historia kwenye kata hiyo.

Mmoja wa wakazi wa kijiji hicho, Mariana Richard, aliishukuru serikali kwa kutekeleza mradi huo, akiutaja kuwa utayabadili maisha yao kwa kuwa walikuwa wakipitia vikwazo vingi ikiwamo kuamka nyakati za usiku kwenda kutafuta maji, pia kuibuka kwa migogoro baina ya wanandoa kwa kuwa muda mwingi wanawake wanautumia kutafuta maji.



Diwani wa Kata ya Naisinyai wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, Taiko Laizer (kulia), akiwakabidhi cheti cha kutambua mchango wao kwa jamii viongozi wa Shirika lisilo la Kiserikali la AKO Tanzania Community Support, linavyosaidia vijiji vya Kambi ya Chokaa na Lengasti juzi, kushoto ni Mkurugenzi wa shirika hilo, Hilda Kimath. **PICHA: GIFT THADEY**

# Anayedaiwa kuchoma moto mwili wa mkewe aomba atete na hakimu

**Na Grace Gurisha**

MFANYABIASHARA Khamis Luwonga (38) anayetuhumiwa kumuua mkewe, Naomi Marijani kwa kumchoma moto kwa kutumia magunia mawili ya mkaa, amemwomba hakimu amsaidie aonane na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam.

Luwonga aliwasilisha maombi hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rhoda Ngimilanga, kwa njia ya mtandao wakati kesi yake ya mauaji ilipoletwa kwa ajili ya kutajwa na kuangalia hatua ya upelelezi ulipofikia.

"Mheshimiwa hakimu, ninaomba nisaidie nionane na Mfawidhi wa Mahakama hii, "alidai Mshtakiwa Luwonga.

Akijibu ombi hilo, Hakimu Ngimilanga alimweleza mshtakiwa kuwa anachokisema utaratibu upo wazi, anachotakiwa ni kuandika barua kisha aipeleke kwa mfawidhi, naye akishaipata atatoa maelekezo, hivyo yeye hana utaratibu wa kumsaidia.

Baada ya Hakimu Ngimilanga kusema hayo, aliahirisha kesi hiyo hadi Januari 13 mwakani kwa ajili ya kutajwa na kuangalia hatua iliyofikiwa katika upelelezi. Awali Wakili wa Serikali, Faraja Ngukah, aliiomba mahakama hiyo ipange tarehe nyingine ya kutajwa kwa kesi hiyo kwa kuwa upelelezi haujakamilika.

Mshtakiwa Luwonga alidai mke wake Naomi kila siku alikuwa anamwomba Mungu afe kuliko kuendelea kuishi katika ndoa yao na alikuwa anang'ang'ania kifo chake kwa nguvu, hivyo kwa sasa mtoto wao anaishi bila wazazi.

Pia alidai kifo cha Naomi hakikusababishwa na yeye peke yake, bali kuna watu wengine waliohusika zikiwamo familia za pande zote mbili, maofisa wa polisi na watumishi wa ngazi za chini serikalini.

"Kama tukio nililoshtakiwa nalo Watanzania wanaaangalia uharibifu uliotokea, hawaangalii chanzo nini, nina maumivu makubwa sana ya kifo cha mke wangu kipenzi Naomi kwa sababu baadhi ya watu wanaodharau matukio.

"Walipaswa kuzuia mambo ya hatari kutokea na siyo kusubiri uharibifu kutokea. Hata vitabu vya dini vinaeleza hayo, kwenye Quran na kwenye Biblia ukisoma utaona ninachokizungumza kwamba ukimwona mtu anataka kukengeuka, unamweka sawa," alidai Luwonga.

Alidai siyo yeye peke yake anayehusika na kifo cha mke wake, akiituhumu familia yake, familia ya mkewe, baadhi ya maofisa wa polisi, watumishi wa chini wa serikali na jamii kwa ujumla kwa kushindwa kufanya uamuzi.

Katika kesi hiyo ya mauaji namba nne ya mwaka 2019, mshtakiwa Luwonga ambaye ni mkazi wa Kigamboni, Dar es Salaam, anadaiwa Mei 15, 2019, akiwa Gezaulole eneo la Kigamboni, alimuua Naomi Marijani.

Mshtakiwa huyo anadaiwa kumuua mkewe, Naomi, kisha kumchoma moto kwa kutumia magunia mawili ya mkaa na baadaye kuchukua majivu ya mwili huo na kwenda kuyafukia shambani kwake.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# Jela miaka 30 kwa kumnajisi binti wa umri wa miaka 16

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKAZI wa Kijiji cha Geilailumbwa wilayani Longido mkoani Arusha, Lemindia Lesiria amehukumiwa kutumikia kifungo cha miaka 30 gerezani baada ya kutiwa hatiani kwa kosa la kumnajisi msichana mwenye umri wa miaka 16.

Lesiria alihukumiwa kutumikia adhabu hiyo jana na Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha. Hukumu hiyo ilisomwa na Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Regina Oyier aliyekuwa anasikiliza shauri hilo.

"Mahakama hii imekutia hatiani mshtakiwa Lemindia Lesiria katika kosa la kubaka ambalo ni kinyume cha kifungu cha 130(1), (2)(e) na 131(1), (3) vya Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2002," alisema.

Katika hukumu hiyo, Hakimu Oyier alisema mshtakiwa Lesiria na mshtakiwa mwenzake, Kulasa Mandeu walitenda kosa hilo na walisababisha majeraha kwa msichana huyo baada ya kumnajisi.

Ilidaiwa mahakamani huko kuwa washtakiwa hao walitenda kosa hilo la kujeruhi kwa fimbo kabla ya kumnajisi mtoto huyo Septemba 14 mwaka huu.

Kosa hilo la kushambulia na kujeruhi ni kinyume na kifungu cha 225 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai.

Kwa mujibu wa Hakimu huyo, mahakama hiyo imewatia hatiani katika makosa yote matatu, baada ya ushahidi wa upande wa mashtaka kuthibitisha makosa hayo pasipo na shaka.

Alisema, mahakama hiyo imemhukumu mshtakiwa wa pili, Kulasa Mandeu kifungo cha miaka mitano gerezani kwa kila kosa na kulipa faini ya Sh. milioni mbili kama fidia ya kumjeruhi msichana huyo.

Hakimu Oyier alisema kosa la kujeruhi kwa kumchapa viboko msichana huyo ni kinyume cha kifungu cha 225 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai.



Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Geita wakiwa wameuchukua mwili wa marehemu Benjamini John baada ya kuuopoa kwenye Mto Nyapa Mtaa wa Nyapa Kasamwa, Mkoa wa Geita jana. **PICHA: JOCTAN NGELLY**

# Fundi ujenzi afa maji akivuka mto kwenda kujenga

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

FUNDI ujenzi, Benjamin John (30), amekufa maji baada ya kuzama kwenye mto Nyapa wakati akivuka kwenda kujenga nyumba Mtaa wa Nyapa Kasamwa, mkoani Geita.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kaimu Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji mkoani hapo, Edward Lukuba alisema, tukio hilo lilitokea Desemba 28, majira ya saa mbili asubuhi eneo la Kasamwa.

Alisema askari wa Zimamoto walipata taarifa majira ya saa sita mchana na kufika eneo la tukio kumtafuta, lakini hawakufanikiwa kumpata kutokana na maji kuwa mengi.

Lukuba alisema Desemba 29, saa moja asubuhi walifanikiwa kuuona mwili ukielea juu ya maji na askari wa Zimamoto waliutoa mwili na kuupeleka katika Kituo cha Afya Kasamwa, Wilaya ya Geita kwa uchunguzi zaidi."Mtu kazama maji Desemba 28 mwaka huu majira ya saa mbili asubuhi wananchi walijaribu kumtoa baada ya kushindwa ndipo wakatoa taarifa kwetu sisi Jeshi la Zimamoto na Uokoaji majira ya saa sita mchana kitendo hicho kinafanya mtu kupoteza maisha yake, lakini taarifa ingetolewa mapema kwenye Jeshi la Zimamoto lingeweza kuyaokoa maisha yake kwa wakati," alisema.

Kaka wa marehemu Zakayo John (36) alisema mdogo wake alikuwa anavuka Mto Nyapa kwenda kujenga nyumba, lakini alipoingia ndani ya mto huo maji yalimzidi nguvu na kuzama.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Nyapa, Kasamwa Maneno (52) alisema alipata taarifa majira ya saa tatu asubuhi na kukuta Benjamin akiwa ameshazama maji.

Alisema matukio ya watu kuzama kwenye mto huo ni tukio la saba, ameiomba serikali kujenga daraja ili kuokoa maisha ya watu kwa sababu wakazi wa wengi wa Kasamwa wanalima pembezoni mwa mto huo.

Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Kasamwa, Dk. Emmanueli Alex, alithibitisha kupokea mwili wa marehemu Benjamin.

# TRA Kariakoo yazindua kampeni kuelimisha wanunuzi kudai risiti

**Na Mwandishi Wetu**

MENEJA wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Kikodi Kariakoo, Alex Katundu amezindua kampeni ya 'Twende Nao Tukawaelimishe' yenye lengo la kuwaelimisha wanunuzi kuhusu umuhimu wa kudai risiti za kielektroniki (EFD) kila wanaponunua bidhaa kwenye eneo la kibiashara la Kariakoo.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam wakati akitoa elimu ya umuhimu wa kudai risiti kwa wanunuzi waliokutwa wamenunua bidhaa bila kudai risiti, meneja huyo amesema elimu ya kodi imekuwa ikitolewa mara kwa mara kwa wafanyabiashara, itakuwakumbusha wanunuzi wengi kutosahau wajibu wao wa kudai risiti.

"Mara nyingi tumekuwa tukitoa elimu kwa wafanyabiashara kuhusu matumizi sahihi ya mashine za kutolea risiti za EFD na sasa hivi tumekuja na mkakati maalum wa kuwaelimisha wanunuzi juu ya haki yao ya kudai risiti kila wanapofanya ununuzi," alisema.

Meneja Katundu alisema kampeni hiyo itafanyika kwa kuwakusanya wanunuzi wote watakaokutwa wamenunua bidhaa bila kuwa na risiti na kupelekwa kwenye Ofisi ya TRA Kariakoo iliyoko Mitaa ya Lumumba na Kipata, Dar es Salaam kwa ajili ya kuwaelimisha.

"Kwa kuwa wanunuzi hawa wanakutwa katika maeneo mbalimbali ya Kariakoo, hivyo kazi hii inafanyika kwa kuwakusanya wote wanaokutwa wamenunua bidhaa lakini hawana risiti ambapo wanaletwa hapa ofisini kwa ajili ya kuwaelimisha na kuwaomba wawe mabalozi kwa wengine wenye tabia ya kutokudai risiti," alifafanua Katundu.

Alisema elimu hiyo itakuwa ikitolewa bure kwa kuwaeleza wanunuzi umuhimu wa kudai risiti ili kuepuka adhabu ya faini ya Sh. 30,000 hadi sh. milioni 1.5.

Mmoja wa wanunuzi wa bidhaa Kariakoo, Elizabeth Kimaro alitoa wito kwa wanunuzi wenzake wenye tabia ya kutokudai risiti, kutumia haki na wajibu wao wa kudai risiti kwa maendeleo ya taifa.

## Wananchi walia na uporaji ziwani

**Na Gurian Adolf,** NKASI

BAADHI ya wakazi wa vijiji vilivyoko mwambao wa Ziwa Tanganyika mkoani Rukwa, wameiomba serikali mkoani hapa kukomesha ujambazi unaoonekana kuanza kushamiri siku hadi siku katika maeneo yao.

Ombi hilo walilitoa juzi wakati wa mkutano wa hadhara uliofanyika katika kijiji cha Lyapinda, kata ya Kizumbi wilayani hapa wakati Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Queen Sendiga, akisikiliza kero mbalimbali zilizoibuliwa katika mkutano huo na kuwapatia majibu.

Mmoja wa wakazi hao, Paul Chizya, alimwambia mkuu huyo wa mkoa kuwa hivi sasa kumekua na vitendo vya ujambazi katika kata za Wampembe, Kirando na Kabwe wilayani Nkasi na inadhaniwa kuwa watu kutoka mataifa jirani wamekuwa wakifanya ujambazi huo.

Alisema, kata hizo ziko mwambao wa Ziwa Tanganyika na wakazi wake ni wavuvi na kwamba wamekuwa wakivamiwa na majambazi wanapokuwa ziwani wakivua samaki na kuporwa vyombo vyao vya uvuvi pamoja na mali mbalimbali.

"Majambazi hao wanatuteka tukiwa ziwani, wanatupora vyombo vyetu vya uvuvi pamoja na mali nyingine, kitendo kinacholeta hofu pindi tunapofanya shughuli zetu ziwani. Tunaiomba serikali ya mkoa ikibidi itumie Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) ili lipambane na majambazi hao na kuwamaliza kabisa," alisema Chizya.

Kutokana na hoja hizo, Sendiga aliwahakikishia wananchi hao kuwa serikali kamwe haitakubali majambazi waendelee kufanya vitendo vya kihalifu na iko makini katika kushughulikia kero hiyo na itawamaliza kabisa.

Pia aliitaka Idara ya Uhamiaji Mkoa wa Rukwa kuhakikisha inawadhibiti watu wanaoingia nchini kinyume cha sheria kwa kuwa, baadhi yao ndio wanaofanya vitendo hivyo.

Mkuu huyo wa mkoa aliwataka wananchi wanaoishi vijiji vya mwambao na vile vilivyoko mpakani kuacha kuwapokea wageni wanaotoka nchi jirani kwa kuwa baadhi yao ndio wanaofanya vitendo vya ujambazi.



Mwenyekiti wa kikundi cha wajasiriamali wa kutengeneza majiko eneo la Majengo, Kipara Ally, akiwa na wenzake kwenye eneo lao la kazi jijini Dodoma jana, wajasiriamali hao wanaomba uongozi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma kuwasaidia eneo la kudumu la kufanyia shughuli zao. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Serikali kuwapanga upya wananchi waliovamia eneo Hifadhi Nanyumbu

**Na Munir Shemweta,** NANYUMBUNA

SERIKALI imeamua kuwapanga upya wananchi wa vijiji vya Mbagala Mbuyuni na Marumba. Nanyumbu mkoani Mtwara ili kutatua migogoro ya matumizi ya ardhi na kuleta usalama kwenye maeneo hayo.

Akizungumza na wananchi wa kitongoji cha Wanika kata ya Mkonona wilayani hapa juzi wakati wa ziara ya mawaziri wa wizara za kisekta, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, alisema kitakachofanyika kila kijiji kitapewa utaratibu utakaosimamiwa na mkuu wa mkoa atakayewapanga wananchi wake na kuyaacha maeneo ambayo si salama kukaliwa na wananchi huku akisisitiza hakuna haki ya mtu itakayopotea.

"Mheshimiwa Rais (Samia Suluhu Hassan) anatambua tunayo shule yenye madarasa matatu na hapa tulipo kuna kaya 94 ambazo ziko hapa na ukienda kitongoji jirani ziko kaya 134, hivyo serikali inajua idadi ya watu kwenye maeneo hayo na mahitaji yao," alisema.

"Timu ya mawaziri wanane wa wizara za kisekta inazunguka nchi nzima kuzungumza na wananchi sambamba na kuwafahamisha dhamira njema ya serikali yao katika kuhakikisha inalinda usalama wao pamoja na usalama wa mipaka ya nchi," aliongeza.

Kwa mujibu wa Dk. Mabula ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Mawaziri Wanane wa Wizara za Kisekta, serikali itafuata utaratibu mzuri wa kuwapanga wananchi wa maeneo hayo kwenye vijiji husika ili kila mtu aendelee na maisha yake bila tatizo. "Kama Mheshimiwa Rais ametoa kinachostahili, kipi ambacho kitakuwa kimebaki? Ikolojia tunataka kuiona inavyokwenda ninyi wote ni mashahidi ukipita huko kina cha maji kinazidi kupungua, kuna mahali unaona mchanga ni kwa sababu shughuli za kibinadamu zimeenda katika vyanzo vya maji," alisema Dk. Mabula.

Awali, wananchi wa Nanyumbu waliieleza kamati ya mawaziri wa kisekta kuwa wamepokea maelezo na kusubiri kitakachofanyika.

Mkazi wa kitongoji cha Wanika, Othman Said, maarufu kama Gonga, alibainisha kuwa anaishi kwenye vijiji hivyo kama nyumbani lakini pia kama walinzi na kueleza kuwa huko nyuma waliwahi kuwakamata watu waliodhaniwa kuwa ni al Shabab.

Mkuu wa Wilaya ya Nanyumbu, Mariam Chaurembo, aliwaambia wananchi wa wilaya hiyo uamuzi wa serikali kupanga upya vijiji, utatoa nafasi kwao kuanza kufanya shughuli za uchumi maeneo sahihi na kubainisha kuwa vijiji vitatengenezewa matumizi bora ya ardhi kwa lengo la kubainisha maeneo ya kilimo na ufugaji.

Awali, akizungumza na uongozi wa mkoa wa Mtwara, Dk. Mabula alisema mkoa huo unahusisha migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji na mitaa 12 iliyoainishwa sehemu kuu tatu kulingana na aina ya mgogoro.

Aliitaja sehemu ya kwanza kuwa, ni vijiji na mitaa 10 ambayo wananchi wake wataondolewa kwenye eneo la hifadhi na shamba la MATI na TARI huku sehemu ya pili ikihusisha kijiji kimoja ambacho mgogoro wake wa mipaka na hifadhi umerejewa kwa njia shirikishi kati ya halmashauri ya wilaya ya Masasi, halmashauri ya kijiji cha Chingulungulu na wataalamu wa Pori la Msanjesi lilipo chini ya TAWA.

# Watu wanaoishi na ukoma wapewa msaada

**Na Thobias Mwanakatwe,** MKALAMA

WATU 140 wanaoishi na ugonjwa wa ukoma katika kijiji cha Nungwi, Mkalama mkoani Singida, wamepewa msaada wa vyakula na mavazi ili kusherehekea sikukuu ya kuukaribisha Mwaka Mpya wa 2023.

Vitu vilivyotolewa ni pamoja na mahindi, mchele, sabuni, sukari, nguo na mashuka ya kujifunika. Msaada huo umetolewa na ofisi ya Mkuu wa Wilaya Mkalama, Mkurugenzi wa Halmashauri na Kanisa la Maranatha lililoko Nduguti.

Akikabidhi vifaa hivyo, Mkuu wa Wilaya ya Mkalama, Sophia Kizigo, alisema msaada huo umelenga kuhakikisha wenye ukoma hao wanasherehekea sikukuu hiyo kwa furaha na amewatia moyo kwa kuwataka kutokata tamaa kutokana na changamoto waliyonayo kwani tatizo hilo linaweza kumpata yeyote. Kizigo alisema, wako watu wenye ulemavu unaoonekana na usioonekana hivyo, jamii inapaswa kuishi na watu hao kwa usawa na kutowanyanyapaa kwa namna yoyote.

"Nimedokezwa na mwenyekiti wenu hapa kuwa mmetoka kujishughulisha, hivyo niwapongeze sana kwani pamoja na hali mliyonayo, bado mnajishughulisha na uzalishaji mali, kazi ambazo kwa kiasi kikubwa zinachangia maendeleo ya wilaya ya Mkalama na taifa kwa ujumla," alisema.

Baadhi ya wanufaika wa msaada huo, Helena Samweli na Ilanda Salehe, waliushukuru uongozi wa wilaya ya Mkalama kwa kuwapelekea msaada huo na kuwaomba wasisite kufanya hivyo wanapopata nafasi kwa kuwa, kitendo hicho kimewafanya wajisikie wenye furaha na kuthaminiwa na viongozi wa ngazi za juu.

Uongozi wa Wilaya ya Mkalama kwa kushirikiana na wadau wake mbalimbali umekuwa na utamaduni wa kuwatembelea na kuwapeleka misaada kwa jamii hiyo ambayo imekuwa ikiishi na changamoto ya kuathiriwa na ugonjwa wa ukoma kwa muda mrefu.

# China kuanza tena kutoa pasipoti, visa kuanzia Januari 8, 2023

**Na Mwandishi Maalum**

CHINA itaboresha sera na hatua za usimamizi wa uhamiaji kuanzia Januari 8, 2023 kwa kutilia maanani hatua za kukabiliana na UVIKO-19 nchini humo.

Idara ya Taifa ya Uhamiaji ya China imetoa taarifa Desemba 27, mwaka huu, ikisema kwamba sera na hatua zilizoboreshwa ni pamoja na kuanza tena kukubali na kuidhinisha maombi ya raia wa China ya pasipoti za kawaida kwa madhumuni ya utalii na kutembelea marafiki nje ya nchi kuanzia tarehe hiyo. Kwa mujibu wa taarifa ya tovuti ya gazeti la umma nchini humo, Idara hiyo pia itaanza upya mchakato wa uidhinishaji kwa wakazi wa China Bara kutembelea Mkoa wa Utawala Maalum wa Hong Kong kwa madhumuni ya utalii na biashara, pamoja na kutoa vibali vya kutoka na kuingia vya Jamhuri ya Watu wa China na vibali vya kutoka na kuingia kwa maeneo ya udhibiti wa mpaka.

Huduma zinazohusiana na maombi ya visa za kawaida, vibali vya ukaazi na vibali vya kuishi kwa wageni zitarejeshwa, taarifa hiyo imesema, huku ikiongeza kuwa taratibu za kuharakishwa zinaweza kutumika ikiwa kuna uhitaji wa dharura.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, huduma zitakazorejeshwa pia zitajumuisha utoaji wa visa kwenye bandari, utekelezaji wa sera ya usafiri wa visa bila malipo ya saa 24/72/144, na utoaji wa vibali vya muda vya kuingia.

China pia itashuhudia urejeshaji wa taratibu wa huduma zinazohusiana na kibali cha abiria kuruhusiwa kupita kwenye bandari na njia za ardhi, pamoja na kutoka na kuingia kwa abiria na wakazi wa mpaka kupitia bandari za ardhi na korido kwa wakazi wa mipakani. Njia za haraka katika bandari zilizo karibu na mikoa ya utawala maalum ya Hong Kong na Macao zitarejea katika shughuli za kawaida, imesema taarifa hiyo. Na uhudumiaji wa abiria kwenye bandari za majini, pamoja na kutoka na kuingia kwa abiria wa kimataifa kwenye bandari zilizochaguliwa, utaanza tena kwa utaratibu.



Mkazi wa Mtaa wa Muhongolo Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Naomi Kusekwa, akieleza namna wanavyofanyiwa vitendo vya ukatili na waume zao ndani ya familia, wakati wa kampeni ya mtaa kwa mtaa ya kutoa elimu ya ukatili iliyoandaliwa na Ofisi ya Ustawi wa Jamii Kahama jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

## Wazazi wanaolazimisha watoto tohara za kienyeji waonywa

**Na Samson Chacha,** TARIME

MKUU wa Wilaya ya Tarime mkoani Mara, Kanali Michael Mtenjele, amekemea vitendo vinavyofanywa na baadhi ya wazazi katika Tarafa ya Ingwe kuwapeleka watoto wao wa kiume waliopata tohara vituo vya afya na kuwalazimisha kuwarejesha kufanyiwa upya ya kimila.

Akikemea vitendo hivyo, Mkuu huyo aliyeongozana na Kamati ya Ulinzi na Usalama, alisema serikali inatoa elimu kwa vijana ambao hawajapata na wanaotaka kufanyiwa tohara kwenda katika vituo vya afya ili kujiepusha na magonjwa hatari yakiwamo Ukimwi.

Kanali Mtenjele alisema: "Tunasikitishwa na baadhi ya wazazi ambao vijana wao wamefanyiwa tohara salama katika vituo vya afya na wengine wameelekea kupona na wanaambiwa kwenda kufanyiwa tohara za kimila upya, huo ni ukatili mkubwa kwa vijana hao tunawaonya wazazi serikali itawachukulia hatua kali za kisheria."

Alisema mzazi yeyote atakayebainika na kukamatwa akimlazimisha mtoto wake wa kiume aliyekwisha fanyiwa tohara salama kwenda kufanyiwa kwa mara ya pili kienyeji hatavumiliwa.

Pia alisema zaidi ya wasichana 400 wanaopinga unyanyasaji wamekwepa kufanyiwa ukeketaji wakiwamo wanafunzi waliokimbia nyumbani kwao na kwenda kuhifadhiwa katika kituo cha kulelea watoto wanaoishi katika mazingira magumu na yatima cha Kanisa Katoliki, Masanga Tarafa ya Ingwe na wanapata mafunzo mbalimbali yakiwamo ya kujikinga na ukatili wa kijinsia, ukeketaji na wengine kuendelea na masomo katika kituo hicho.

# TRA yawashukuru walipakodi, yakusanya bil. 16.4/-

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), Mkoa wa Iringa imewashukuru wadau wake walipakodi kwa ushirikiano katika matukio mbalimbali kwa mwaka 2022.

TRA imefanikiwa kukusanya Sh. bilioni 16.4 kwa robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2022/23, wakati lengo lilikuwa ni kukusanya Sh. bilioni 16.1.

Hayo alibainishwa na Meneja wa TRA Mkoa wa Iringa, Paul Walalaze, wakati akitoa salamu za kuuaga mwaka 2022 na kuukaribisha Mwaka Mpya 2023 kwa wateja wake jana.

Akizungumza na Nipashe, alisema kwa mwaka 2022, TRA ilipata ushirikiano mkubwa kutoka kwa wadau na kuomba uendelee hadi mwaka mpya 2023 ili kujenga taifa kwa kulipa kodi.

Walalaze alifafanua kuwa wamefanya matukio ya kielimu pamoja na kusikiliza kero mbalimbali kutoka kwa walipakodi kwa mwaka 2022.

Alisema ushirikiano walioupata kutoka kwa wadau hao umewapatia mwanga wa kukusanya kodi kwa robo ya mwaka fedha 2022/23, ambao wanaendelea kutekeleza. "Mwaka wa fedha wa serikali unaanza Julai mosi, 2022 hadi Juni 30, 2023, tunapokwenda kuuaga mwaka 2022, napenda kuwaasa walipakodi kwamba kila wanapokwenda kufanya manunuzi yoyote wadai risiti na risiti hizo ziwe za kielektroniki (EFD) kulingana na thamani ya fedha walioitoa," aliwakumbusha.

Kwa wauzaji TRA inasisitiza kuwa lazima watoe risiti kulingana na mauzo yanayofanywa na kuongeza kuwa kutofanya hivyo ni kukwepa kodi. "Ziko faini ambazo zinaambatana na kutotoa risiti sahihi kwa muuzaji kutokana na mauzo na pia faini zinazoambatana na mtu ambaye hadai risiti pindi anapofanya manunuzi," alisema Meneja wa TRA.

Ili kupuekana na watu kulipa faini, TRA imekuwa ikitoa elimu ya mlipakodi mara kwa mara ili kuwawezesha watu kulipa kodi kwa hiari (tax compliance) ili kujenga taifa, alisema Walalaze.

"Ikumbukwe kwamba taifa haliwezi kujengwa na watu wengine mbali ni sisi wenyewe Watanzania kulipa kodi mbalimbali," alisema.

Tunapoenda kuuaga mwaka 2022, TRA inawakumbusha wadau wote kulipa kodi ya mapato ya awamu ya nne, ikumbukwe kwamba kodi hizi zinalipwa wa awamu, awamu ya kwanza inalipwa mwezi Machi, wa pili inalipwa mwezi Juni, ya tatu mwezi Septemba na awamu ya nne inalipwa Desemba 31," Walalaze alifafanua.

"Tunawahimiza wana Iringa wote, wafanyabiashara na walipakodi wote kujitokeza kulipa kodi kwa ajili ya maendeleo ya taifa. Njooni ofisini kuangalia madeni yenu ambayo ni miaka ya nyuma na miezi ya nyuma ili kujua kiasi unachodaiwa na upewe control namba ya malipo," aliwakumbusha. Alisema mwaka 2023 ni wa EFD kwa kudai risiti kutokana na ununuzi na kutoa risiti kulingana na mauzo yote yanayofanyika.



# Kibano wenyeviti vijiji, mitaa wanaouza adhi kihuni chanukia

**Na Hamida Kamchalla,** HANDENI

KIBANO dhidi ya wenyeviti wa serikali za vijiji na mitaa wanaouza ardhi kinyume na utaratibu na kusababisha migogoro kinanukia.

Mpango wa kuwabana viongozi hao unatarajia kuanza Januari mosi mwaka ujao, ulitangazwa jana na Mkuu wa Wilaya ya Handeni, mkoani Tanga, Siriel Mchembe.

Mchembe alitangaza utaratibu huo alipokwenda Kijiji cha Taula wilayani humo kutatua mgogoro wa ardhi uliokuwa ukitishia uvunjifu wa amani.

"OCD (Mkuu wa Polisi wa Wilaya), wasake, wakamate na kuwachukulia hatua za kisheria viongozi wa vijiji, kata na wananchi wote ambao wanauza maeneo yao kinyume na utaratibu na kusababisha migogoro kila uchao.

"Kama kuna mtu yeyote umeuziwa eneo la mtu mwingine hapa, mkabe aliyekuuzia akurudishie pesa yako. OCD, mtu aliyetapeliwa ardhi hapa Taula na Kwedizinga, mkamate aliyetapeli weka ndani, fungua kesi. Hatutaki migogoro Taula, tunataka maendeleo," alisema

Katika kikao hicho cha utatuzi wa migogoro ya ardhi, Mkuu wa Kituo cha Polisi Mkata, Juma Wandi, aliwaonya wanaojihusisha na kuuza ardhi kinyemela, hasa ngazi ya familia kufuata taratibu za uuzaji wa ardhi.

"Mheshimiwa DC (Mkuu wa Wilaya), migogoro mingi ya Taula na Kwedizinga, inatokana na kudhulumiana. "Inatokea wengine mnadhulumu mali za watoto wa ndugu zenu walioachwa na wazazi wao, kwa sababu tu wewe una mamlaka kwenye ile familia. Haiwezekani, tutakufunga."

Kutokana na kuchipua kwa kasi kwa migogoro hiyo, Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Wilaya ya Handeni, Richard Mpungu, alisema wameanzisha dawati la uchunguzi kuhusu madai ya kuwapo vibali vya kughushi vya uuzwaji wa ardhi, ambavyo huandaliwa na viongozi, bila kuwashirikisha wananchi wao.

# Wanne wakamatwa wakisafirisha kilo 304 za mirungi

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

JESHI la Polisi mkoani Manyara linawashikilia watu wanne kwa kosa la kukutwa wakisafirisha dawa za kulevya aina ya mirungi bunda 661 ambazo ni sawa na kilogramu 304.10.

Watuhumiwa hao walikuwa wakisafirisha dawa hizo za kulevya kutoka Mkoa wa Arusha kwenda Wilaya ya Kondoa, mkoani Dodoma.

Jana Kamanda wa Polisi wa mkoani humo, Kamishna Msaidizi (ACP), George Katabazi, alithibitisha kukamatwa kwa watuhumiwa hao.

Kwa mujibu wa Katabazi watuhumiwa hao walikamatwa wakati wa operesheni ya kusaka wauzaji wa dawa za kulevya.

"Ni kweli juzi tulikamata dawa za kulevya aina ya mirungi na watuhumiwa wanne pamoja na magari mawili. Tuliwatia mbaroni majira ya saa 10:45 usiku katika kizuizi cha Minjingu kilichoko Kata ya Nkaiti, Wilaya ya Babati," alisema.

"Askari wakiwa katika upekuzi wa magari walifanikiwa kuwakamata watuhumiwa wawili wote wanaume," alisema Katabazi.

Aidha, alisema watuhumiwa walikuwa wameficha dawa hizo kwenye eneo la mfumo wa viyoyozi vya basi hilo, mali ya Kampuni ya Machimula's Express lenye namba za usajili T.550DGK.

Kampuni hiyo ya mabasi inamilikiwa na mfanyabiashara Salum Kanyinyi wa Kondoa, ambalo hufanya safari zake kati ya Arusha na Kondoa.

Vilevile alisema pia katika operesheni hiyo, karibu na Kituo cha Polisi Babati waliwakamata watuhumiwa wengine wawili, wakiwa na bunda 320 za bangi zenye uzito wa kilogramu 147.5.

Alisema watuhumiwa hao walificha dawa hizo ndani ya bodi ya gari namba T.225 APF, Nissan Pickup, linalomilikiwa na Elibariki Kilep wa Arusha.



Mwenyekiti wa Nyanza Group ya Mji Mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, Malimi Kija (kulia), akimkabidhi mwanachama wa kikundi hicho, Emmanuel Kipunile, kalenda na fulana juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# TMDA yapewa jukumu la ukaguzi majengo, miundombinu

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MKOA wa Kilimanjaro umeipa kazi Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba nchini (TMDA), kujielekeza zaidi kuyafanyia ukaguzi majengo na miundombinu inayotumika kutoa huduma ya dawa na vifaa tiba, kwa kuwa baadhi yake yanahatarisha usalama wa watumiaji.

Katika ukaguzi huo serikali imesisitiza wakaguzi wa dawa na vifaa tiba kukabidhi ripoti yake kwa TMDA, juu ya madhara yoyote yanayohisiwa.

Katibu Tawala wa Mkoa huo, Willy Machumu, alielekeza kuanza rasmi kwa ukaguzi huo jana, wakati wa ufunguzi wa mafunzo kwa wakaguzi wa dawa na vifaa tiba wa halmashauri saba mkoa huo.

"Hakikisheni mnalinda afya za jamii, kwa kusimamia uingizaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi, ambavyo vinakidhi vigezo vya ubora, usalama na ufanisi.


"Aidha, fanyeni ukaguzi wa mara kwa mara wa majengo yanayotoa huduma na kufanyabiashara ya dawa na vifaa tiba kuhusu madhara yoyote yanayohisiwa kusababishwa na uchakavu wa majengo ya kutoa huduma."

Kabla ya Machumu kutoa maelekezo hayo, Kaimu Meneja wa TMDA, Kanda ya Kaskazini, Dk. Furaha Nyunza, alisema wakaguzi hao wanapewa kwanza mafunzo ya maadili ya ukaguzi na namna ya kutambua bidhaa duni.

Pia watafundwa namna ya kutambua bidhaa bandia, mbinu za ukaguzi, maadili, utunzaji sahihi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi kama sehemu ya ugatuaji wa madaraka kwa ngazi za halmashauri.

"Mafunzo haya yanakwenda kuwaongezea uelewa wakaguzi wetu na tunakwenda kupunguza malalamiko ya wateja, ambao ni watumiaji wa dawa," alisema.

Alisema washiriki wa mafunzo hayo ni wafamasia, wataalamu wa maabara na maofisa mifugo.





## Hospitali ya Kibong'oto kutengeneza chanjo za magonjwa

**Na Anjela Mhando,** SIHA

CHANJO za kinga ya magonjwa ya binadamu zitaanza kuzalishwa hapa nchini wakati wowote kuanzia sasa baada ya Hospitali ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi ya Kibong'oto kukamilisha mchakato mzima wa utekelezaji wa mradi huo.

Jana Mkurugenzi wa Hospitali hiyo, Dk. Leonard Subi, alisema mradi huo utalisaidia taifa kuokoa fedha nyingi za kigeni zinazotumika kuagiza chanjo nje ya nchi.

Kwa mujibu wa Dk. Subi mradi huo unaanza kutekelezwa baada ya maabara kubwa na ya kisasa kujengwa na serikali kwa Sh. bilioni 12.5

"Kuzalishwa kwa chanjo hizo hapa nchini itakuwa ni mafanikio makubwa hasa ikitiliwa maanani kwamba asilimia 100 ya chanjo zinazohitajika kwa ajili ya matumizi zinatoka nje ya nchi," alisema.

Maabara hiyo ina uwezo wa kuchunguza vimelea hatarishi vya maradhi duniani kama ebora, chikungungunya, corona, kifua kikuu na kifua kikuu sugu.

"Kama tunao huo uwezo, maana yake hakutakuwa na haja ya kupeleka sampuli nje ya nchi, badala yake tutazichakata Kibong'oto. Kwa hiyo fedha zilizokuwa zinaenda nje ya nchi zitabaki hapa Tanzania, kwa ajili ya matumizi mengine ya maendeleo," alisema.

Aidha, alisema pia hospitali hiyo ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi imeanzisha huduma kwa kutumia gari maalum, lenye vifaa vya kisasa vya teknolojia ya juu kuwafikia wagonjwa wengi.

Hospitali ya Kibong'oto, ilianzishwa kama kliniki kwa ajili ya kuwahudumia majeruhi ambao walikuwa ni waathirika wa vita kuu ya pili ya dunia.



Mtafiti Mkuu Mwandamizi wa Kituo cha Utafiti wa Mifugo (TALIRI), Walter Mangesho, akifafanua kuhusu malisho ya mifugo katika shamba jana wakati Kamati ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo ya Uwakilishi Zanzibar ilipotembelea kituoni hapo, kujifunza maendeleo ya ufugaji. Wa tatu kulia ni Waziri wa Wizara hiyo Zanzibar, Shamata Khamis na (wa nne kulia) ni Mwenyekiti wa Kamati, Yussuf Iddi. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# Waandishi wa habari kuisaidia serikali kutangaza vivutio

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

CHAMA cha Waandishi wa Habari mkoani Arusha (APC), kimeahidi kuisaidia serikali kuvitangaza vivutio vya utalii vinavyopatikana katika Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara, kwa kuwa havipatikani katika hifadhi nyingine yoyote nchini.

Moja ya vivutio ambavyo havijulikani vizuri hata na Watanzania wenyewe ni pamoja na chemichemi ya maji moto ili kuvuta watalii wengi zaidi na kuchangia kukuza uchumi wa Taifa.

Akizungumza jana jijini Arusha, Mhifadhi Mkuu katika Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara, Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi, Neema Mollel, akizungumza na waandishi wa habari waliotembelea hifadhi hiyo na baadaye kufanya mkutano mkuu maalum katika ukumbi wa hifadhi hiyo, alisema bado vivutio vya utalii katika hifadhi hiyo havijulikani na watu wengi.

"Ujio wenu wa kutembelea hifadhi yetu na kufanya mkutano mkuu wenu tunawashukuru mno, tunaamini vivutio vyetu ambavyo havijatangazwa mtatumia vyombo vyenu vya habari kutangaza vivutio vingi vizuri vilivyoko katika Hifadhi ya Ziwa Manyara ambalo kwa sasa maji yamejaa," alisema.

Vivutio vingine vilivyoko katika Hifadhi ya Taifa ya Manyara ni simba wenye uwezo wa kupanda juu ya miti, utalii wa kutumia mitumbwi na utalii mpya wa kupita juu ya madaraja ya kamba na kuona chini wanyama wa aina mbalimbali kwa ukaribu zaidi.

Aidha, alisema vivutio hivyo ni fahari ya Tanzania na vipo kwa ajili ya kila mmoja, hivyo ni vema kila mtu akatumia muda wa likizo na sikukuu kutembelea hifadhini wakiwa na familiya zao kujionea vivutio ambavyo Mungu ameijalia nchi.

Alisema vivutio vingi ambavyo Watanzania wanapaswa kuviona, badala ya kuachia wageni pekee, wazawa wanapaswa kulipia Sh.11, 800 kwa mtu mzima na mtoto Sh.2,200 na magari madogo Sh. 23,000.

Katika kikao hicho, Mwenyekiti wa APC, Claud Gwandu, alisema waandishi wa habari ni miongoni mwa wadau wakubwa wanaopaswa kutembelea hifadhi za taifa na kuzitangaza ili Watanzania wafahamu umuhimu wa kutembelea vivutio vilivyoko kwenye hifadhi hizo.

Alisema waandishi wa habari ni chachu ya kutangaza vivutio vya utalii nchini na kutokana na hilo APC waliamua kufanya mkutano huo ili kutoa fursa ya kutembelea Hifadhi ya Ziwa Manyara kwa ajili ya kuendelea kutangaza vivutio vilivyoko.

Alisema: "Sisi tunakuhakikishia baada ya kumaliza mkutano wetu tumejipanga kutangaza hifadhi hii kupitia vyombo mbalimbali vya habari, hapa tuko waandishi zaidi ya 40 kwa hiyo tegemea kuona habari nyingi katika vyombo nyetu vya habari."

# Wamwomba RC kuingilia mgogoro wa ardhi unaofukuta

**Na Oscar Assenga,** TANGA

WAKAZI wa Mtaa wa Mwanzange ulioko Kata ya Majengo jijini Tanga, wamemwomba Mkuu wa Mkoa huo, Omary Mgumba, kuingilia kati mgogoro wa ardhi unaofukuta hivi sasa kati yao na Taasisi ya Muslim Associations.

Wananchi hao wanaituhumu taasisi hiyo kuvamia eneo lao la makazi na kusababisha mgogoro unaotishia uvunjifu wa amani.

Mjumbe wa Serikali ya Mtaa huo, Regina Hatibu, aliwasilisha kilio cha wananchi hao jana kwa Mkuu wa Mkoa alipotembelea eneo hilo.

Regina alisema kuwa wazazi wao walikuwapo katika eneo hilo tangu mwaka 1930, lakini ilipofika mwaka 1989, mgogoro huo ulianza baina yao na taasisi hiyo, inayodai eneo lote la hekari saba ni la kwao.

"Mkuu wa Mkoa tusaidie eneo hili ni kubwa lakini siyo eneo lote ni la kwao eneo hili ambalo lina nyumba 21 ni la wakazi wa mtaa huu wa Mwanzange tangu kipindi hicho cha wazee wetu," alisema Regina.

Regina alisema kuwa ombi lao kwa Mkuu wa Mkoa ni kuachiwa kuendelea kuishi katika makazi hayo kwa kile wanachokiamini wana uhalali wa umiliki wa eneo hilo ingawa taasisi hiyo imelifikisha jambo hilo mahakamani na kuamuliwa wananchi hao waondoke kwa kupewa notisi.

Aidha, alisema baada ya mahakama kutoa maamuzi hayo ya ushindi kwa taasisi hiyo walikata rufani katika Mahakama ya Ardhi ambapo bado hakujatolewa maamuzi yoyote ingawa wanaishi kwa mashaka kutokana na hofu ya kuja kuhamishwa.

Hamisi Hassan anayekadiriwa kuwa na umri wa zaidi ya miaka 80, alisema wazazi wao waliishi katika eneo hilo tangu miaka ya 1930 na hapakuwa na mtu aliyejitokeza na kudai eneo hilo ni mali yake.

Akijibu ombi hilo, Mkuu huyo wa Mkoa, alisema serikali ipo pamoja na wananchi hao ingawa jambo hilo lipo Mahakama ya Ardhi na kutokana na taratibu serikali haiwezi kuingilia chombo cha kisheria hadi pale kitakapotoa maamuzi yake.

Mgumba alisema lengo la ziara yake katika eneo hilo la hekari saba ambapo kuna sehemu ya makaburi, uwanja na makazi ya watu ni kuona namna gani wanaweza kukaa na pande hizo mbili, Taasisi ya Ibadhi na wananchi hao kuona njia mbadala ya kumaliza mgogoro huo.

"Nimekuja kwa maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan, kushughulikia jambo hili na sote tunajua kuwa mgogoro huu upo mahakamani na hatuwezi kuingilia. Tusubiri uamuzi wa kisheria ndipo tutakapoona namna ya kufanya,"alisema Mgumba.

Hivyo aliwatoa wasiwasi wananchi hao kwa kuwaeleza kuwa ipo njia ya mazungumzo inaweza kufanywa na serikali pamoja na tasisi hiyo nje ya makahama na kumaliza mgogoro huo kwa kutumia busara.

Ukurasa 14



UWT katika ajenda mwaka mpya 2023, miradi maendeleo kona zote



# BUFE

IJUMAA DESEMBA 30, 2022

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Nipashe

**ISABELA DOS SANTOS**
**Mama tajiri Afrika matatani, mahakama ikiamuru kushikwa mali zake Dola bn.1.4/-**

Ukurasa 15

# NGO 'yawatoa' kinamama kuwaingiza katika kilimo cha kisasa kwa ushindi

**Na Thobias Mwanakatwe, Ikungi**

KILIMO ni kiungo muhimu katika kuchagiza maendeleo na kuhakikisha uhakika wa chakula. Wakati kilimo kinabaki kuwa uti wa mgongo wa jamii nyingi barani Afrika, katika baadhi ya nchi kumejengwa mazoea kwamba kazi hiyo inafanywa na kada fulani pekee katika jamii.

Hapo ndipo Shirika la Farm Africa kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa linalohusika na masuala ya wanawake UN-Women, zimeamua kuwekeza kwa kada ya wanawake katika kilimo zao la alizeti.

Meneja Mwandamizi wa Farm Africa, Tumaini Elibariki, anaiambia Nipashe, kwamba shirika hilo limejikita kuwawezesha kiuchumi kupitia kilimo cha alizeti ambacho, miongoni mwa wanufaika wake ni wanawake na wasichana kutoka katika vijiji vya Mnang'ana kata ya Sepuka, kipumbiko kata ya Dung'unyi na Irisya na Munyu kutoka katika kata ya Irisya Wilaya ya Ikungi mkoani Singida.

Anasema Farm Africa inayofadhiliwa na Shirika la Maendeleo ya Korea (KOICA), inawaunga mkono wanawake kwa asilimia 100, kwa ajili ya kuboresha huduma za kilimo cha alizeti kwa jamii.

Elibariki anasema, kampuni hiyo na washirika wake, wameshafanya mengi kwa wanawake wa kata ya Sepuka, Irisya na Dung'unyi, ambayo ni pamoja na kutoa huduma za ugani kwa wakulima wanaopewa ushauri, mafunzo na utafutaji wa masoko ya zao la alizeti.



Mwenyekiti wa AMCOS kata ya Mnang'ana wilayani Ikungi, mkoa wa Singida, Elizabeth Juma, akimuonyesha Balozi wa Sweden nchini Tanzania, Charlotta Ozaki Macias, (aliyeshika mkoba) mashine ya kupandia, inayotumiwa na wanawake wanaolima alizeti katika kata hiyo **PICHA: THOBIAS MWA-**

Shughuli nyingine ambazo wanawake wananufaika nazo anataja ni kupewa huduma za pembejeo, yaani mbegu, mbolea na dawa, hai kadhalika huduma ya zana na teknolojia ya kilimo shambani na hifadhi baada ya mavuno.

Elibariki anasema katika kuhakikisha wanawake hao walioijiunga katika kikundi wanaendesha shughuli zao kisasa, Farm Africa imewajengea ghala la kuhifadhi mazao katika Kijiji cha Mnang'ana.

Anasema ni mradi unaotekelezwa kijijini Mnang'ana katika kata ya Sepuka, ukilenga kusaidia wananchi kiuchumi, ambako hadi sasa umewafikia zaidi ya wanawake 500 wa vijiji vinne vya mradi.

Elibariki anaweka wazi manufaa wanayopata wanawake hao, baada ya Balozi wa Sweden nchini Tanzania, Charlotta Ozaki Macias, kutembelea mradi huo kujifunza, akikiri wanufaika wa mradi huo wameweza kupewa mafunzo mbalimbali ya kilimo cha alizeti, kuongeza thamani ya mazao na jinsi ya kutafuta masoko ya ndani na nje ya nchi.

"Kupitia mradi huu wanawake na watu wengine wa vijiji vya kata ya Sepuka kumewawezesha kuboresha Chama cha Ushirika cha Mnang'ana na vyama vingine vya Mng'unyu na Amcos ya Mng'unyu" anasema Elibariki.

Pia, anafafanua kuwa, wanawake hao wamefundishwa uzalishaji mbegu bora, hivyo ni wakati sasa wa kuongeza kasi ya kilimo, kwa kupanua maeneo ya kilimo ili kuwawezesha kuvuna mazao mengi na kupata kipato na soko kubwa.

Elibariki anaeleza kwamba, kupitia shirika hilo wameweza kuboresha Chama cha Ushirika cha Mnang'ana na vyama vilivyopo vijiji jirani, ikiwamo Amunyu ambako wamejifunza matumizi ya mbegu bora na namna ya upandaji, hali kadhalika matumizi sahihi ya pembejeo.

**MAOFISA SERIKALI**

Kwa upande wake, Mkuu wa Idara ya Kilimo Wilaya ya Ikungi, Gurisha Msemo, anasema mradi huu ambao unajulikana kama 'Tufikie usawa kijinsia wa kumuwezesha mwanamke, unatekelezwa katika vijiji vya Kipumbiko, Irisia, Munyu na Mnang'ana.

Anataja miradi inayotekelezwa ni pamoja na kilimo cha alizeti na mbogamboga, mpango bora wa matumizi ya ardhi na umilikishwaji na mradi wa kupunguza ukatili wa kijinsia.

Msemo anasema, katika kuhakikisha miradi hiyo inakuwa na mafanikio kumejengwa soko la kisasa la mboga Ikungi mjini, kituo cha kutoa taarifa kwa wahanga wa ukatili wa kijinsia na anataja idadi ya wananchi walionufaika ni kati ya 6,000 hadi 14,000.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Justice Kijazi, anasema kimsingi miradi hiyo inayoendeshwa na shirika la Farm Africa imeleta manufaa makubwa kwa wananchi, hususani wanawake kwa kuwainua kiuchumi.

Anasema wanufaika wa miradi hiyo jambo la msingi ni kuitunza na kuienzi miradi hiyo ili iweze kuwanufaisha zaidi kwani hata halmashauri inapata mapato yake kupitia sekta ya kilimo.

UCHUMI

# UWT katika ajenda mwaka mpya 2023, miradi maendeleo kona zote

## • Handeni waanza safari kufuga nyuki



Mwenyekiti wa UWT Taifa, Mary Chatanda, akipeana mkono na Mhifadhi wa Shamba la Nyuki la Mwambao Handeni, Juma Mchafu, alipomkabidhi mwenyekiti huyo baadhi ya mizinga kwa ajili ya mradi wa UWT Wilaya ya Handeni.

**Na Sabato Kasika, aliyekuwa Korogwe**

UMOJA wa Wanawake Tanzania (UWT), ni mojawapo ya jumuiya za CCM ambazo zinamiliki miradi midogo midogo ya kiuchumi, ambayo imekuwa ikisaidia jumuiya hiyo kuendesha shughuli zake.

Miongoni mwa miradi inayoendeshwa na umoja huo, inatajwa kuwa ni ya vibanda, mashine za kusaga na mingine midogo ambayo haijaipa UWT nguvu kiuchumi kuweza kujitutumua.

Mwenyekiti wa CCM Taifa, Rais Samia Suluhu Hassan akifungua Mkutano wa 10 wa UWT jijini Dodoma, ameitaka kwenda kufanya miradi mikubwa itakayoipa nguvu ya kiuchumi.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, kutokana na udogo wa miradi hiyo, haiwezi kuipa nguvu kubwa ya kiuchumi badala yake imekuwa ina guswa na kuachwa, kwa kuwa haina uwezo wa kuendesha umoja huo.

Kutokana na maelezo hayo, Mwenyekiti wa UWT Taifa, Mary Chatanda, anayabeba hayo akisema ajenda kuu ya umoja huo mwaka 2023, ni kujiimarisha kiuchumi kwa kubuni miradi zaidi na kuongeza wanachama.

Akizungumza na wanachama wa umoja huo na wa CCM mkoani Tanga katika mapokezi yake yaliyofanyika mjini Korogwe wiki iliyopita, alipotua kwao kwa mara kwanza tangu ashike nafasi hiyo, Mwenyekiti Mary anaahidi kusema, atazunguka kila mkoa na viongozi wenzake kuhamasisha wanachama wa umoja huo, wabuni miradi ya kiuchumi itakayosaidia umoja ujitegemee, lakini pia kuongeza idadi ya wanachama.

"Kwa miaka mitano ambayo tutakuwa madarakani, tunataka kuhakikisha umoja wetu unakuwa imara kiuchumi na kuwa na idadi kubwa ya wanachama watakaosaidia kukitetea chama na serikali yake," anasema Mary.

Pia, anasema katika kipindi cha miaka hiyo, wataenda na dira iliyotolewa na Mwenyekiti wa CCM Taifa, kwa lengo la kutaka umoja ulio imara na ukisaidie chama katika harakati zake.

"Jambo la msingi ni kusimamia miradi iliyopo ili iwe na tija, na kuongeza mingine mikubwa, hivyo tutashirikiana na wataalam wa mambo ya uchumi watusaidie jinsi ya kubuni miradi hiyo, ili lengo letu litimie," anasema.

Anafafanua kuwa watafikia malengo waliyojiwekea ya kujiimarisha kiuchumi na kuongeza idadi ya wanachama iwapo watavunja makundi yaliyokuwapo wakati wa mchakato wa uchaguzi na kuwa wamoja.

"Tuliochaguliwa ndio viongozi wa UWT, tutaongoza miaka mitano, kwa mantiki hiyo, wale wote waliokuwa wakitushabikia au wenye mapenzi ya dhati nasi tunawashukuru, tuimbe na tusimame na UWT na chama," anasema.

Mwenyekiti huyo anasema ushirikiano ndio njia pekee itakayowafanya wafanikishe ajenda mbili ambazo wamepanda kuanza nazo mwaka 2023, za kujiimarisha kiuchumi kwa kubuni miradi zaidi na kuongeza wanachama.

**MIZINGA NYUKI**

Katika mapokezi nyumbani kwao Korogwe, Mwenyekiti huyo wa UWT Taifa, pia alikabidhi mizinga ya nyuki kwa wanachama wa Umoja wa Wilaya ya Handeni, ikiwa ni mkakati wa kubuni miradi zaidi ya uchumi.

Shamba la Nyuki la Mwambao, Handeni, limetoa mizinga 50 kwa umoja huo, ambao baadhi yake ilikabidhiwa na Mwenyekiti huyo na mhifadhi wa shamba hilo, Juma Mchafu, kwa ajili ya UWT wilaya ya Handeni.

Mary anaushukuru uongozi wa shamba hilo kwa kutoa mizinga hiyo na anasema itakuwa ni sehemu ya mkakati wa UWT kujiimarisha kiuchumi katika wilaya hiyo, na kwamba watahakikisha umoja.

Mwenyekiti wa UWT Wilaya ya Handeni, Sophia Masimba, anasema kwa muda mrefu wamekuwa na mradi wa maturubai na viti ambavyo huwa wanakodisha katika sherehe na misiba.

"Kwa muda mrefu tuna mradi wa maturubai mawili na viti 100 ambavyo huwa tunakodisha, turubai dogo shilingi 30,000 na kubwa shilingi 60,000. Kwa upande wa viti, kila moja tunakodisha kwa shilingi 300,"anasema Sophia.

Pia, anaeleza kuwapo mradi huo mwingine wa ufugaji kuku wa kienyeji inayofanyika kwenye baadhi ya kata kama Konje, Mabanda na Chanika, lakini haijaimarika.

"Handeni ina kata 33, miradi inafanyika kata hizo tatu, nyingine wana UWT wanaendelea na ujenzi wa mabanda ya kufugia kuku. Tunawashukuru Shamba la Nyuki Mwambao kwa msaada wa mizinga ya nyuki," anasema.

Anasema wanachosubiri sasa ni kupata elimu ya ufugaji, ili wajue ni vifaa gani vinatumika, na kwamba wanataka wawe na kiwanda kidogo cha kusindika asali na kufafanua ana uhakika soko la asali ni kubwa ndani na nje ya nchi.

Mhifadhi wa Shamba la Nyuki Mwambao, Mchafu, anasema baada ya kumalizika Sikukuu za Krismasi na mwaka mpya watatoa mafunzo kwa baadhi ya wanachama hao wa UWT ya jinsi ya kuhudumia mizinga.

"Baada ya hapo tutakuwa tunafuatilia kuona kama wanaendelea vizuri au kama kuna changamoto, zilizo ndani ya uwezo wetu, basi tuwasaidie kuzitatua ili kuhakikisha mradi huo wa kufuga nyuki uwe na tija," anasema Mchafu.


Baadhi ya wanachama wa UWT na CCM wakiwa katika mkutano wa mwenyekiti huyo mjini Korogwe alipotangaza ajenda za kubuni miradi zaidi ya kiuchumi na kuongeza idadi ya wanachama wa umoja huo. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**

BIASHARA

ISABELA DOS SANTOS

# Mama tajiri Afrika matatani, mahakama ikiamuru kushikwa mali zake Dola bn.1.4/-

• Waathirika na dokezo la kilichomo nyuma ya pazia



MNAMO mwaka 2019, Isabela dos Santos, binti wa rais wa zamani wa Angola, alitajwa kuwa mwanamke tajiri zaidi barani Afrika. Mnamo mwaka 2013, chombo cha habari Forbes kilitangaza kwamba jumla ya utajiri wake ulikuwa umezidi Dola za Marekani bilioni mbili, hivyo alikuwa bilionea wa kwanza wa kike wa Afrika.

Baba yake Isabela, Rais Jose Eduardo dos Santos, alifariki Julai mwaka huu, baada ya kuongoza kwa takriban miongo minne hadi 2017. Miaka mwili tu baada ya kuondoka madarakani baba huyo, binti akajikuta anaanza kukabiliwa na tuhuma nzito za ufisadi, mali zake zikiwa njia panda.

Mnamo mwaka wa 2019, Mahakama ya Juu ya Angola iliamuru kukamatwa kwa mali zake kwa madai ya kusimamia fedha za serikali kwa kampuni ambayo alikuwa na hisa wakati wa urais wa baba yake, ikiwa ni pamoja na kampuni kubwa ya mafuta ya Sonangol.

Hatua ya mahakama kuamuru kuwekewa kizuizi mali zenye thamani ya karibu Dola za Marekani bilioni mbili, ikieleza kwamba kuna ushahidi wa madai ya ubadhirifu na utakatishaji fedha haramu, sasa ikaamuru kukamatwa fedha za Isabela katika taasisi zote za benki.

Ukamataji huo pia unajumuisha hisa zote alizo nazo katika kampuni ya Angola ya Embalvidro, pamoja na asilimia 100 ya hisa katika kampuni ya mawasiliano ya simu ya Unitel T+ ya Cape Verde na Unitel STP huko Sao Tome e Principe.

Pia, kunatajwa kuwapo asilimia 70 ya hisa zake katika kampuni zilizoko nchini Msumbiji, nazo mahakama inahimiza zinapaswa kukamatwa. Msemaji wa Isabela hakujibu mara moja hoja hizo, huku mhusika akikanusha uamuzi huo wa kisheria una sura za kisiasa. Agizo hilo linakuja, huku shirika la polisi duniani, Interpol, limetoa notisi ya Isabela kutafutwa na kukamatwa kokote aliko duniani.

Tangu mwaka 2018, serikali ya Angola imekuwa ikionyesna kusudio la kumshtaki Isabel kwa jinai na ufisadi uliochangia kwenye magumu ya kiuchumi nchini Angola katika miaka iliyotangulia. Lakini Isabel hakurudi tena Angola akibaki Ureno, taifa lililomiliki koloni Angola.

Mnamo Desemba 30, 2019, Mahakama ya Mkoa wa Luanda iliagiza kufungiwa kwa akaunti za kwenye benki za Angola na kukamatwa hisa zake katika kampuni. Baadaye anatajwa kuhamia katika Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), kama nchi yake rasmi ya kuishi.

Mnamo Januari mwaka 2020, serikali ya Angola ilitangaza kwamba inachukua hatua za kisheria kunyakua mali za dos Santos nchini Ureno.

**SAFARI ALIKITOKA**

Isabel dos Santos ni mzaliwa wa mwaka 1973, mfanyabiashara na mjasiriamali wa kike kutoka nchini Angola, akiwa mtoto wa kwanza wa Rais Jose Eduardo dos Santos, aliyengoza nchi hiyo tangu mwaka 1979 walipopata uhuru.

Inaelezwa kuwa, mzizi wa utajiri wake Isabel dos Santos alizaliwa huko Baku, Azerbaijan katika iliyokuwa Jamhuri ya Umoja wa Kisovieti (USSR) akiwa binti wa kwanza wa Jose Eduardo dos Santos na mkewe wa kwanza, Tatiana Kukanova raia wa huko USSR, ambaye walikutana alipoenda kusoma huko.

Isabela, baada ya kupitia shule ya wasichana ya Kent Uingereza, alisomea uhandisi umeme katika Chuo cha King's jijini London, ambako alikutana na mumewe Sindika Dokolo, mtoto wa milionea kutoka iliyokuwa Zaire, sasa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Katika miaka 20 iliyopita, baada ya masomo akaanza kazi ya Uhandisi Mradi katika kampuni mojawapo, iliyokuwa imeshinda mkataba wa kusafisha mji, kisha akatumikia nafasi za usimamizi katika kampuni kadhaa zilizoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Ulaya.

Baada ya miaka ya 1990 aliporejea kwao jijini Luanda, alijiunga na baba yake, akaanzisha biashara ya malori. Mwaka 1997, akaanzisha klabu ya starehe ya Miami Beach na kwa kipindi cha karibu miaka 20 alipanua biashara zake, katika sura ya uwekezaji zaidi nje ya nchi hasa nchini Ureno.

Katika siku za mwishoni mwa uongozi wa baba yake, alimteua Isabela kuwa Mwenyekiti wa kampuni ya umma ya Sonangol, inayohusika na mafuta nchini Angola (nchi hiyo inazalisha mafuta), ikawa suala lilizua lawama na utata, mtoto wa rais kutunukiwa nafasi hiyo. Baada ya kuingia madarakani, Raus Joao Lourenço, aliyemrithi Mzee Eduardo dos Santos, ndani ya miezi miwili kuapishwa, alimuondoa Isabela katika nafasi hiyo.

Mnamo Desemba 30, 2019, Korti ya Mkoa wa Luanda iliamuru kukamatwa kwa akaunti ya benki ya binafsi ya dos Santos, mumewe, Sindika Dokolo, na Mário Filipe Moreira Leite da Silva. Kulingana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wafanyabiashara hao watatu waliingia katika kushughulika na serikali ya Angola kupitia kampuni Sodiam, inayouza almasi ya umma, pia kampuni ya mafuta ya serikali.

Pamoja na mikataba hiyo, serikali ya Angola inatajwa ilipata hasara ya dola bilioni 1.14 na korti ikatoa hati ya hatua hizo kisheria tajwa. Pia, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Ureno imetamka kutambua rasmi kwamba uchunguzi umefunguliwa ndani ya shughuli kadhaa za Isabel, hata mwenyewe ameamua kuhamia Dubai kama makazi rasmi ya kuishi.

Kuna mengi yanatajwa dhidi yake, kama vile kutia saini ushirikiano tata wa pamoja na kibiashara na kampuni alizowajibika nazo, Angola, Hadi karibuni anatajwa kumiliki miradi na kampuni kadhaa, ikiwamo Trans Africa, kampuni ya Gibraltar iliyoanzishwa kufanya biashara ya almasi, kampuni za mawasiliano na simu, kampuni katika ya nishati ya jijini Amstertdam Uholanzi inayowekeza katika nishati na mafuta.

Isabela anaingia katika rekodi, kwani mnamo Novemba 2015, Shirika la Habari la Uingereza (BBC) lilimuorodhesha katika wanawake 100 wenye ushawishi mkubwa duniani.

***Kwa mujibu wa habari za kimataifa.***

UCHUMI

# Mapinduzi jinsia yalivyozalisha makubwa kijijini kwenye biashara misitu, kinamama waking'ara

**Na Christina Haule, Morogoro**

KAMPENI dhidi ya matukio ya unyanyasaji kijinsia na mfumo dume, zimeanza kupungua katika vijiji vya mradi wa kuhifadhi misitu, kwa kuwezesha Biashara Endelevu ya Mazao ya Misitu Tanzania (CoForEST), baada ya wahusika kupatiwa elimu ya jinsia.

Ofisa wa Sheria kutoka Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu (MJUMITA), Elida Fundi, anasema tangu kuanza mradi huo mwaka 2015 na kufika 2017, katika baadhi ya vijiji wamefanikiwa kutoa elimu ya jinsia kwa wanavijiji 35 vya mradi huo mkoani Morogoro, ambavyo 20 ni vya wilayani Kilosa, 10 kutoka Morogoro Vijijini na vitano vya wilayani Mvomero.

Anasema, masuala ya jinsi na jinsia yanapaswa kutambulika kwenye jamii, ili kuifanya iishi katika mitazamo chanya kiakili, kisaikolojia pia katika kusaidiana, ili kuweza kukuza uchumi wao mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Mmoja wa wanawake anayepata elimu ya jinsi na jinsia Esther Saidi, mkazi wa kijiji cha Lulongwe, tarafa ya Tununguo, wilayani Morogoro, anasema elimu ya jinsia imewasaidia wakazi wa kijijini hapo katika masuala mbalimbali, ikiwamo vijana kuacha kukaa kijiweni na kuhamia kwenye shughuli za usimamizi wa misitu, pia wanaume kuacha kuwatumia wanawake kuleta maendeleo na kisha kuwatelekeza.

Anaitaja faida nyingine ya elimu jinsia kwao, ni kinamama wenyewe sasa wanajitambua na kujikita kwenye shughuli za Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Jamii (USMJ), ikiwamo kukata na kuchoma mkaa kwa njia endelevu na kuingia kwenye vikundi vya vikoba, kwa ajili ya kupata mitaji ya kuanzisha biashara na kujikwamua kiuchumi.

**KUTOKA KIJIJINI**

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Mlilingwa, Tarafa ya Tununguo wilayani Morogoro, Hamisi Mteneti, anasema kijiji hicho chenye jumla ya wakazi 3,551 kati yao wanaume ni 1,628 na wanawake 1,623 wanajishughulisha na mradi huo, kuanzia mwaka 2016.

Anasema katika hilo, wana Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi na sheria zake ndogo, hata wamefanikiwa kubadilika kutoka kuwakatalia wanawake zao kumiliki mali hadi wanawake kuwa na uwezo wa kumiliki mali kama majumba na pikipiki.

Mwanamke aliyefanikiwa kujenga nyumba kupitia mradi huo, Zainabu Athumani, anasema awali hakuona umuhimu kujishughulisha na chochote, lakini baada ya kupata elimu na mume wake kuelimika, alifanikiwa kukata, kuchoma na kuuza mkaa, hata akajenga nyumba ya vyumba vinne.

"Vijana wenzangu na wanawake wenzangu wajitahidi kusimama kwenye shughuli za maendeleo, kwa sababu, ukiwa na chako huwezi kunyanyasika," anasema Athumani.

Ali Semwali, mkazi wa kijiji cha Msolokelo kata ya Pemba wilayani Mvomero, anasema elimu ya jinsi na jinsia ambayo imetolewa kwa jamii yao, imewasaidia kukabiliana na changamoto waliyokuwa wanakumbana nayo, kwa wanawake wa kabila hilo kutoonekana na thamani mbele za wanaume.

Anasema kipindi cha nyuma katika kijiji hicho wanawake walikuwa wakiachwa nyuma kujadili mambo mbalimbali kwenye jamii na ikibainika wamejitokeza au wamesema, basi wanaume huchukua hatua, ikwamo kupigwa.

Semwali anasema, pia elimu hiyo imewaondolea ubaguzi na unyanyasaji kwa wanawake kuonekana kuwa hawana uwezo wa kufanya jambo lolote, ambayo kwa sasa wanashiriki kwenye mikutano kugombea na hata kuongoza katika nafasi mbalimbali za uongozi, tofauti na zamani.

"Wanawake walikuwa wanabanwa kwa kuzuiwa kutoa kauli mbele za wanaume, lakini baada ya elimu hiyo kutolewa wamepata fursa ya kuzungumza popote, hata kushika nyadhifa za uongozi." anasema.

Stamili Kisingeli, mkazi wa kijijini Msolokelo kata ya Pemba, Mvomero anashukuru kuwapo mradi huo, kwa sababu umemkweza kuwa mwanamke anayejiamini, akiwa na safari kuanza kimiliki ng'ombe watatu na akapata elimu hata akaongeza ng'ombe wakawa wamefikia 20.

Pia, anasomesha watoto wake watatu, mmoja yupo kidato cha nne huku mama huyo akiendelea kushiriki katika vikundi mbalimbali vya kiuchumi.

Vilevile, anakiri TFCG na MJUMITA inawainua kwa kuwaondoa wanawake kutoka kwenye lindi la umasikini na kuwafanya wenye uchumi mzuri, ikiwa ni zao la kuzingatia mafunzo ya kuchoma mkaa endelevu, huku miti inakatwa kwa utaratibu wa utunzaji wa mazingira.



Ofisa Mawasiliano wa asasi TFCG, Betty Luwuge, akizungumza na wakazi wa kijiji cha Msolokero, kata ya Pemba wilayani Mvomero, mkoani Morogoro. **PICHA: CHRISTINA HAULE.**

**KUJIFUNGUA ZAHANATI**

Wanawake wa kijiji cha Msolokelo wilayani Mvomero, wanajivuna kuhamia utamaduni wa kwenda kujifungulia zahanati, ikiwa ni zao la elimu ya jinsi na jinsia.

Mwanamke aliyepata elimu jinsia, Amina Kiguguye, anasema zamani hawakupenda kwenda kuzalishwa zahanati, wakijihisi wangedhalilika kuonekana kwa wanaume.

Mama huyo ambaye sasa ni mkunga wa kujitolea, anasema amewahi kushuhudia baadhi ya wanawake wakipelekwa kwenye zahanati hiyo mara ya kwanza, baada ya kujifungua, jambo ambalo ni hatari kwao na watoto wao kiafya.

"Kuna dada mmoja nilimshuhudia, aliumwa akaambiwa awahi zahanati, akaondoka kuelekea mtoni badala ya zahanati na wakati anataka kuvuka mto tu akajifungua.

"Watu wakamsaidia na mtoto wakawaleta zahanati kutibiwa na alipoulizwa alisema aliogopa kuchunguliwa na wanaume" anasimulia Amina.

Anasema, wanawake kukataa kupata huduma ya zahanati haikuishia kujifungua, pia ilihamia hata chanjo, dai kuu likiwa wanaweza wakaugua.

Mariam Selemani, anasema uelewa mdogo wa wakazi wa kijijini hapo, ulimsababisha kuishi na changamoto hiyo ya kuacha kwenda kujifungua kwenye zahanati na kujifungulia majumbani, hali iliyosababisha wakati mwingine kinamama kukosa watoto.

Anasimulia zamani hapakuwapo zahanati kwenye kijiji hicho na walitembea umbali mrefu kwenda kliniki vijiji jirani akavitaja majina ya Pemba, Kibati na Bwagala kupata huduma za matibabu na kujifungua, jambo lilochangia wakajifungua majumbani, hata baada ya kuwepo zahanati.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Juma Futula, anasema elimu jinsia imewasaidia wakazi kubadilisha mitazamo yao, hasa kwa wanaume kuwazuia wanawake kuongea mbele yao, hata kuacha kujitokeza kwenye masuala ya maendeleo.

Anasema zamani mwanamke hakuwa na nafasi ya kuzungumza au kujitokeza kwenye mikutano, lakini sasa wanajitokeza na kuendeleza shughuli za maendeleo, ikiwamo kuchagua na kuchaguliwa kwenye uchaguzi wa kisiasa.

Futula anasema, kwa kushirikiana na wanawake walianza shughuli za uvunaji miti kitaalamu mwaka 2014 zenye mita za ujazo 304.3 na kufanikiwa kupata shilingi milioni 33.5.

Anasema fedha hizo wamezitumia kuimarisha miradi ya maendeleo. ikiwemo ujenzi wa barabara, kuboresha zahanati, madawati kwenye sekondari ya kata na kumalizia nyumba za walimu, wakibakiwa na akiba benki shilingi milioni 15.4.



Baadhi ya wananchi wakimsikiliza Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja (hayupo pichani), alipozungumza nao kuhusu uvamizi katika msitu wa kuni, wilayani Mvomero, mkoani Morogoro katika ziara yake. **PICHA: MTANDAO.**

**SERIKALI NA UN**

Ofisa Maliasili Mkoa wa Morogoro, Joseph Chuwa, anasema katika kutekeleza miradi ya uhifadhi wa mazingira kwa kushirikiana na taasisi za serikali na zisizo za kiserikali wakiwemo MJUMITA na TFCG wanahakikisha uhifadhi mazingira kupitia uhifadhi wa misitu iliyopo unafanyika vizuri.

Anasema ni juhudi zinazosaidia juhudi za serikali kuhakikisha mazingira na misitu inahifadhiwa kwa mustakabali wa maendeleo ya watu wake.

Shirika la Umoja wa Mataifa (UN), katika taarifa yake linasema ukatili dhidi ya wanawake na wasichana unasalia kuwa kitendo cha ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu duniani kote, ukiathiri zaidi ya wanawake milioni 1.3, takwimu ambayo hata hivyo haijabadilika kwa zaidi ya muongo mmoja.

Inatamka utokomezaji ukatili dhidi ya wanawake ni jukumu la kila mtu, ikifafanua: "Onyesha mshikamano wako na harakati za utetezi wa hali za wanawake na uchechemuzi duniani kote.

"Iwe ni mwanaharakati wa msimu au ndio kwanza unaanza, kuna njia 10 ambazo kwazo unaweza kuchangia katika kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia"

Mambo 10 ya kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na wasichana yanajumuisha hoja: "Paza sauti- zungumza, fahamu tatizo pamoja na dalili, kemea unyanyasaji wa kijinsia, hoji mfumo dume, fadhili mashirika ya wanawake, paza sauti kwa hatua na huduma bora, saka takwimu zaidi, chechemua ili kuwepo na sheria thabiti, unga mkono uongozi wa wanawake na harakati nyingine za kuinua wanawake."

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres anasema ukatili dhidi ya wanawake na wasichana ni ugonjwa wa kimataifa unaoleta fedheha kubwa katika jamii zote duniani.



TAFAKURI YA MLALAHOI

# Hawa ndio Watanzania na nchi yao bwana!






NA JOSEPH KULANGWA
Simu: +255 713 410008
barua pepe:
kulangwasos@gmail.com

BILA shaka mnajikusanya kwa ajili ya Sikukuu ya Mwaka Mpya baada ya kupigika kwenye Noeli wiki jana. Kusanyeni nguvu, kwa sababu siku kuu za leo si lelemama.

Mwaka fulani hivi nilisafiri kwenda nchi ya Mashariki ya Mbali; Japani. Siku hiyo nilitua kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Narita na kupokewa na mwenyeji wangu kwa gari dogo hadi hotelini.

Tukiwa njiani baada ya kutoka eneo la Narita, nikashangaa kuona ukuta wenye kimo kirefu pembeni mwa barabara na wenye urefu wa kilometa takriban 20 hivi.

Nilishangaa, kwani sikupata awali kuona ukuta wa aina ile, nilipomwuliza mwenyeji wangu ndani ya ukuta huo kinafanyika kitu gani, akasema hakuna kitu ila umejengwa na Serikali kwa ajili ya kuzuia ngurumo za magari zinazosumbua wakazi wa maeneo ya pembeni mwa barabara.

Ilinishangaza, kwa sababu nchini mwetu sikuzoea kuona hilo, kwamba Serikali inapoteza fedha zake kujenga ukuta eti kwa sababu kuna watu wanasumbuliwa na ngurumo za magari kweli! Leo kuta kama hizo naziona Mirerani, Arusha, Ikulu ya Chamwino na makazi ya Waziri Mkuu, Dodoma.

Lakini, barabarani nashuhudia seng'enge zikijengwa kando mwa barabara ya Morogoro pale Mbezi Luis karibu na stendi ya Magufuli, Dar es Salaam, pia kando mwa reli ya kisasa kuzuia watu na wanyama kukatiza!

Serikali imefanya hivyo, ili kuokoa maisha ya watu na wanyama ambao wanadhani wanaweza kukatiza kokote. Kwa wanyama naelewa, lakini binadamu kweli mnazuiwa kukatiza reli au barabara mpaka mnajengewa madaraja ya juu, lakini bado hamtaki!

Rafiki yangu Eric Majanja kutoka Kigali, Rwanda alipokuja Dar es Salaam wiki jana, alishangaa alichokiona jijini hapa, aliniuliza kuhusu madaraja yaliyojengewa uzio kuzuia watu kukatiza, lakini akagundua kuna maeneo watu hao hao wavivu wa kupanda juu ya madaraja, wametoboa na kupenya.

Alichokishangaa zaidi ni bodaboda walivyo wengi na wasivyofuata kabisa sheria za usalama barabarani, huku wasimamizi wa sheria hizo nao wakiwaangalia kama vile hawawaoni na kuelekeza nguvu kwenye magari.

Majanja akaniambia kwao hilo halipo, ni kwamba sheria ni sheria na inatekelezwa na kuheshimiwa bila shuruti, na kwamba akiukaye anakabiliwa na adhabu kali ya faini au kifungo jela bila huruma yoyote.

Nikamwambia kwetu hilo ni nyimbo tu za Bibi Tarabushi, kwamba bodaboda ni kama wafalme fulani hivi wasioguswa na itokeapo wameguswa, huguswa kidogo na kuachwa, kwa kile kinachodaiwa ni wanyonge.

Nikamwambia, kuwa hapa kwetu hivi sasa wanaitwa 'maofisa usafirishaji' hivyo wana heshima kubwa kiasi kwamba hata wakikosea, hutozwa faini ndogo tu ambayo huitoa sawia ili wakaendelee na mambo yao.

Nikamfahamisha kuwa awali 'maofisa usafirishaji' hao walikuwa wakitozwa faini kama waendeshao magari, Sh 30,000 kwa kosa, lakini Bunge likaamua kushusha mpaka Sh 10,000 kwa kilichodaiwa kuwa ni wanyonge wasio na kitu.

Ikadhihirika, kuwa kumbe ukiwa mnyonge hata ukifanya kosa gani faini yako nayo itatolewa pia kinyonge. Nikakumbuka jinsi mwenye gari anavyopata kibano ikitokea amemgonga 'ofisa usafirishaji'. Atazingirwa na 'maofisa' wenzake na kusukwasukwa na ikiwezekana gari lake lichomwe moto.

Hiyo maana yake ni kwamba kwa unyonge huo dereva bodaboda anaweza kuua mtu lakini akaachwa au kupewa kifungo cha nje au hata faini ya Sh. 10,000 kwa sabahu tu ni mnyonge!

Nilimsimulia ndugu yangu Majanja, akanitazama hakunimaliza. Katika kumkomelea, nikamwambia nchini hapa kuna nyumba za kuabudu ambazo kwao Rais Paul Kagame alifungia 500 kutokana na kuendeshwa visivyo, pia kutoonyesha umuhimu wake kwa jamii, hapa kwetu si tu yanaheshimika bali yanaogopwa.

Kuna mengine yana mazito mengine ya karibuni hayajapoa, yanakinzana na nadharia za kufikia wokovu! Hiyo kama si uchawi na ushirikina ni kitu gani?

Majanja akaniuliza kwaini Rais Samia Suluhu Hassan, asifungie nyumba hizo za ibada, nikamjibu kuwa akifanya hivyo watasema mengi dhidi yake, ni vema akaacha tu watu wenyewe waamue kusuka au kunyoa, kwani aliyeturoga Watanzania pengine alishakufa.

Alinitazama kwa kunikatia tamaa, huku nami nikimshangaa kwa kunihurumia mimi na Taifa langu, huku nikijisemea kimoyomoyo kuwa atuachie kitanda chetu na kunguni wetu, kwani pilipili iko shamba haitamuwasha asilani. Hao ndio Wabongo bwana! Alamsiki!

BIASHARA

# Wazalishaji pikipiki waja na toleo lenye mfumo mwizi hamudu kuiba

## •Haiondoki bila 'kumtambua' mmiliki...



Meneja Mauzo wa kampuni ya kuuza pikipiki, Razack Kasanga (wa tatu kulia) akitoa maelezo jana kwa wateja walionunua pikipiki ofisini kwake, namna ya kutumia kifaa cha kuizima pikipiki hata ikiwa mbali, mahususi kwa ajili ya kupambana na wezi, kwenye toleo jipya la pikipiki hizo. **PICHA: HALFANI CHUSI.**

**Na Halfani Chusi**

KUIBIWA na kuporwa pikipiki, ni kati ya matatizo makubwa yanayo wakumba waendesha pikipiki nchini maarufu bodaboda, wengi wao wamekufa na wengine wamepata ulemavu wa kudumu, kwa kujeruhiwa na wezi huku wengine wakipoteza maisha kabisa.

Simanzi huwa inaibuka pale unapomuona kijana mtaani akiwa katika hali ya ulemavu (amepoteza kiungo) wakati akipambana na majambazi walipokuwa wanataka kumpora pikipiki yake.

Ikiwa kuendesha pikipiki ni njia waliyochagua vijana kujikimu kimaisha na kufanya familia zao zichanue kwa kupata mahitaji muhimu, pasi na shaka kwa namna yoyote, wanahitaji kuwa salama kumudu huduma za familia kupitia kazi hiyo.

Ni kawaida sana unapokaa kwenye vijiwe vya bodaboda kukutana na simulizi ya bodaboda aliyekufa kwa kudhuriwa wakati akiporwa pikipiki au amebaki salama lakini pikipiki imeibiwa.

Licha, ya kuwapo kwa madhila hayo yanayowakabili bodaboda kwa muda mrefu, lakini bado bodaboda, inabaki kuwa nyenzo muhimu kwa vijana kujiingizia kipato na kuendesha familia zao.

Hiyo inabeba sura kwamba, kelele za vijana wengi kukosa ajira zinakoma hapo na wengine wamefanikiwa kubadili maisha kwa kujiajiri humo.

Swali la kujiuliza ni lini? Wahusika wa utengenezaji na kuuza pikipiki zitakuja na mfumo wa mtu anapoibiwa pikipiki aweze kuifuatilia na kuipata au kuizima isiwake?.

Kama ilivyo kawaida, wizi unatia hasara, umasikini, hasa pale mtu anapoibiwa pikipiki yake kwa wastani, anakuwa amepoteza kiasi cha shilingi milioni mbili na ushee, hiyo ni kutokana na thamani ya pikipiki ilivyokuwa juu.

### ZIARA KWA WADAU

Katika kujifunza zaidi Nipashe iliamua kutembelea kampuni ya kuuza pikipiki yenye makao makuu yake Posta Mpya Jijini Dar es Salaam, kujifunza zaidi pamoja na kufahamu, wana mikakati gani ya kuweka ubunifu utakaowawezesha wateja wao kukipata chombo pindi kinapoibiwa?

Maana ukweli uliopo, inawezekana wapo wengi hata wanaogopa kununua pikipiki, wakihofia kuibiwa na kuweka maisha yao rehani kama ilivyozoeleka. Hapo ndipo, Meneja Mauzo wa Kanda, Razaki Kasanga, akaja na majibu yanayoleta picha ya kukoma madhila hayo.

Hapo panaorodheshwa vifo vya kukatwa mapanga, kupoteza mali hali inayofanya wengi kudondokea kwenye ulemavu wa kudumu na kubaki tegemezi kwenye familia.

Kasanga anasema, wizi wa pikipiki ulishamiri kwa kiasi kikubwa kipindi cha nyuma, kwa sababu hakukuwapo namna ya kuipata pindi inapoibiwa jambo ambalo wezi walijivunia.

Meneja huyo anafafanua: "katika kukabiliana na hali hiyo limekuja toleo jingine la TVS CC 125, ambalo lipo sokoni, lina kifaa kama rimoti ambacho unaweza kutumia kuizima pikipiki ikiwa kwenye umbali kidogo, hivyo hata mwizi akishakupora, unaweza ukaizima na asiweze kuifanya chochote"

### ILIVYO TEKNOLOJIA

Meneja huyo wa mauzo, anafafanua namna teknolojia hiyo mpya inavyoweza kumuokoa mtumiaji pikipiki dhidi ya wezi, akitamka: "Hii ni teknolojia ambayo ili injini iwake, itahitaji mchakato wa uthibitisho kutoka kifaa maalumu kinachoitwa 'Immobiliser Unit.' Pia kuna kifaa kingine kama rimoti kinachoitwa 'key fob.'

"Kazi yake ni kupeleka mawasiliano kwenye' Immobiliser Unit' ambayo hupeleka mawasiliano moja kwa moja kwenye kifaa maalumu cha umeme kilichopo kwenye pikipiki kinachojulikana kama TCI (wengi wamezoea kuita CDI) ambacho huamua pikipiki iwake au isiwake.

"Kwa hiyo, 'keyfob' hupeleka mawasiliano kwenye mfumo wa pikipiki uliohifadhiwa kwenye TCI baada ya kuthibitishwa na Immobiliser Unit" anasema.

Meneja Mauzo Kasanga anafafanua:"Kwa sasa, teknolojia hii ipo kwenye pikipiki zetu mpya zenye rangi ya dhahabu, zifanyiwa maboresho katika mfumo wa injini yenye nguvu zaidi na siti imara zenye rangi ya maruni."

Ili kuunganisha mfumo huo, Kasanga anafafanua kiufundi kuwa dereva wa pikipiki anapoikaribia pikipiki kwa umbali unaokadiriwa kuwa futi 10, muunganiko hutokea wenyewe (automatically), huku akiwa na hicho kifaa, pikipiki inakuwa kama imemkariri

Anasema, dereva anapoisogelea pikipiki, anapaswa kubonyeza kitufe kwenye 'keyfob' kupitia 'Immobiliser Unit' ili kuunganishwa na hapo anaweza kuwasha pikipiki.

Kwenye 'keyfob' utaona taa ya kijani kuashiria tayari kwa kuwasha pikipiki, na taa nyekundu kuashiria kuwa pikipiki haiwezi kuwaka kwa kuwa haija unganishwa.

Hivyo ukishaunganisha kwa 'key fob' utaweza kuwasha pikipiki yako kwa kutumia funguo ya pikipiki au kwa kutumia kiki ikiwa pikipiki yako haina betri.

### UNAKATAJE MAWASILIANO?

Meneja Mauzo huyo anaeleza kitaalamu kwamba, mtu anapotaka ama kukata mawasiliano au kuzuia pikipiki isiwake wakati imeibwa, dereva atatakiwa kubonyeza kitufe kwenye 'key fob' kusitisha muunganiko, hapo utaona taa ya rangi nyekundu kuashiria haijaunganishwa na pikipiki itakuwa salama .

Anafafanua, hata ikitokea mwizi akifika na pikipiki umbali wa futi 10, muunganiko utakata wenyewe na pikipiki itazima, mpaka dereva atakapoisogelea tena.

Kasanga anaasa katika hilo, ni taaluma iliyopaswa kutumika kwa kila kampuni inayozalisha vifaa vya usafirishaji, kuwaweka salama wateja wao.

Pia, anaeleza madhara husika, kwamba hata anayeiba akiwa ameondoka nayo kwenda mahali fulani pikipiki imezima, haiwezi kuwaka mpaka mwenye mali awe amefika, kwa hiyo ni kikwazo kwa muibaji.

Kasanga anaeleza:"Sisi tulikuwa tunatumia sana zamani unakuta mteja wetu amekuja kununua pikipiki hapa baada ya siku kadhaa unasikia analalamika kaibiwa pikipiki yake, hilo jambo sisi lilikuwa linatuumiza kama kampuni ndio maana muda wote tulikuwa tunaangalia ni namna gani tutakuja na suluhu ya hilo.

"Tukaweka nadhiri tukasema tunahitaji kufanya maboresho na kuwa kampuni namba moja kuleta pikipiki zenye ulinzi ambao itakuwa kinga ya mteja akinunua."

Anasema maboresho ya pikipiki huendana na wakati na ndiyo maana kasoro zilizozungumzwa awali, zinazidi kuboreshwa na ndivyo ilivyo biashara hiyo.

Ofisa huyo anahitimisha kwa kutaja manufaa yaliyoko inaligusa hata Jeshi la Polisi, kwa kuirahisishia kupambana na wezi wa pikipiki, kwa sababu itakuwa rahisi kwa muhanga aliyeibiwa, kumpata mwizi wake.


UCHUMI

# Mwaka 2022 unaaga, 2023 unaingia, tathmini yako inakupa majibu gani?

**Na Pankras Luoga**

IKIWA ni kesho tu saa sita yaan usiku, mwaka huu 2022 unatuaga, ni muhimu kukumbushana kufanya tathmini ya kina juu ya malengo yetu ya mwaka tuliyojiwekea kipindi tunaanza mwaka huu. Kwa kutumia mfano wa miradi ya maendeleo basi malengo yetu ni ya mradi wa miezi kumi na mbili.

Na kama tujuavyo umuhimu wa kufanya tathimini mara baada ya kufika mwishoni mwa muda wa utelekezaji wa mradi wowote basi sasa ni wakati muafaka wa kila mmoja wetu kufanya tathmini ili kujua kama ameweza kufikia malengo yake ya mwaka au la! Na kuweza kupata mafunzo ya kwanini amefanya au hakuweza kufanya vizuri katika kufikia malengo yake hayo ya mwaka.



Nyumba katika hali duni.

**MALENGO YA MWAKA**

Mfano rahisi wa malengo na namna ya kufanya tathimini ya mwaka, ni mtu anapoweka lengo la kujenga nyumba nne kwa mwaka 2022, yaani ifikapo mwezi wa 10 na 12 tarehe 31, 2022 kwa kutenga kiasi cha fedha za Kitanzania milioni 40 na huku akiwa tayari ana viwanja vinne.

Anaweza kufanya tathimini kwa kuanza kuangalia viashiria vifuatavyo; je mpaka sasa mwishoni mwa mwaka amefanikiwa kujenga nyumba ngapi ?; lengo lake la mwanzoni mwa mwaka likiwa ni kujenga nyumba nne ifikapo mwishoni mwa mwaka 2022.

Mengime ni, je mpaka sasa ameshatumia kiasi gani cha pesa na mwisho kabisa ni vitu gani vimefanya afanye vizuri au vibaya katika utekelezaji wa malengo husika katika kipindi hiki cha mwaka mzima? Hayo yatakuwa ni mafunzo katika utekelezaji wa malengo ya mwaka ujao 2023.

Majibu ya maswali hayo, hutumiwa kulinganishwa na malengo yaliyopangwa na kuona kama kweli utekelezaji umefikia malengo au la. Kwa kutumia mfano wa ujenzi wa nyumba hapo juu, muda wa miezi 12 na siku zilizopita mpaka sasa, yaani imebaki siku moja kabla ya muda wa utekezaji mradi au malengo kuisha basi tunategemea nyumba zote nne ziwe zimeshajengwa au nyumba ya tatu imekamilika na nyumba ya nne ipo kwenye hatua za mwisho za umaliziaji. Hivyo, inatoa picha kwamba malengo ya kujenga jumla ya nyumba nne kwa mwaka mzima yamefikiwa au la.

Pia matumizi ya fedha tunategemea kuwa mpaka sasa fedha zote ziwe zimetumika yaani milioni 40 au pungufu kidogo, ili kujua kuwa matumizi yamekwenda sawa na mipango iliyowekwa mwanzoni mwa mwaka.

Majibu hayo yatafanya mtu mwenye kufanya tathimini katika malengo yake aweze kutambua kama kweli malengo yake ameyafikia au siyo. Tukumbuke hii ndio hutengeneza mwanzo mzuri wa kuweka mipango ya mwaka ujao yaani mwaka 2023.

Kumbuka ikiwa uliweza kutimiza malengo yako vizuri, basi mipango ya mwaka ujao utakuwa mpya na kuanza malengo mengine, ila kama hukuweza kutekeleza, basi mambo yaliyobaki kuyakamilisha mwaka huu huwa ya kwanza kuyapanga, ili kuyatekeleza mwakani na kuanzisha machache mapya.

Cha msingi hapo ni kuwa, huwezi kuanza kuweka mipango mingine mipya ya mwaka mpya wakati bado kuna vitu havikukamilika katika mpango wa mwaka uliopita.

“Ogopa sana kuwa mtu wa kuweka mipango mipya kila siku bila kuikamilisha na kupenda kuhamia kwenye mipango mingine wakati ya awali hujakamilisha. Kwani, mwishoni huna kitu hata kimoja ulichoanza na kukamiliza,” kuna tahadhari ya kinadharia.

**FAIDA ZA TATHMINI**

Kuna faida gani za kufanya tathimni mara baada ya kufika mwisho wa mwaka wa utekelezaji wa malengo yetu?

Tathimini mara baada ya kuisha kwa mwaka wa utekelezaji wa malengo, itakusaidia kufanya yafuatayo: kujua utekelezaji na ukamilifu wake, kulingana na malengo ya mwanzo mwa mwaka; pili kujua nini kiwe malengo ya mwaka ujao kutokana na kile kilichotokea mwaka huu ikiwa ni pamoja na kuanza na kukamilisha malengo ya mwaka jana au kuweka malengo mengine mapya ya kuyatekeleza kwa mwaka mpya kwa maana mwaka 2023.

Pia, inaepusha kuwepo tabia ya kuweka malengo mapya kila siku na kila mwaka, bila ya kuhakikisha ukamilishaji wa malengo ya awali. Mfano hai ni kila mwaka mpya, mtu anaanza mpango mpya kwa maana mwaka 2022 alipanga kujenga nyumba kabla hajamaliza mwaka 2023, anapanga kuanza kulima shamba hata kabla ya kumalizia ile nyumba yake ya mwaka 2022.

Kibaya zaidi inakuwa, inapofika mwaka 2024, mtu anaanza kufuga kuku kabla ya kutimiza lengo la mwaka 2023. Na zaidi ya hayo yote tathimini ya kina mwishoni mwa mwaka husaidia katika kupata mafunzo kutokana na utekelezaji wa malengo ya mwaka uliopita.



Nyumba bora katika hatua za ujenzi. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Mafunzo hayo huwa ni juu ya nini kilitokea na kusababisha nifanye vizuri au vibaya katika kufikia malengo ya mwaka husika.

Hiyo itamsaidia katika kufanya vizuri katika kuyafikia malengo ya mwaka unaofuata kwa kuepuka yale mambo yaliyokwamisha kufikia malengo ya mwaka uliopita na kuyashikilia vizuri yale mambo mazuri yaliyofanya kufikia malengo katika mwaka uliopita.

Suala la kujifunza zaidi ni katika kufanya vizuri katika kupanga na kuyafikia malengo kutokana na yaliyotokea mwaka uliopita.

Kitaalamu ni kwamba, kila mtu afanye tathimini ya mwishoni mwa mwaka juu ya utekelezaji wa malengo yake huku akilinganisha na malengo yake aliyojiwekea mwanzoni mwa mwaka kwa maana ya mwezi wa kwanza mwaka 2022.

Hilo ni muhimu sana katika kutambua amefikia malengo yake ya mwaka au la! Na pia kupata mafunzo ya nini kilimfanya afanye vizuri katika kufikia malengo yake ili mambo hayo aweze kuyaendeleza katika mwaka ujao kwa maana mwaka 2023 ili aweze kufikia malengo yake.

Pia kujifunza mambo gani ambayo yalimkwamisha katika kufikia malengo yake kwa mwaka 2022 ambayo ni muhimu kuyaepuka katika mwaka 2023 ili kufikia malengo husika atakayojiwekea.

Mwisho kabisa, tathimini ya kina ya utekelezaji wa malengo ya mwaka na kujua kama yamefikiwa au hapana husaidia katika kuweka mipango ya mwaka unaofuata kutokana na kile kilichotokea mwaka wa uliopita.

Huwezi kuanza kuweka mipango mipya ya mwaka 2023 bila kwanza kuhakikisha ile ya mwaka uliopita yaani 2022 imekamilika kikamilifu. La sivyo unaweza ukawa mtu wa kuweka mipango mipya kila siku kila mwaka ila utekelezaji wake ni sifuri.

Kufanya tathimini ya kina ya malengo ya mwaka hutoa mafunzo katika upangaji na utekelezaji wa malengo ya mwaka unaofuata yaani 2023.

***Mwandishi ni Mhadhiri Msaidizi katika fani ya Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathimini ya miradi ya afya - Chuo Kikuu cha Sayansi na Tiba Muhimbili. Anapatikan kwa simu: +255 757645746.***

# Mtoto wa miaka 11 ambaye michoro yake inauzwa bei inayotikisa nchi

**Na Mwandishi Wetu**

HUYU ni Andres Valencia, msanii mpya zaidi katika ulimwengu wa sanaa: mvulana wa miaka 11, kivutio cha tamasha la Art Miami, mojawapo ya maonyesho muhimu ya kisasa ya sanaa nchini humo, mwishoni mwa juma la kwanza la Desemba.

Wakati Andres alipigwa picha na waandishi wa habari na watazamaji kwenye usiku wa ufunguzi na kuwasalimu wakusanyaji na watu mashuhuri, Chase Contemporary, jumba la sanaa la New York ambalo linamwakilisha, liliuza karibu kazi zake zote.

Kazi zake karibu zote ziliuzwa katika tamasha la sanaa huko Miami. Ndiyo, hata mchoro wa "wavulana" wanaokunywa na kuvuta sigara na toleo la ujazo la Venusaur, dinosaur unayopenda kutoka kwa mchezo wa video wa Nintendo.

Zote mbili, kama turubai zake nyingi za rangi, bila shaka zinamkumbusha mchoraji wa Guernica. Kwa hili alipata jina la utani 'Picasso kidogo'.

"Bei ya wastani ya picha zake za uchoraji ni karibu dola 150,000," anasema Bernie Chase, mmiliki wa Chase Contemporary.

Mafanikio ya Andres katika Art Miami hayakushangaza. Kitu kama hicho kilikuwa tayari kimetokea mnamo Juni iliyopita, wakati wa onyesho lake la kwanza kwenye makao makuu ya jumba la sanaa.



Kijana Andres Valencia (11), akiwa amezungukwa na kazi za sanaa yake. **PICHA: MTANDAO.**

Yeyote aliyerudi nyumbani na kazi zozote kati ya 35 zilizoonyeshwa alilipa kati ya dola 50,000 na dola 125,000.

Kazi nyingine bei ya juu hivi majuzi kwenye mnada ilikuwa ;Bi. Cube', picha ya mtindo wa Cubist aliyochora alipokuwa na umri wa miaka 9 tu.

Mbali na yeye, kazi ya Maya, kwa heshima ya binti ya Picasso, pia iliuzwa kwa bei ya juu wakati wa hafla ya hisani iliyofanyika Capri, Italia, mnamo Julai.

Vipengele vyake vikali na picha za uchoraji kutoka kwa mitazamo mingi zilikuza mkusanyiko wa Mwigizaji wa Kolombia Sofia Vergara, mmoja wa waigizaji wanaolipwa pesa nyingi zaidi kwenye televisheni nchini Marekani, mjasiriamali mwenye nguvu wa muziki Tommy Mottola au nyota wa Hollywood Channing Tatum.

Mnamo Novemba, mwimbaji wa BTS anayejulikana kama 'V' alisambaza kazi nyingine ya Andres na wafuasi wake milioni 50 kwenye Instagram.

"Asante @andresvalenciaart kwa kazi hii nzuri ya sanaa! Tangu nilipoona kazi yako kwa mara ya kwanza, nimekuwa shabiki," aliandika karibu na picha ya mtu anayelia katika michoro ya bluu. Chapisho hilo lilikuwa na 'likes' zaidi ya milioni 10.

Haya yote humfanya kijana huyo mara nyingi aishie kwenye vichwa vya habari.

Elsa na Guadalupe Valencia, wanasema wanajaribu kuwapa maisha kwa kadri inavyowezekana watoto wao Andrés na Atiana

"Hatujazaliwa tajiri na kabla niwe mtaalamu, nilikuwa mfanyakazi wa kijamii kwa miaka mingi, nikifanya kazi katika nyumba za watoto na magereza, na nilijionea jinsi unyonge ulivyo. Tuna bahati sana," anasema.

Kwa hiyo, wanasisitiza kwa watoto wao umuhimu wa kuchangia katika jamii. Kitu ambacho, wanasema, Andres tayari amefanya.

Mengi ya kile alichopata kutokana na sanaa yake kilitolewa kwa mashirika kama vile amfAR na Unicef. Na hivi majuzi, alitoa asilimia 100 ya mauzo ya nakala ya Uvamizi wa Ukraine kusaidia watoto katika nchi hiyo iliyokumbwa na vita kupitia Wakfu wa Klitschko.

***Kwa mujibu wa BBC.***


---

Dondoo: Kulia
1. nchi ambayo ni mkulima mkubwa wa mahindi duniani
6. pengine
7. hali ya mtu kuwa mchafu baada ya kufanya ngono
10.kujiunga na kikundi fulani
11.mwanasiasa mashuhuri Kenya
12.Jiji kubwa kusini mwa Uturuki
14.dhamira
16.mojawapo ya madude makubwa angani yanayozunguka jua

Chini:
1. watu wa karibu
2. tunu
3. chokaa ya kupaka nyumba
4. sema kwa heri
5. japokuwa
8. ahali
9. halafu, mwishowe
13.kitaya
15.kanya

## CHEMSHABONGO NA -00 39 00-


Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com



Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

MUNGU
MBUNI
NYUMA
UZIMA
AMBONI
ZUMA
UJUZI
ZAKARIA
MAMBO
ISAKA
SANAAN
NJAA, AMUA,
WASIKIVU, NIA

maoni SMS: 0787 00 97 94




Majibu toleo lililopita

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| B | O | M | A | | B | A | A |
| A | D | A | M | U | | N | |
| T | A | K | A | | O | G | A |
| A | | A | N | A | S | A | |
| | M | Z | I | M | A | | |
| U | Z | I | | I | M | B | A |
| | I | | | N | A | A | M |
| I | M | A | N | I | | S | I |
| | U | | | | | I | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| P | A | N | G | A | | T | |
| A | G | A | | J | A | A | |
| P | O | M | B | E | | P | |
| A | | B | O | N | D | E | |
| | M | A | N | D | E | L | A |
| | B | | D | A | R | I | |
| K | E | T | E | | E | | S |
| | G | | | | V | A | A |
| T | E | M | B | E | A | | A |

# Viongozi wapenda rushwa maeneo ya uchimbaji waonywa

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

VIONGOZI wa vijiji wanaogawa maeneo ya uchimbaji madini katika Wilaya ya Chunya Mkoani Mbeya kwa kupokea rushwa kwa baadhi ya wachimbaji, wametahadharishwa wakitakiwa kuacha tabia hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Simon Mayeka, alitoa tahadhari hiyo juzi alipofanya ziara ya kukagua shughuli za uchimbaji katika maeneo mbalimbali wilayani humo.

Mayeka alisema tatizo hilo ni miongoni mwa mambo yanayoifanya sekta ya madini katika wilaya hiyo kushindwa kukua na hata wananchi kutonufaika na madini hayo ambayo ni miongoni mwa rasilimali kubwa katika wilaya hiyo.

Aliwataka wachimbaji wa madini kuhakikisha wanauza madini hayo kwenye masoko yaliyoainishwa na serikali ili kuepuka kukumbana na mkono wa sheria.

Alisema mtu yeyote anayekamatwa akitorosha madini hatua ya kwanza serikali inataifisha madini hayo na kumchukulia hatua zingine za kisheria ikiwamo kupelekwa mahakamani.

Alisema kwa sasa kutokana na kukua kwa teknolojia, bei ya dhahabu inakuwa inajulikana katika soko la dunia, hivyo wachimbaji wanatakiwa kabla hawajauza dhahabu zao wafuatilie kwanza bei ya soko la dunia.

Baadhi ya wachimbaji wa dhahabu waliiomba serikali kuwasogezea baadhi ya huduma kwenye maeneo yao ili kuwapunguzia gharama za uendeshaji wa shughuli zao.



Spika wa Bunge ambaye ni Mbunge wa Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson, akishiriki kuchimba msingi wa vyumba vya madarasa katika Shule ya Sekondari Iganzo jijini Mbeya jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# RC abaini ufisadi ujenzi wa miradi ya afya wilayani

**Na Nebart Msokwa,**
RUNGWE

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, ameshtukia ufisadi kwenye ujenzi wa baadhi ya miradi ya afya wilayani Rungwe unaodaiwa kufanywa na maofisa manunuzi wa halmashauri.

Maofisa hao hununua vifaa vya ujenzi vyenye ubora mdogo kuliko ulioainishwa na serikali.

Homera alishtukia upigaji huo juzi wilayani Rungwe alipofanya ziara ya kukagua ujenzi wa baadhi ya vituo vya afya wilayani humo, ambako alibaini vifaa vinavyotumika ni tofauti na vilivyoainishwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Akiwa katika Kituo cha Afya cha Kata ya Ndato, Homera alibaini kuwa marumaru zilizotumika zina upana wa 40 kwa 40 badala ya 60 kwa 60 ambavyo ndivyo vilivyoainishwa kwenye mwongozo uliyotolewa na TAMISEMI.

Alisema amebaini kuwa udanganyifu huo unafanyika katika miradi mingi inayotekelezwa ndani ya mkoa huo jambo ambalo linafanywa kwa ushirikiano kati ya maofisa manunuzi na wahandisi kwa lengo la kujinufaisha.

Alisema kutokana na hali hiyo amelazimika kuunda timu maalumu ya wataalamu ambao watapitia miradi yote kwa lengo la kubaini hali ya udanganyifu huo ili hatua zichukuliwe kwa mujibu wa sheria.

"Kinachoonekana hapa ni kwamba ninyi mnabana matumizi ili fedha zinazobaki mzipige, sasa kamati kitakachotokea ni kwamba mtafidia kwa gharama zenu wenyewe, mnachokifanya hapa ni kwamba mnamdanganya Rais Samia maana hii miongozo imeletwa na ofisi yake," alisema Homera.

Alisema maofisa hao wamekuwa wakifanya hujuma hizo kwa kushirikiana na wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu kwa kukubaliana kutaja bei ya vifaa tofauti na iliyoko ili fedha zinazozidi wazichukuwe.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Rungwe, Mpokigwa Mwankuga, alimwomba Mkuu wa Mkoa kuwasaidia kukabiliana na tatizo hilo alkieleza kuwa wamekuwa wakiwahoji maofisa manunuzi kuhusu ununuzi wa vifaa hivyo lakini majibu wanayopewa huwa hayaridhishi.

Alisema maofisa hao wamekuwa wakinunua vifaa hivyo kwa bei kubwa tofauti na ambayo wao wanaijua lakini wakiwahoji wanajibu kuwa wafanyabiashara wanauza vifaa hivyo kwa bei za aina mbili tofauti kulingana na mtu wanayemuuzia.

Alisema wamekuwa wakielezwa kuwa bei ambayo wafanyabiashara hao wanaiuzia halmashauri ni tofauti na wanayomuuzia mtu binafsi jambo ambalo alisema limekuwa likiwatia wasiwasi.

Ofisa Manunuzi wa Halmashauri hiyo, Vumilia Mwaijande, alisema wao huwa wananunua vifaa kulingana na maelekezo ya wahandisi na kwamba vifaa vyote walivyonunua waliekelezwa vinunuliwe vya aina hiyo.

Alisema wahandisi huwa wanatoa sababu ya kutaka vifaa vinavyonunuliwa viwe tofauti na vilivyoainishwa kwenye miongozo na hivyo wao huwa wanazingatia utaalamu huo.

Pamoja na matatizo hayo ambayo yalibainika lakini Mkuu wa Mkoa alisema Wilaya ya Rungwe wamejitahidi kutekeleza miradi kwa wakati tofauti na maeneo mengine.

# Hospitali ya Rufani yaanza mikakati kupunguza vifo vya watoto

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HOSPITALI ya Kanda ya Rufani ya Mbeya, imeanza mikakati maalumu ya kupunguza vifo vya watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano kwa kuanza kutoa mafunzo kwa wauguzi wa baadhi ya mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Hospitali hiyo imeanza kutoa mafunzo hayo kwa wauguzi wa mikoa ya Mbeya na Songwe kwa kuwapatia mbinu za kuwahudumia watoto wachanga wakiwamo wale wanaozaliwa na matatizo

Daktari Bingwa wa Watoto kutoka hospitali hiyo, Dk. Rehema Marando, alisema takwinu zinaonesha vifo vya watoto wachanga ni karibu asilimia 47 kati ya watoto wote walio chini ya miaka mitano.

Alisema mafunzo waliyoyatoa kwa wataalamu hao yanalenga kukabiliana na tatizo hilo kwa kupunguza takwimu za vifo hivyo hasa kuhakikisha kundi hilo linapata huduma sahihi.

"Takwimu ambazo zipo Tanzania zinaonyesha kati ya vizazi hai 1,000, watoto 20 wanafariki, kwa hiyo tumeona tuna kila sababu ya kujengeana uwezo ili kupunguza vifo hivi," alisema Dk. Rehema na kuongeza

"Kati ya hawa wataalamu kuna ambao wako kwenye vitengo wanafanya kazi na tunataka wapate vitu vipya na kwa ambao hawana mafunzo hayo nao waweze kujua ili kuboresha utoaji wa huduma kwa kundi hili," aliongeza.

Mkuu wa Idara ya Watoto katika hospitali hiyo, Dk. Nuru Mlimu, alisema vipo vifo vya watoto wachanga vinavyoweza kuzuilika ikiwa wahudumu wa afya watatumia vema ujuzi walionao na kuwataka wauguzi hao kuwa sehemu ya watakaosaidia kuzuia vifo hivo.

Baadhi ya wahudumu wa afya na madaktari waliopatiwa mafunzo hayo, walisema mafunzo hayo yatawasaidia kuongeza ujuzi wa namna ya kuwahudumia watoto wachanga.

Mmoja wa wataalamu hao, Hamza Yunge, alisema ili kuhakikisha wataalamu wanaookoa maisha ya watoto wanakuwa wengi, watahakikisha wanawafundisha na wenzao ambao hawakupata nafasi ya kushiriki.

Alisema kwenye mafunzo hayo walipata mbinu mpya ambazo hapo awali hawakuwa nazo na kwamba baadhi ya mbinu walikuwa nazo lakini kupitia mafunzo hayo wamekumbushwa.

Kaimu Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya, Dk. France Rutwashoba, aliwataka wahudumu hao wa afya kwenda kufanya kazi kwa kuzingatia maadili ya taaluma yao.

Alisema serikali imewaamini na ndio maana imewaajiri na kuwapatia mafunzo ya kuwaongezea uwezo hasa katika kuokoa maisha ya watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano.





## DC Kongwa akabidhiwa madarasa, shule mbili mpya

**Na Renatha Msungu,**
KONGWA

MKUU wa Wilaya ya Kongwa, Remidius Mwema pamoja na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya wamekabidhiwa vyumba vya madarasa pamoja na shule mbili mpya.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Kongwa, Dk. Omary Nkullo, alifanya makabidhiano hayo katika hafla iliyofanyika katika Kata ya Lenjulu na Chiwe wilayani humo.

Makabidhiano hayo yalihusisha vyumba vya madarasa 70, pamoja na shule mbili mpya katika Kijiji cha Ihanda na Masenha zenye thamani ya Sh. bilioni 1.4, ambazo zitatumiwa na wanafunzi wapya wa kidato cha kwanza mwakani.

Akipokea madarasa hayo kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan, Mwema aliwataka wananchi kuyatunza ili yatumike kama yalivyokusudiwa na kuongeza kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi.

Aidha, alisema jukumu la kuwapeleka watoto shule ni la kila mtu wakati huu serikali ikifuta ada shuleni.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kongwa alisema ujenzi wa madarasa hayo na shule hizo yamekamilika kwa asilimia 100 yakiwa na madawati yasiyopungua 40.

Diwani wa Kata ya Lenjulu, Brown Chisonjela, alizitaja baadhi ya kero zinazoikabili Shule ya Sekondari Lenjulu kuwa ni pamoja na upungufu wa walimu, ukosefu wa maji na mabweni kwa ajili ya wanafunzi wanaokaa mbali.

Alisema pamoja na kero hizo watoto wote wanapaswa kuripoti shule ifikapo Januari mwakani.

Jennifer Jackson mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Lenjulu, alisema pamoja na matatizo yaliyoko shuleni hapo lakini anaishukuru serikali kwa kuwapatia madarasa hayo.

Ujenzi wa madarasa hayo ulianza Oktoba mwaka huu ikiwa ni harakati za serikali kuongeza na kuboresha miundombinu ya elimu ili kuinua sekta ya elimu nchini.

# Rais Samia kuongoza maelfu mkesha kuliombea taifa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika mkesha wa kufunga mwaka wa kuliombea taifa utakaofanyika kesho katika viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma.

Mwenyekiti wa kamati ya mkesha huo kitaifa, Askofu Godfrey Mallasy, alibainisha hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya mkesha huo wa kitaifa.

"Kamati ya mkesha mkubwa wa kitaifa imeandaa mkesha maalum wa kitaifa kwa ajili ya kuliombea taifa utakaofanyika Desemba 31 kwenye viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma kuanzia saa 12 jioni hadi saa 12 asubuhi," alisema Askofu Mallasy. Aidha, alisema mgeni rasmi kwenye mkesha huo anatarajiwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan na viongozi wengine wakuu wa nchi walioko jijini hapo wanatarajiwa kushiriki katika mkesha huo kuliombea taifa," alisema Mallasy.

Alisema amani katika taifa ni moja ya nyenzo muhimu ya kuliinua kiuchumi na kukuza ustawi wa wananchi.

"Amani ndiyo kila kitu katika taifa leo hii tunaweza kufanya shughuli zetu kwa amani lakini kama kutakuwa hakuna amani hakuna kitakachoendelea, hivyo lengo la mkesha huu ni kuhakikisha kuwa tunatumia muda wetu kumwomba Mungu kuendelea kutudumishia amani yetu," alisema.

Kutokana na hali hiyo aliwataka wakazi wa Mkoa wa Dodoma pamoja na mikoa ya jirani kujitokeza kwa wingi kushiriki maombezi ya kuliombea taifa pamoja na viongozi wake.

Alisema mkesha huo umeandaliwa na Kanisa la Tanzania Fellowship of Churches (TFC) na kushirikiana na makanisa mengine mkoani hapo.

Alisema mkesha huo utajumuisha waumini wa dini zote na makanisa yote na kutumbuiza na kwaya mbalimbali, waimbaji binafsi wakiongozwa na timu ya kusifu na kuabudu ya The Unity Praise Team.

"Kaulimbiu ya mkesha huo kila mwaka ni amani, utulivu na ustawi nchi nzima, sauti moja, ambapo mkesha huu wa kuliombea taifa umekuwa ukifanyika kila mwaka tangu mwaka 1997," alisema.




Mjasiriamali wa miti ambaye jina lake halikupatikana akiwauzia wateja wake miche ya miti nje ya soko kuu la Majengo jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wajasiriamali wa majiko waomba eneo kufanya biashara

**Na Ibrahim Joseph,**
DODOMA

WAJASIRIAMALI wa kutengeneza bidhaa za majiko jijini Dodoma wameuomba uongozi wa halmashauri hiyo kuwasaidia kutenga eneo watakalolitumia kufanyika shughuli zao.

Mwenyekiti wa Kikundi cha Wajasiriamali Majengo, Kipara Saidi, alitoa ombi hilo jana alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu ugumu wa mazingira ya kufanya shughuli zao za kutengeneza majiko.

Mwenyekiti huyo alisema wanauomba uongozi wa Jiji la Dodoma kuwatafutia eneo rafiki la kufanyakazi zao katikati ya Jiji baada ya kuondolewa eneo la karibu na soko kuu kwa ajili ya kupisha kituo kipya cha daladala.

Saidi alibainisha kuwa awali baada ya kuondolewa katika eneo hilo uongozi wa Jiji uliwapangia kwenda eneo la Soko la Job Ndugai.

"Wakati wameanza operesheni yao za kusafisha mji na sisi tuliondolewa, hatuwezi kukataa kwamba isifanyike ni sawa tunachoomba watusaidie eneo hapa katikati ya mjini kutokana na aina ya biashara yetu," alisema.

Alisema waliomba kupewa nafasi eneo la Soko la Machinga lakini Jiji wakawapangia kuwa waende Soko la Ndugai.

Alisema kuwa kutokana na aina ya biashara zao za majiko wanazotengeneza haiwezekani mtu kutoka mjini kufuata mfuniko wa jiko katika Soko la Ndugai ambalo lipo mbali.

Kadhalika alisema wajasiriamali wapo zaidi ya 30 na kwa sasa wanafanyia shughuli zao pembeni ya Soko la Majengo baada ya kufukuzwa eneo la awali.

Alisema kundi hilo limekuwa likitoa mafunzo kwa vijana ili kujiajiri lakini kutokana na kukosa eneo la kufanyia kazi wameshindwa kuendelea kuwasaidia.

Naye Katibu wa Wajasiriamali hao, Iddy Kazumba, alisema walikataliwa kupewa eneo Soko la Machinga kwa madai kuwa wao ni wajasiriamali siyo machinga.

Alisema miundombinu iliopo Soko la Ndugai siyo rafiki kwa kazi zao kutokana na kutokuwa na umeme, hivyo wanaomba kutafutiwa eneo la mjini ili kuendeleza shughuli zao.

Hata hivyo alisema bidhaa wanazozalisha ni za gharama ndogo mwananchi hawezi kutumia nauli ya Sh. 2,000 kwenda Soko la Ndugai kufuata jiko peke yake.



# Pazia Mapinduzi kufunguliwa kibiashara

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

TAMASHA la Tisa la Biashara la Sherehe za Mapinduzi linatarajiwa kuzinduliwa leo visiwani Zanzibar na litatoa fursa kwa wafanyabiashara na wajasiriamali kutangaza na kuuza bidhaa zao.

Akizungumza jana na waandishi wa habari ofisini kwake Mjini Zanzibar kuhusu tamasha hilo, Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaaban, alisema tamasha hilo linatoa fursa ya soko kwa wafanyabiashara na wazalishaji wa ndani na nje.

Waziri Omar alisema lengo la tamasha hilo ni kutengeneza mtandao wa wajasiriamali na ni fursa pekee kwa taasisi za serikali ambazo zinatoa huduma mbalimbali zinazoendana na biashara wanazozifanya kushiriki.

Alisema tamasha hilo ni sehemu ya shamrashamra za kuadhimisha sherehe za Mapinduzi ya mwaka 1964 na kaulimbiu ya mwaka huu ni "Ushirikishwaji wa Jinsia Katika Maendeleo ya Biashara".

Sababu kubwa ya kaulimbiu hiyo, alisema ni kuona ushirikishwaji wa jinsia katika biashara ni moja ya ajenda kubwa za Umoja wa Afrika za ufanyaji wa biashara katika eneo huru la biashara limesisitiza kuzishirikisha jinsia zote ili kuondokana na dhana kuwa biashara ni suala la wanaume

"Jamii inapopigania usawa wa kijinsia, Wizara ya Biashara (na Maendeleo ya Viwanda) haiwezi kuwa nyuma lazima kuunga mkono jitihada hizo," alisema.

Aidha, alisema washiriki wa tamasha hilo ni wajasiriamali, wazalishaji, watoa huduma na taasisi za serikali na litakuwa na zaidi ya washiriki 400 kutoka Zanzibar, Tanzania Bara, Uganda, Kenya, Burundi, Siria, Iran na nchi zingine.

Kwa mujibu wa waziri, tamasha hilo pia litakuwa na shughuli zingine za kuhamasisha masuala mbalimbali ikiwamo siku maalum ya bidhaa za Zanzibar, siku ya Mkurabita ya kurasimisha biashara na kuhamasisha matumizi ya mkaa mbadala ili kutunza mazingira.

Waziri huyo alisema tamasha hilo kwa miaka tisa likichukua sura mpya ikiwamo kuwavutia na kuwaweka pamoja watu.

Alisema tamasha hilo limefadhiliwa na watu na taasisi mbalimbali na linatarajiwa kugharimu zaidi ya Sh. milioni 277.3.



Askari wa jiji wakipandisha bodaboda kwenye gari baada ya kuzikamata katika mtaa wa Samora jijini Dar es Salaam jana baada ya vijiwe vyote vya pikipiki katikati ya jiji kuvunjwa. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Miradi ya mabilioni kumaliza kero ya maji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI Mkuu wa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA), Dk. Salha Mohammed Kassim, amesema kukamilika kwa miradi miwili ya maji inayotokana na fedha za mkopo kutoka Benki ya Exim wa dola bilioni 92.18 na mradi wa ahueni ya UVIKO-19, utasaidia kupunguza tatizo la upatikanaji wa maji.

Dk. Salha alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake Kinazini Zanzibar, huku akibainisha kuwa tayari visima 64 vimeshajengwa kwa ajili ya upatikanaji wa huduma hiyo.

Alisema mradi huo utawanufaisha zaidi wananchi wa mkoa wa Mjini Magharibi na mikoa mingine jirani kwa sababu utakuwa na uwezo mkubwa wa kusambaza maji. Kwa sasa, alisema mradi huo umefikia asilimia 68 na mapema mwakani unatarajiwa kukamilika. "Mafundi wetu wanafanya kazi usiku na mchana ili kukamilika Machi, mwakani, kuna uwezekano mkubwa wa kukamilika," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Salha, mradi wa maji unaotokana na fedha za ahueni ya UVIKO-19 wenye thamani ya Sh. bilioni 32.2 ambao unachimba visima 38 unaendelea vizuri. Alisema mradi huo utachangia kwa upatikanaji wa majisafi na salama Zanzibar na kuwanufaisha wananchi wa Unguja na Pemba na tayari matangi ya kuhifadhi maji yanaendelea kujengwa ili kukamilika kwa wakati.

Mkurugenzi huyo alisema visima 38 vimeshakamilika na kwa hatua za kumalizika mradi mzima unatarajiwa kukamilika Machi, mwakani, na hatimaye kukabidhiwa kwa serikali.

Alisema hali ya upatikanaji wa maji Zanzibar imeongezeka kutoka asilimia 55 hadi kufikia asilimia 66 hivi sasa, hivyo kukamilika kwa miradi hiyo mikubwa inakwenda kuongeza asilimia 88 ya upatikanaji wa maji.

"Tumejipanga kuhakikisha huduma ya maji inapatikana bila changamoto yoyote," alisema. Katika kuhakikisha kuwa huduma hiyo kuwa bora, alisema wamejipanga kuagizia pampu za kisasa na kubwa ili patakapotokea tatizo, wananchi wanafungiwa kifaa haraka.

Alisema katika kuboresha uwendeshaji mamlaka hiyo hivi sasa wananchi wanalipia maji kupitia mfupo wa kielektroniki na kuwaondosha wananchi usumbufu wa kulipia maji na kuwafungia mita za maji.

# Matukio ya ukatili yazidi kuongezeka

**Na Mwandishi Wetu**

MATUKIO 177 ya udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa Novemba, mwaka huu, huku waathirika wakuu wakiwa wanawake na watoto.

Hayo yalisema jana kutokana na ripoti ya Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali iliyowasilishwa kwa vyombo vya habari juu ya matukio hayo kwa mwezi huo.

Akiwasilisha ripoti hiyo, Mtakwimu Ramla Hassan Pandu, alisema waathirika wakuu wa vitendo hivyo ni watoto 157 sawa na asilimia 88.7 miongoni mwao wakiwa wasichana 124 na wavulana 33.

Matukio kwa mwezi huo, alisema yameendelea kuongezeka kutoka 164 kwa mwezi Oktoba na kuonyesha kuwa vitendo vya udhalilishaji bado vinaendelea miongoni mwa wanajamii visiwani hapa.

Alizitaja wilaya za Mjini na Magharibi 'B' kuwa ndizo zilizoongoza kuwa na matukio mengi (matukio 47 kwa kila wilaya), ikifuatiwa na Magharibi 'A' iliyokuwa na matukio 40 huku wilaya ya Kaskazini 'B' na Kusini zikiwa na idadi ndogo zaidi ya matukio. Kila moja matatu.

Aidha, alisema vitendo vya ubakaji ndivyo vilivyoongoza vikiwa na matukio 84 (asilimia 47.5), kulawiti (20), kuingilia kinyume cha maumbile (tisa), kutorosha (10), shambulio la aibu/kukashfu (24) na shambulio 30.

"Magharibi 'B' imeripotiwa kuwa na idadi kubwa ya ubakaji ikiwa na matukio 20 (sawa na asilimia 23.8), ikifuatiwa na Mjini matukio 19 (sawa na asilimia 22.6)," alisema Ramla.

Alisema matukio 129 kati ya 177 yaliyoripotiwa yako chini ya upelelezi wa polisi (asilimia 72.9), matukio 45 yako Ofisi ya Mwendesha Mashtaka (asilimia 25.4) na matatu yapo mahakamani.

Mkurugenzi Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Wazee, Siti Abbas Ali, alisema jamii na wazazi wanahitaji kujenga ushirikiano katika malezi ili kuendelea kupunguza vitendo vya udhalilishaji.


Alisema kutokana na ukubwa wa tatizo la udhalilishaji lililoshamiri, kuna umuhimu kwa wanajamii kushirikiana na kila mmoja atapaswa kutoa ushirikiano ili kumaliza tatizo hilo.

Aidha, aliishauri jamii kurudi kwenye misingi ya malezi ya pamoja ya watoto ili kujenga jamii yenye mustakabali bora wa maisha kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

Naye Mkuu wa Divisheni ya Jinsia Wizara ya Ustawi wa Jamii, Jinsia na Watoto, Halima Abdulrahman Omar, alisema ili kupunguza vitendo vya udhalilishaji ikiwamo ubakaji, jamii inapaswa kuwekeza katika utoaji wa elimu na kuzungumza na watoto katika njia ya kuwaelewesha namna pia ya kujilinda.

Mkaguzi wa Polisi Makao Makuu ya Polisi Dawati la Jinsia, Makame Haji Haji, alisema ni vizuri kwa wazazi wakafuatilia nyendo za watoto wao kila siku tena kwa umakini ili kujua namna ya kuepusha vitendo vya udhalilishaji.

Uwasilishaji wa ripoti hiyo ya udhalilishaji chini ya Shirika la Umoja wa Mataifa linalohusika na masuala ya wanawake ni katika jitihada za kupambana na vitendo hivyo dhidi ya wanawake na wasichana.





Mafundi wa Shirika la Umeme (TANESCO) wilayani Muheza, mkoani Tanga, wakipakia nguzo katika lori eneo la Msangazi kwa ajili ya kuwasambazia umeme wananchi wa vijijini juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# TARURA yawaonya makandarasi barabara wababaishaji

**Na Restuta Damian,** KAGERA

WAKALA wa Barabara Mijini na Vijiji (TARURA) mkoani Kagera imewaonya makandarasi wanaomba kazi wakati hawana mitaji wala vifaa vya kufanyia kazi hiyo.

Akizungumza jana Mjini Bukoba katika kikao cha kwanza cha mwaka 2022/2023, kwa wajumbe wa Bodi ya Barabara, Meneja wa TARURA, Aviti Theodory alisema, wanapotangaza kazi hujitokeza makandarasi wengi kuomba, lakini baadhi yao wanapopata hushindwa kuifanya na kuimaliza kwa wakati kutokana na kukosa vifaa pamoja na mitaji.

Alisema tatizo hilo hufanya utekelezaji wa miradi hiyo kushindwa kukamilika ndani ya muda uliopangwa kati yao na mkandarasi.

"Unakuta mtu anaomba kazi, lakini akienda kwenye utekelezaji anakosa mitambo na anajikuta amevuka ule muda unaotakiwa," alisema Theodory.

"Kazi nyingi zinatolewa ndani ya miezi minne hadi sita ziwe zimekamilika lakini atakaa kutafuta mitambo ndani ya hiyo miezi hadi muda unaisha na sisi tunampiga adhabu ya kulipa fedha," alisema Theodory.

Aidha, alisema zipo shughuli za ujenzi na matengenezo ya ukarabati wa barabara na makaravati ngazi ya vijiji na halmashauri kulingana na uhitaji.

Alisema wakala inahudumia mtandao wa kilomita 6,403 kwa mkoa mzima na kilomita 106 zimewekewa lami na kilomita 6,297 zipo kwa kiwango cha changarawe na udongo.

Aliongeza kuwa mwaka 2022/2023, serikali iliwatengea bajeti ya Sh. bilioni 28.9.

# Waombwa kutoa maeneo bure kupisha mradi wa umeme

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

WAKAZI wa Mkoa wa Kagera hususani katika Manispaa ya Bukoba wameombwa kutoa maeneo yao bila kudai fidia ili kuruhusu Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kupitisha nguzo za umeme.

Lengo la hatua hiyo ni kuhakikisha wananchi wanapatiwa huduma hiyo kwa gharama ya Sh. 27,000, kupitia mradi wa kupeleka umeme kwenye maeneo ya pembezoni mwa miji, manispaa na majiji.

Akizungumza wakati wa kuzindua mradi huo katika Kata ya Ijuganyondo iliyoko katika Manispaa ya Bukoba, Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato, alisema kuwa mradi yote haina bajeti ya kulipa fidia.

Alisema makandarasi wanaotekeleza kazi hiyo wanafahamu kuwa kuna mazao ya wananchi katika mashamba, hivyo watatumia busara wakati wa utekelezaji.

"Nimeamua kulisema hili hapa kwa sababu ni mradi wa kwanza wa aina hii kwenu huko vijijini wanalijua hili, maana wananchi wakitaka kulipwa fidia gharama za mradi zitakuwa kubwa na serikali itashindwa kutimiza lengo lake la kuhakikisha wananchi wengi wananufaika na nishati hii," alisema.

Hivyo, aliwaasa viongozi wakiwamo wenyeviti wa serikali za mitaa, madiwani na vyama vya siasa wa maeneo ambayo mradi huo utapita, kukaa vikao na wananchi na kufanya mikutano ya haraka ili kukubaliana na mkandarasi wapi wapitishe laini za umeme.

Mkurugenzi Mkuu wa REA, Hassan Said, alisema wao pamoja na kwamba jukumu lao ni kupeleka umeme vijijini, lakini walifikia uamuzi wa kuwahudumia pia wananchi wanaoishi pembezoni mwa miji, manispaa na majiji, kutokana na maeneo hayo kuwa na watu ambao maisha yao hayana tofauti na wanaoishi vijijini.

Said alisema kuwa mradi huo utatekelezwa katika maeneo 47 na kwamba kati ya hayo 26 yapo katika Wilaya ya Bukoba na kuwataka wananchi kuondoa vikwazo kwa mkandarasi ili huduma hiyo iwafikie mapema. Diwani wa Kata Ijuganyondo, Ally Magimbi, aliishukuru serikali kwa kuona umuhimu wa kata yake kuwa miongoni mwa maeneo yatakayonufaika na mradi huo na kwamba wananchi wake wapo tayari kuupokea bila ya kikwazo chochote.

# Uhaba watumishi wa afya waitesa H'shauri ya Magu

**Na Vitus Audax,** MAGU

HALMASHAURI ya Wilaya ya Magu mkoani Mwanza inakabiliwa na uhaba wa watumishi wa afya hali inayosababisha ufanisi mdogo katika utoaji wa huduma kwa wagonjwa.

Imeelezwa kuwa halmashauri hiyo ina watumishi 486 ambao wanahudumia katika vituo vyote vya afya wilayani humo, ikiwa ni pamoja na zahanati na wale walioko katika Hospitali ya Wilaya.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Magu Dk. Mary Kapinga aliyasema hayo na kusema kuwa wilaya hiyo inakabiliwa na upungufu wa wahudumu wa afya kwa asilimia 50.

Alisema kuwa idadi ya watumishi wa afya ni wachache kulinganisha na mahitaji, hali ambayo kwa wakati mwingine imekuwa ikisababisha huduma kutolewa chini ya viwango vinavyotakiwa.

Dk. Kapinga alisema licha ya serikali kuimarisha sekta ya afya lakini bado kuna uhitaji wa wadau wa afya kuhakikisha wanaongeza juhudi ili kupatikana wahudumu wa kutosha.

Baadhi ya wanawake wajawazito waliomba serikali kuendelea kuimarisha huduma za afya ili kukabiliana na vifo vya watoto na mama wajawazito.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti baadhi ya wanawake wajawazito wilayani humo waliiomba serikali kuboresha utoaji wa huduma za afya katika hospitali na vituo vya afya kwa kuongeza watumishi pamoja na vifaa tiba.

Glory Molely alisema wahudumu wa afya hospitalini hapo wanajitahidi kutoa huduma kwa wakati japokuwa kuna wakati wanakosa huduma stahiki kutokana na uchache wao.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, alisema serikali inatambua upungufu wa watumishi akiahidi kushirikiana na serikali katika kutatua tatizo hilo.

# Bodaboda wachangamkia fursa za mikopo ya nishati

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

BODABODA zaidi ya 150 mkoani Mwanza wamepatiwa mkopo wa nishati mbadala ya gesi ikiwa ni hatua ya kudhibiti matumizi ya mkaa na kuni vinavyochangia ongezeko la vifo na hewa ya ukaa nchini.

Hatua hiyo itawezesha makundi mbalimbali kufikiwa na kupata mkopo ili kumiliki nishati hiyo na kuwanusuru na vifo vitokanavyo na matumizi ya nishati chafu na kuwa na taifa lenye watu wenye afya.

Akizungumza baada ya kutoa elimu ya faida za matumizi ya gesi, Meneja Mauzo wa Taifa Gesi, Kanda ya Ziwa, Victor Kihwili, alisema wanapambana kuhakikisha watu wanaondokana na matumizi ya mkaa na kuni na kutumia nishati safi.

Alisema wanaungana na serikali kuyafikia makundi tofauti ili kuifikia jamii yote iweze kutumia nishati hiyo na kwamba wao wameanza kutoa mkopo wa nishati hiyo kwa kundi hilo.

Alisema kuanzia sasa waendesha bodaboda watachukua gesi na kulipa ndani ya miezi miwili na tayari wamefanikiwa kutoa mkopo kwa zaidi ya watu 150.

Alisema ili kuokoa afya za Watanzania ni lazima ziwepo jitihada ili kunusuru hali hiyo, kwamba kupitia viongozi wa bodaboda watawawezesha kupata mkopo huo.

Mrakibu wa Jeshi la Polisi, Dastan Kombe, akimwakilisha Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza aliwataka bodaboda kuwa waaminifu, watii sheria bila kushurutishwa, wasiwe chanzo cha uhalifu na wachangamkie fursa zinazojitokeza kuboresha maisha yao.

Mmoja wa wandesha bodaboda, Yohana Kaholwe, aliiomba serikali na wadau wa gesi kuwa na nguvu ya pamoja ya uboreshaji huduma za upatikanaji wa nishati hiyo ili kuwawezesha wananchi wengi hususani wa kipato cha chini.

# Wataalamu wahadharisha kuzuka kirusi kipya Corona

**BEIJING, China**

WATAALAMU waonya huenda kukazuka aina mpya ya kirusi cha Corona, wakati huu ambao China inashuhudia kiwango kikubwa cha maambukizi katika mwezi huu, na hivi karibuni ikiondoa masharti.

Wataalamu hao wa masuala ya afya walisema jana kuwa wakati onyo hilo likitolewa baadhi ya mataifa ikiwemo Marekani ilitangaza masharti mapya kwa wasafiri kutoka China.

Katika wiki tatu za kwanza za mwezi Desemba pekee, inakadiriwa watu milioni 248 nchini China waliambukizwa virusi hivyo.

Aidha, hospitali na sehemu za kuchomea maiti zinatajwa zikielemewa katika taifa hilo ambalo hivi karibuni mamlaka ilitangaza kusitisha sera yake ya udhibiti wa maambukizi iliyokuwepo tangu kuzuka kwa janga hilo miaka mitatu iliopita.

Wataalamu wa afya wanahofia kwamba China itakuwa ni kitovu cha kuzalisha aina mpya ya virusi, ambapo hadi sasa vinaweza kusambaa miongoni mwa karibu moja ya tano ya watu duniani ambao hawana kinga ya kutosha na wale ambao hawajachanjwa.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Afya Ulimwenguni katika Chuo Kikuu cha Geneva, Antoine Flahault, aliliambia shirika la habari la AFP kwamba kila maambukizo mapya yanapoongezeka nafasi ya virusi hubadilika.

Hoja hiyo inaungwa mkono na Soumya Swaminathan, ambaye aliwahi kuwa mwanasayansi mkuu wa Shirika la Afya Ulimwenguni hadi mwezi Novemba, akisema mtu kutopata chanjo hasa kwa makundi ya wazee kunaongeza hatari.

"Sehemu kubwa ya wachina wako kwenye hatari ya kuambukizwa, kwa sababu wazee wengi hawajachanjwa au kupata chanjo ya nyongeza," alisema.

Pia alisisitiza kwamba kwa sasa kuna haja ya kuwa makini na aina nyingine za virusi vitakavyojitokeza.

MASHARTI MAPYA

Katika kuchukua hatua ya kudhibiti maambukizi hayo yanayoshuhudiwa kuongezeka, baadhi ya mataifa ikiwemo Marekani, Italia, Japan, India na Malaysia, wiki hii yametangaza masharti ya kiafya kwa wasafiri wanaoingia wakitokea China pamoja na maeneo yake maalum ya utawala ya Hong Kong na Makau.

Waziri Mkuu wa Italia, Anthony Albanese, alisema wanatekeleza ushauri wa wataalamu wa afya kwa kuhakikisha kila mmoja anapima kabla ya kuingia nchini humo.

"Tunachokifanya ni kuchukua hatua sio tu kwa sababu ni China, na tutafata ushauri wa wataalamu katika kujiondoa kwenye hatari, watu watapaswa kupima kabla ya kupanda ndege, hivyo kuna hatua mbalimbali tutazichukua," alisema.

Inaelezwa kuwa vituo vya udhibiti wa magonjwa nchini Marekani navyo vimetangaza hatua hiyo itakayoanza kutekelezwa kuanzia Januari tano, 2023 na wasafiri watalazimika kutoa taarifa zao za vipimo na chanjo dhidi ya corona kabla ya kuondoka.

Vile vile, inabainishwa kuwa India na Japani nazo zinatekeleza sharti la upimaji wa lazima wa kipimo cha PCR kwa abiria wote kutoka China, ikiwa ni njia moja wapo itakayosaidia, iwapo kuna ucheleweshwaji wa taarifa kutoka Beijing.

Mkuu wa taasisi ya kudhibiti virusi katika Kituo cha Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa China, Xu Wenbo, aliwaambia waandishi wa habari kwamba aina nyingine ndogo za Omicron zimegunduliwa hivi karibuni nchini China katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita.

**DW**



Rais wa Sudan Kusini, Salva Kiir akiwa katika hafla ya kuwaaga wanajeshi wa jeshi la watu wa Sudan Kusini, mjini Juba, wakielekea DRC kulinda amani. **PICHA: VOA.**

# Mawaziri 3 wajiuzulu DRC

**KINSHASA, DRC**

MAWAZIRI watatu nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) ambao ni wanachama wa chama cha mgombea urais Moise Katumbi wamejiuzulu baada ya rais wa nchi hiyo kutaka kufahamu ni nani wangemuunga mkono katika uchaguzi ujao.

Katumbi, mfanyabiashara tajiri ambaye aliwahi kuongoza eneo lenye utajiri wa madini la Katanga, alitangaza mapema mwezi huu kwamba atagombea nafasi ya rais katika uchaguzi uliopangwa kufanyika mwishoni mwa mwaka 2023.

Inaelezwa kuwa Rais Felix Tshisekedi aliwaita jana mawaziri watano ambao ni wanachama wa chama cha Katumbi cha Ensemble pour la Republique ili kujua msimamo wao na ndipo Waziri wa mipango, waziri wa uchukuzi na naibu waziri wa afya walipowasilisha baadaye ombi lao la kujiuzulu.

Tshisekedi, ambaye aliingia madarakani Januari mwaka 2019, tayari ametangaza kuwa ana nia pia ya kugombea muhula wa pili mwaka ujao.

**DW**

## Sudan Kusini yapeleka wanajeshi DRC

**JUBA, Sudan Kusini**

SUDAN Kusini imetuma wanajeshi 750 kujiunga na Kikosi cha Afrika Mashariki kinachojaribu kuleta amani mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) ambayo inakabiliwa na machafuko kwa muda sasa.

Rais wa Sudan Kusini Salva Kiir, alituma rasmi wanajeshi mashariki mwa DRC jana ili kujiunga na kikosi cha kanda ya Afrika Mashariki kinacholenga kumaliza miongo kadhaa ya umwagaji damu nchini humo.

Wanajeshi hao wanaungana na vikosi kutoka Kenya, Burundi na Uganda, katika kile kinachojulikana kama mtihani kwa uwezo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kujibu ghasia katika eneo hilo na kuleta utulivu. Akihutubia wanajeshi mjini Juba kabla ya kuondoka, Rais Kiir alishauri kikosi hicho kudumisha weledi wa hali ya juu.

"Mnakwenda na dhamira ya kufanikiwa kuleta amani Congo. Sasa mnakwenda kwenye jukumu la kulinda amani, kofia zenu pekee ndizo zitabadilika na kuwa za bluu, kwa sababu mtashiriki katika operesheni ya pamoja ya nchi zote za Afrika Mashariki. Nawasihi mkaonyeshe nidhamu na kufuata amri pamoja na kutekeleza maagizo," alisema Rais Kiir.

Pia aliwaagiza wanajeshi kutofanya uhalifu kama vile ubakaji.

"SPLA wakati wa mapambano ya ukombozi ilikuwa na nidhamu kubwa. Sitaki muende kusababisha vurugu au uhalifu. Msiende kufanya ubakaji wa wanawake na wasichana," alisisitiza Rais Kiir.

Waziri wa Ulinzi na Masuala ya wanajeshi wa zamani Angelina Teny, alisema kwamba kama mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Sudan Kusini ina mchango katika usalama na utulivu wa DRC.

"Tuliombwa kuchangia kikosi, na tumekuwa tukijiandaa kwa muda wote huu na kikosi kiko tayari. Wamepokea tu maagizo yao ya mwisho kutoka kwa rais na amiri jeshi mkuu, sasa watakuwa njiani kwa ajili ya operesheni hiyo," alisema Angelina.

Aliongeza kuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki imetoa uungaji mkono wa kikanda kwa kupelekwa kwa wanajeshi wa Sudan Kusini mashariki mwa DRC.

Alisema kupelekwa kwa wanajeshi wa nchi hiyo ni hatua nzuri inayofanywa na nchi inayopambana na maswala yake ya usalama.

Wanajeshi wa Sudan Kusini watawekwa katika mji wa Goma, ambako watafanya operesheni ya kurejesha hali ya kawaida katika eneo hilo, ambako wanajeshi wa Congo wanapambana na kundi la waasi la M23, ambalo linashutumiwa kuwalenga raia katika mzozo uliodumu kwa takriban muongo mmoja.

**VOA**

# HABARI PICHANI



Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama wakiwa ni miongoni mwa washiriki katika sherehe ya maadhimisho ya siku ya shukrani na furaha kwa Mlipakodi ambayo Rais wa Zanzibar Dk Hussein Mwinyi alitoa tuzo mbalimbali.



Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Dk. Juma Akili (kushoto) na Mawaziri wa Wizara tofauti wakimsikiliza Rais wa Zanzibar Dk Hussein Ali Mwinyi




Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Mwinyi, akikabidhi Tuzo ya wanaotoa ushirikiano zaidi kwa ukusanyaji kodi kwa Wilaya ya Kusini,Sheha wa Shehi ya Paje Mohamed Rajab (Shelisheli).



Wafanyakazi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRB) wakifuatilia kwa makini hotuba iliyotolewa na Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Mwinyi.



Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Mwinyi akimkabidhi Tuzo ya mlipa kodi mkubwa wa Bodi ya Mapato Zanzibar kwa Meneja Mkazi wa Kampuni ya Zanzibar Petroleum, Actaf Jiwan.

**PICHA ZOTE: IKULU**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOSEPHAT JEREMIA KAAYA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T 460 DNL** aina ya **TOYOTA- IST,** Chasis No.**NCP600107116.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi.

**Taarifa ya polisi**

**MWA/NYA/RB/493774/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SAFINA KHALFAN SELEMAN** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 531 DPN.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi.

**Taarifa ya Polisi:**

**ARU/ARU/RB/491305/2022.**

**TEGEMEZA AUCTION MART LIMITED**
**Kesi namba 56/22**
**Mdai: SAID ISIKE**
**Mdaiwa: DANFORD ELIASANTE**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Tunatoa siku 14 kwa mdaiwa kulipa deni lako. Baada ya huo muda kama hujalipa basi mali yako itauzwa kwa mnada.

| AINA YA MALI | TAREHE | MAHALI |
|---|---|---|
| Gari T 612 DDJ TOYOTA NOAH | 18/01/2023<br>Muda saa 4:00 Asubuhi | MBEZI BEACH BONDENI |

**MASHARTI YA MNADA**

Pesa italipwa asilimia 25% siku ya mnada baada ya siku 14 itamaliziwa 75% kama hautamaliza basi pesa uliyotoa awali haitarudishwa. Gharama za kubadili umiliki ni za mteja. Mali itauzwa kama ilivyo. Kwa mawasiliano piga simu namba **0719 187 677.**

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE — BBN Limited TZA

## OMBI LA KUELEZA MASLAHI KWA UTOAJI WA huduma za Kukata/Kuchonga na Kuchomelea Chuma.

## KUMB No. ETJ-BB-PR-EI-GEN-GE-0108

BESIX Ballast Nedam Limited, inayotekeleza kazi za awali za Ujenzi wa Gati na Kituo cha Kupakilia katika Ghuba ya Tanga kwa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), inakaribisha Makampuni ya kitaalamu kueleza nia yao kwa:

**Huduma za kukata/kuchonga na kuchomelea, na mashine za uchomeleaji**

Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.

Uendelezaji wa Mradi wa EACOP unahusisha uhandisi, ujenzi, uendeshaji na matengenezo ya bomba la kusafirisha mafuta ghafi linalovuka Uganda na Tanzania ikijumuisha Gati yenye Kituo cha Kupakia Mafuta kwa Meli za Mafuta, karibu na Tanga nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA VIFAA / HUDUMA:**

- Kukata/Kuchonga nguzo za chuma kwa ajili ya Kusawazisha
- Uchomeleaji wa Nguzo za chuma kwa eneo lenye kina kifupi (Semi-Automatic Weld with Travel Band)
- Uchomeleaji wa Nguzo za chuma kwa eneo lenye kina kirefu (Semi-Automatic Weld with Travel Band)
- Kuchomelea nguzo za chuma kwenye mihimili ya Gati eneo lenye kina kifupi (Manual Weld)
- Kupasha chuima joto kwenye maungio kwa kutegemea WPS na vifaa vingine
- Ugavi kwa ajili ya vifaa vya kuchomelea, kukata na kuchonga pamoja na vifaa vya matumizi muhimu.

**KIWANGO CHA MAHITAJI:**

Kampuni zinazoonyesha nia yao zinaalikwa kuandika ombi lao kwa:

- Wasifu wa kampuni wenye uthibitisho wa uwezo wa kutosha wa kifedha na rasilimali za kutosha na zenye uwezo kusimamia kandarasi
- Orodha ya uzoefu iliyo na historia ya ugavi / rekodi inayoonyesha uzoefu usiopungua miaka mitano (5) katika kutekeleza huduma zinazofanana za huduma za uchomaji chuma zinazohitajika kulingana na viwango vya kimataifa vinavyojulikana katika biashara ya Mafuta na Gesi au soko linalolinganishwa.
- Orodha ya wachomelea bomba za chuma waliofuzu au kuhitimu mafunzo husika.
- Orodha ya vifaa vya kuchomelea na kukata/kuchonga chuma
- Sera ya Ubora ya Kampuni na mipango ya Afya, Mazingira na Usalama eneo la kazi na uthibitisho wa ubora wa: ISO 9001:2015, ISO 14001:2015, OHSAS 18001 (ISO45001:2018), EN ISO 14732, EN ISO 90606-1, ISO 11484, EN ISO 90609-1, EN ISO 10893-8, 10893-11 au vyeti sawa
- Kuzingatia kanuni za mafuta ya petroli na utumiaji wa rasilimali za ndani (Local Content) ya 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Watoa Huduma kwa Wasambazaji wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha nia, unapendekezwa sana.

Makampuni yanayovutiwa ambayo yanakidhi mahitaji ya chini kabisa na yana uwezo wa kutoa huduma zilizoorodheshwa hapo juu yanapaswa kueleza nia yao kwa kutuma barua pepe pamoja na hati zilizoorodheshwa kwa **procurement@bbnjv.com (Ukubwa wa Juu wa Barua Pepe na viambatanishi: MB 20. & Nyaraka zote lazima ziwasilishwe kwa lugha ya Kiingereza)** mnamo au kabla ya **tarehe 14 Januari 2023, saa 12:00 jioni kwa Saa za Tanzania,**

Makampuni yanayokidhi kwa kuridhisha mahitaji ya chini kabisa yaliyo hapo juu yatatathminiwa na yakichaguliwa yataalikwa, kulingana na saini ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

**Kumbuka :** Kampuni zilizohitimu awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni yao ili kuendeleza mchakato wa Wito wa Zabuni.

## BURUDANI



# KIM: KANYE ANANIPA WAKATI MGUMU



MSANII Kanye West maarufu kama Ye anampa wakati mgumu sana Kim Kardashian hasa katika malezi ya watoto wao baada ya wazazi hao kuachana.

Katika mahojiano na Podcast ya mtangazaji, Angie Martinez, Kim amesema kushiriki kwenye suala la malezi na Ye ni jambo gumu sana.

Aidha, Kim aliweka wazi tofauti zake na Kanye hataki ziwaathiri watoto na namna wanavyomchukulia baba yao.

"Ninaweza kupitia magumu mengi, wakati nipo kwenye gari ninawapeleka shule, wanataka kusikiliza nyimbo za baba yao.

"Haijalishi ni yapi tunapitia, inabidi nitabasamu na niweke nyimbo zake na nicheze kama hakuna kibaya kilichotokea.

"Nikiwashusha tu na kurudi nyumbani, naangua kilio," alieleza Kim.

# DIAMOND: NITAPANDA JUKWAANI NA SIMBA



MSANII Diamond Platnumz amezua gumzo mitandaoni baada ya kudai anafikiria kuingia kwenye ukumbi wa kutumbuiza shoo yake ya kufunga mwaka akiwa na mnyama wa porini, Simba.

Katika video ambazo msanii huyo alizipakia kwenye Instagram yake, alionekana akifanya ziara kwenye ukumbi wa shoo hiyo ambao maandalizi kabambe yalikuwa yanaendelea na yeye kuonekana amesimama na msanii, Young Lunya.

Katika video hiyo, alisema alikuwa anajaribu kumchorea taswira kamili Lunya jinsi anapanga kupanda kwenye steji na Simba.

"Nikimwelewesha Young Lunya jinsi nitakavyoingia naye Simba stejini. Lakini mwenyewe kaonekana kama ana hofu na hakubaliani kabisa na wazo la mimi kuingia stejini na Simba.

"Naendelea kusisitiza Simba ndio bao za shoo na nikimwomba yeye awe ndio kama anamleta hivi, ili kesho hadithi iwe mbuzi ndio kamleta Simba," Diamond aliandika kwa utani.

Shoo hiyo kwa jina la Cheers inatarajiwa kufanyika kwenye Ukumbi wa Ramada ambapo Diamond na msanii wake Zuchu, watatumbuiza.

# JOKATE ATAJA JINA LA MTOTO WAKE

MKUU wa Wilaya ya Temeke jijini, Dar es Salaam, Jokate Mwegelo amefichua sura ya mtoto wake mchanga na kutangaza jina lake.

Jokate ambaye alijifungua wiki chache zilizopita, aliweka hadharani picha akiwa amempakata mtoto wake mchanga mikononi huku akiwa amejawa na furaha tele.

Alitangaza jina la mtoto huyo ni Totoo na kuwataka watu kuanzia sasa kukoma kumuita Jokate bali wamuite mama Totoo.

"Jina lake ni Totoo. Niite mama Totoo, Shukrani zote ni kwa Mungu," aliandika kiongozi huyo.

Jokate ambaye alikuwa ni mfanyabiashara na mtangazaji, aliteuliwa na hayati Rais John Magufuli kama Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe mwaka 2018

# YANGA YAIFUATA MTIBWA BILA NYOTA WAKE WATATU

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Yanga kiliondoka jijini Dar es Salaam jana kuelekea Morogoro kwa ajili ya kuivaa Mtibwa Sugar ikiwakosa wachezaji wake watatu, Feisal Salum 'Feitoto', Denis Nkane na Aboutwalib Mshery kutokana na sababu mbalimbali lakini wakiahidi kuwapa wanachama na mashabiki wao zawadi nzuri ya mwaka mpya.

Feitoto hayupo kambini kutokana na mgogoro wake wa kimaslahi na klabu hiyo, Nkane na Mshery ni majeruhi.

Ofisa Habari wa Yanga, Ally Kamwe, alisema jana wamejindaa vyema kuelekea mechi hiyo itakayochezwa kesho kwa sababu wanataka kufunga mwaka 2022 kwa kutowasononesha mashabiki wao.

"Tunakwenda kuwapambania wanachama na mashabiki wa Yanga kwa kuhakikisha tunauaga vizuri mwaka 2022 na tunaingia vizuri mwaka 2023. Nakumbuka sikukuu ya Krismasi tuliwapa zawadi mashabiki pale kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kwa kuifunga Azam FC mabao 3-2, kwa maandalizi tuliyonayo, tunaamini tunakwenda tena kuuaga mwaka vizuri," alisema Kamwe.

Kuhusu wachezaji majeruhi, Kamwe alisema Nkane atakuwa nje kwa muda wa wiki sita huku Mshery afya yake inaendelea vizuri.

"Nkane aliumia na sasa ni majeruhi, kwa mujibu wa madaktari wetu atakuwa nje kwa muda wa wiki sita, wiki nne za kuwa mbali kabisa na uwanja, na wiki mbili zitakazofuata ataanza mazoezi mepesi, kabla ya kujiunga na wenzake, Mshery yeye muda mrefu ni majeruhi lakini kwa sasa anaendelea vizuri na muda si mrefu anaweza kuonekana uwanjani," alisema ofisa huyo.

Yanga itakuwa inajaribu kuendeleza wimbi la ushindi kwa mechi ya sita mfululizo, baada ya kupoteza kwa mara ya kwanza mabao 2-1 dhidi ya Ihefu SC iliyochezwa Novemba 29, mwaka huu.

Baada ya hapo, mabingwa hao watetezi wameshinda mechi tano mfululizo, ikichapa Prisons bao 1-0, mabao 2-0 dhidi ya Namungo, ikachapa Polisi Tanzania mabao 3-0, na idadi kama hiyo ya mabao ikageuzwa na Costal Union, kabla ya kuadhibu Azam FC mabao 3-2 Desemba 25, mwaka huu.

Ikimaliza mechi hiyo, Yanga itaelekea Zanzibar kushiriki mashindano ya Kombe la Mapinduzi yanayotarajiwa kufanyika kuanzia Jumapili ikishirikisha timu 11 za hapa ndani na Aigle Noir kutoka Burundi.



Wachezaji wa Yanga, Dickson Job (kushoto) na Mkongomani, Jesus Moloko wakionyesha pozi ya kulala baada ya kumaliza mazoezi jana asubuhi na kusafiri kuelekea Morogoro kuifuata Mtibwa Sugar. **PICHA: MTANDAO**

# Kanda, Shikalo watemwa Mtibwa

**Na Hadija Mngwai**

MTIBWA Sugar imetangaza kuachana na nyota wake wanne akiwamo mlinda mlango, Farouk Shikalo na Deo Kanda na nafasi zao zitachukuliwa na wachezaji wengine kwa ajili ya kuboresha kikosi cha timu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo inaendelea.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Mtibwa Sugar yenye pointi 24 iko katika nafasi ya nane.

Akizungumza na gazeti hili, Ofisa Habari wa Mtibwa Sugar, Thobias Kifaru, alisema tayari wameshawafungulia mlango wa kwaheri wachezaji wanne ili kupisha usajili wa dirisha dogo ufanyike kwa ufanisi.

"Kuna mapendekezo ya Kocha, Salum Mayanga ameyatoa na uongozi unayafanyia kazi, kuna nyota ambao tunawahitaji tunafanyanao mazungumzo na yakishakamilika basi watu watawaona uwanjani," alisema Kifaru.

Aliwataja wachezaji wengine ambao wamewaacha ni pamoja na Hamadi Juma na Nickson Kibabage ambaye amekwenda Singida Big Stars.

"Lengo letu tunahitaji kuwa na kikosi kilicho bora na chenye ushindani katika michezo iliyobakia ya mzunguko wa pili na hatimaye kumaliza msimu katika nafasi za juu," alisema Kifaru.

Mtibwa Sugar ambayo imetoka kuchapwa mabao 3-1 na Ihefu SC, kesho itawakaribisha Yanga kwenye Uwanja wa Manungu, ulioko Turiani mkoani Morogoro.

## Dodoma Jiji FC kusajili wapya 2

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kumnasa, Adeyum Suleiman kutoka Geita Gold, Dodoma Jiji FC iko mbioni kukamilisha usajili wa wachezaji wengine wapya wawili ambao watasaidia kuongeza nguvu kwenye mechi za hatua ya lala salama zilizobakia.

Mjumbe wa Kamati ya Usajili ya Dodoma Jiji, Fredrick Mwakisambwe, aliliambia gazeti hili baada ya kumpata Adeyum, sasa wanafanyia kazi mapendekezo ya Kocha, Melis Medo kwa kusajili mshambuliaji na kiungo wa kati.

"Tumeanza na eneo la beki wa kushoto, eneo hilo lilikuwa na mapungufu kutokana na mchezaji wetu mmoja kuwa majeruhi, sasa tulikuwa tunamtumia winga, Emmanuel Martin, kwa kipindi hiki kirefu, tumeona kuna haja ya kuongeza nguvu eneo hilo.

Lakini bado mwalimu ameendelea na tathmini yake, amesema kuna eneo la ushambuliaji linatakiwa kufanyiwa kazi, ikibidi pia eneo na kiungo ili mwisho wa siku kikosi kizidi kuimarika zaidi," alisema mjumbe huyo.

Dodoma Jiji inatarajiwa kuikaribisha Kagera Sugar katika mechi ya raundi ya 19 ya ligi hiyo itakayochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini, Dodoma.

## Mkwawa Queens yalia na mastraika

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania ikiwa imesimama kupisha kambi ya timu za taifa, Kocha Mkuu wa Mkwawa Queens ya Iringa, Shaaban Zanzibar, amesema tatizo kubwa linaloisumbua kikosi chake ni umaliziaji mbovu.

Akizungumza na gazeti hili, Shaaban, alisema mastraika wake wanashindwa kutumia vye nafasi wanazozipata na kuisababishia matokeo mabaya timu hiyo.

Kocha huyo alisema amebaini safu yake ushambuliaji inahitaji kuongeza umakini ili kumaliza tatizo hilo na anaamini watazinduka na kupata ushindi.

"Tumepoteza mechi mbili mfululizo na lakini kuna mapungufu tumeyaona, nimeanza kuyafanyia kazi, tumemaliza sikukuu na sasa tumeanza tena mazoezi, pia tulianza kwa kucheza na timu kubwa ambazo zimetusaidia kugundua mapungufu," alisema kocha huyo.

Mkwawa Queens ilianza ligi kwa kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya The Tigers Queens na mchezo uliofuata ilikutana na kipigo cha mabao 4-0 kutoka kwa Yanga Princess na mchezo wake uliopita ilifungwa magoli 2-0 na Fountain Gate Princess.

## ZISIKUPITE

### JUDE KIPAUMBELE MADRID

REAL Madrid itaweka kipaumbele mpango wa kumnunua kiungo wa kati wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya England, Jude Bellingham, hapo mwakani huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19 akitarajiwa kuchagua Timu ya Hispania badala ya Liverpool. ***(Goal)***

### GREALISH KUMBADILI LEAO

KLABU ya Manchester City iko tayari kuwapa AC Milan kiungo wao wa kati, Jack Grealish mwenye umri wa miaka 27, ili kubadilishana na mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ureno, Rafael Leao mwenye miaka 23. ***(Calciomercato)***

### JOAO APANDISHWA DAU

KLABU za Manchester United, Arsenal na Chelsea zina mashaka kuhusu kufikia ada ya uhamisho wa mkopo ya Atletico Madrid ya pauni milioni nane kwa ajili ya mshambuliaji wake wa Ureno, Joao Felix mwenye umri wa miaka 23. ***(Sport)***

### JURANOVIC ATAKIWA CHELSEA

CHELSEA wanavutiwa na mlinzi wa Celtic na Timu ya Taifa ya Croatia, Josip Juranovic, mwenye umri wa miaka 27 kama mbadala wa Reece James (23) ambaye kwa sasa ni majeruhi. ***(Sky Sports)***

### DUMFRIES AGOMBEWA EPL

CHELSEA pia inamtazama mlinzi wa Inter Milan na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Denzel Dumfries, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 pia akiwa kwenye rada za Manchester United. ***(La Gazzetta dello Sport)***

### NEWCASTLE YAMTEMA JORGINHO

KLABU ya Newcastle United imefutilia mbali uwezekano wa kumsajili kiungo wa kati wa Chelsea, Jorginho mwenye umri wa miaka 31. ***(Football Insider)***

### MILINKOVIC KUTUA ARSENAL

ARSENAL ipo katika nafasi nzuri ya kumsajili kiungo wa kati wa Lazio na Timu ya Taifa ya Serbia, Sergej Milinkovic-Savic mwenye umri wa miaka 27. ***(Corriere dello Sport, via Express)***

### MUDRYK KUIKAMUA ARSENAL

KLABU ya Shakhtar Donetsk imesema inataka karibu euro milioni 100 kwa ajili ya winga wa Timu ya Taifa ya Ukraine, Mykhailo Mudryk mwenye umri wa miaka 21, ambaye anaripotiwa kuwa ni chaguo la kwanza la Arsenal. ***(Clciomercato)***

### UNITED KUTOSAJILI JANUARI

MANCHESTER United itajielekeza zaidi kusajili katika dirisha la usajili la majira ya joto mwaka ujao badala ya kutumia dirisha la Januari. ***(Sky Sports)***

### UNITED YAMTAKA MORATA

MSHAMBULIAJI wa Atletico Madrid na Timu ya Taifa ya Hispania, Alvaro Morata mwenye umri wa miaka 30 ameripotiwa kusakwa kwa mkopo na Manchester United. ***(ESPN)***

### MKOREA ANUKIA UNITED

MCHEZAJI mmoja kwenye orodha ya wanaosakwa na Manchester United ni mlinzi wa Napoli na Timu ya Taifa ya Korea Kusini, Kim Min-jae mwenye umri wa miaka 26. ***(Italia)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE: NGUVU ZOTE SASA NAZIELEKEZA PSG

●●● Asema bado maumivu ya kufungwa na Argentina yanamsumbua ingawa...

**PARIS, Ufaransa**

KYLIAN Mbappe hatasahau kichapo cha Ufaransa katika fainali ya Kombe la Dunia kutoka kwa Argentina hivi karibuni, lakini fowadi huyo amesema kwa sasa akili yake imejikita zaidi kwa Paris Saint-Germain.

Licha ya kufunga mabao matatu 'hat-trick' kwa kikosi hicho cha Kocha, Didier Deschamps, kwenye fainali, Mbappe na wachezaji wenzake walilikosa kombe hilo baada ya kufungwa kwa penalti kule Qatar.

Wakati mchezaji mwenzake, Lionel Messi bado hajarejea Paris baada ya ushindi wake, Mbappe alirudi haraka kwenye uwanja wa nyumbani, na kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Strasbourg katika mechi ya Ligi Kuu Ufaransa iliyochezwa juzi huku Neymar akitolewa nje kwa kadi nyekundu.

Akizungumza baada ya kufunga penalti dakika ya 96 aliyojishindia mwenyewe, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 alikiri machungu ya kupoteza kwa Ufaransa kule Doha atakaa nayo milele, lakini alisisitiza haoni wachezaji wenzake wanapaswa kulipa gharama ya hisia hizo.

"Binafsi, sitawahi kukataa," alisema. "Lakini klabu yangu haiwajibiki kwa kushindwa timu ya taifa. Ninajaribu kurejea na nguvu chanya.

"Nilijaribu kuleta nguvu kwa timu yangu, na tunatumaini kuendeleza msimu wetu bila kushindwa. Lilikuwa Kombe la Dunia - klabu haina uhusiano wowote nayo."

Aliporejea PSG kwa haraka kutoka katika majukumu ya kimataifa, Mbappe alisisitiza dhamira yake ya kuweka mambo ya klabu na nchi tofauti, na kuongeza: "Ujumbe ni rahisi.

"Inaonyesha haijalishi nini kitatokea kwa timu ya taifa, PSG ni kitu kingine. bado tumedhamiria kubeba kila taji."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,062,0
MECHI KALI
SIMBA
VERSUS
TANZANIA PRISONS
1 | 1.11
X | 5.07
2 | 11.77
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom | m-pesa
halopesa
airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# FIRMINO AKILI YOTE KURUDISHA KIWANGO



**LIVERPOOL, England**

ROBERTO Firmino "alichanganyikiwa" kwa kutoitwa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya Brazil na kukosa kucheza Kombe la Dunia, lakini sasa amesisitiza hiyo atatumia kama motisha kwake.

Fowadi huyo wa Liverpool alikosekana kwa mshangao kwa kocha mkuu Tite kwa michuano hiyo iliyofanyika Qatar, ambapo Brazil ilitolewa katika hatua ya robo fainali kwa penalti na Croatia.

Firmino alikuwa ameanza vyema msimu huu katika ngazi ya klabu, akifunga mabao tisa na kuandikisha asisti nne kwenye mechi 21 alizocheza, (akianza michezo 16).

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 alisema hiyo ilikuwa sehemu ya "mpango wa Mungu", na anatumaini inaweza kumtia moyo kuimarika zaidi.

"Bila shaka ilisikitisha kutoitwa kwenye Kombe la Dunia, lakini kama nilivyosema hapo awali, hiyo ni sehemu ya mpango wa Mungu na ninafuata mpango wa Mungu," alisemaakiiambia talkSPORT.

"Kwa kweli inanipa motisha zaidi na zaidi kutokwenda Kombe la Dunia, kwa hiyo nitafanya bidii kurejea Selecao."

# Gakpo: Van Dijk alinishawishi

**LIVERPOOL, England**

CODY Gakpo amebainisha ushawishi wa Virgil van Dijk ndio uliochangia kwenye uamuzi wake wa kujiunga na Liverpool baada ya Wekundu hao kuthibitisha rasmi kuwasili kwake kutoka PSV Jumatano.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi amesajiliwa na kikosi cha Kocha, Jurgen Klopp kwa uhamisho unaodaiwa thamani ya pauni milioni 37 kutokana na msimu wa kuvutia wa Kombe la Dunia.

Kuwasili kwa Gakpo hapo Merseyside ni kichocheo kikubwa kwa vijana wa Klopp na pigo kwa wapinzani wao Manchester United, ambapo fowadi huyo alikuwa amepigiwa upatu kuungana na raia mwenzake wa Uholanzi, Erik ten Hag.

Akizungumza na tovuti ya Liverpool baada ya kumaliza uhamisho wake, Gakpo alisema ni Mholanzi mwingine aliyemsaidia kumshawishi.

"Wakati huo nilikuwa napigiwa simu na kocha aliingia ofisini na kuniona," alisema Gakpo alisema kuhusu Van Dijk.

"Tulizungumza kidogo. Tulizungumza mengi kupitia simu.

"Alichoniambia hii ni hatua sahihi kwangu kufanya uamuzi, kukuza kipaji na kuwa mchezaji bora, klabu ni kubwa, lakini pia kama familia halisi.



078,169/-

# FEITOTO AIBUKIA ZANZIBAR AKIISAIDIA JKU KUSHINDA

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**



WAKATI Yanga ikitua salama mkoani Morogoro, kiungo wake, Feisal Salum maarufu kama Feitoto aliisaidia timu yake ya zamani, JKU FC kupata ushindi dhidi ya Mlandege katika mechi ya kirafiki iliyochezwa kwenye Uwanja wa Amaan jana asubuhi.

Feitoto alifunga bao moja wakati JKU ilipopata ushindi wa mabao 4-2 katika mchezo huo wa kujiandaa na hatua ya mwisho ya Ligi Kuu Zanzibar ambayo kwa sasa itasimama kupisha mashindano ya Kombe la Mapinduzi yatakayofanyika kuanzia keshokutwa visiwani hapa.

"Naomba nisiongee chochote, naomba sana, ikifika siku ya kuzungumza, nitaongea" kiungo huyo wa Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars) alisema.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa JKU, Khatib Shazir alisema, timu hiyo haijamsajili Feitoto na huwa ana kawaida ya kwenda kufanya mazoezi nao anapokuwa Unguja kwenye mapumziko.

"Leo (jana) alikuwa kufanya mazoezi kama kawaida yake, lakini tulikuwa na mechi ya kirafiki kujiandaa na mzunguko wa lala salama hivyo akaona ni vyema ajumuike na wenzake," Shazir alisema.

Kutokana na kutoonekana kambini, Feitoto alishaondolewa katika mipango ya benchi la ufundi la Yanga ambayo kesho itaivaa Mtibwa Sugar kwenye Uwanja wa Manungu, Turiani mkoani Morogoro.

Wakati huo huo Ofisa Habari wa Yanga, Ally Kamwe alisema, mara baada ya mchezo wa kesho kumalizika, klabu hiyo itatoa taarifa rasmi kuhusiana na hatma ya kiungo huyo Mzanzibari.

# SIMBA, PRISONS

INATOKA UK. 32

ya kuwapo kwa tofauti ya pointi sita dhidi ya vinara na mabingwa watetezi, Yanga, lakini pointi hizo ni ndogo kwa klabu kubwa kama Simba.

Kocha Msaidizi wa Tanzania Prisons, Shaban Mtupa, alisema wamejipanga vizuri na wanatambua wanakutana na Simba yenye wachezaji wazuri na wakubwa ambao wanaweza kuwapa matokeo chanya wakati wowote.

Mtupa alisema wanatambua umuhimu wa mchezo huo kwa sababu ya uzoefu wa wachezaji wa Simba, wataongeza umakini kuhakikisha wanazuia wapinzani wao kufika kwenye lango lao na kupunguza mashambulizi ya mara kwa mara.

"Tumejipanga vizuri, tumeona ubora wa wapinzani wetu na tumejiimarisha katika kila idara ikiwamo safu ya ulinzi, tutakuwa makini na washambuliaji wa Simba, lakini na washambuliaji wetu nao wanatakiwa kutumia vyema nafasi wanazotengeneza ili kupata matokeo mazuri," alisema Mtupa.

Simba yenye pointi 41 iko katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi hiyo nyuma ya Yanga yenye pointi 47 wakati nafasi ya tatu inashikiliwa na Azam FC yenye pointi 38.

Mechi nyingine za ligi hiyo zitakazochezwa leo ni Dodoma Jiji FC wakatikaribisha Kagera Sugar huku Singida Big Stars ikiwaalika Geita Gold FC kutoka mkoani Geita.

# YANGA, AZAM FC

INATOKA UK. 32

kupiga hodi Azam kwa ajili ya kuanza mchakato wa kuwasajili nyota hao.

"Azam wametupa muda wa kusubiri na tunaamini Yanga ni timu kubwa na mzigo upo wa kutosha kabisa, kwa ajili ya kukamilisha kupata huduma ya wachezaji hao. Kuhusu idadi ya wachezaji wa kigeni nani ataacha kupisha hao wataweka wazi baada ya kufanikiwa," Kamwe alisema.

Aliongeza kutokana na Fei Toto kutoonekana kambini, klabu inaendelea na vikao vya ndani ili kuamua hatima ya mchezaji huyo ambayo itatangazwa hivi karibuni.

"Fei Toto bado ni mchezaji halali wa Yanga, kama kuna klabu inamhitaji mchezaji huyo basi ifuate taratibu zote na kuja mezani kama tulivyofanya sisi kwa Azam FC tulivyowaambia tunawahitaji wachezaji wao wawili, kusikiliza ofa yetu," aliongeza.

Fei Toto jana alionekana kwenye Uwanja wa Amaan, Zanzibar na kuisaidia JKU kupata ushindi wa mabao 4-2 katika mechi ya kirafiki dhidi ya Mlandege.


# SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 31/12/22 | 18:00 | AFC Bournemouth vs Crystal Palace | 2.80 | 3.20 | 2.48 |
| 02. 31/12/22 | 18:30 | Hapoel Tel Aviv FC vs Maccabi Netanya FC | 2.55 | 3.35 | 2.65 |
| 03. 31/12/22 | 18:30 | Sekhukhune United vs AmaZulu FC | 2.50 | 2.85 | 3.10 |
| 04. 31/12/22 | 19:00 | Bnei Sakhnin FC vs Hapoel Haifa FC | 2.49 | 3.20 | 2.80 |
| 05. 31/12/22 | 20:10 | FC Ashdod vs Hapoel Jerusalem FC | 2.65 | 3.20 | 2.65 |
| 06. 01/01/23 | 15:00 | Blackburn Rovers vs Cardiff City | 2.18 | 3.35 | 3.25 |
| 07. 01/01/23 | 17:00 | Angers SCO vs FC Lorient | 2.90 | 3.25 | 2.40 |
| 08. 01/01/23 | 18:00 | Crewe Alexandra vs Tranmere Rovers FC | 2.75 | 3.20 | 2.55 |
| 09. 01/01/23 | 18:00 | Doncaster Rovers vs Carlisle United | 2.49 | 3.25 | 2.80 |
| 10. 01/01/23 | 18:00 | Hartlepool United vs Harrogate Town | 2.65 | 3.25 | 2.60 |
| 11. 01/01/23 | 18:00 | Grimsby Town vs Stockport County FC | 3.05 | 3.25 | 2.31 |
| 12. 01/01/23 | 18:00 | Walsall FC vs Mansfield Town | 2.60 | 3.25 | 2.65 |
| 13. 01/01/23 | 18:00 | Morecambe FC vs Burton Albion | 2.70 | 3.45 | 2.45 |
| 14. 01/01/23 | 18:00 | Blackpool vs Sunderland AFC | 2.85 | 3.15 | 2.49 |
| 15. 01/01/23 | 18:00 | Huddersfield Town vs Luton Town | 2.80 | 3.25 | 2.49 |
| 16. 01/01/23 | 18:00 | Colchester United vs Swindon Town | 2.95 | 3.20 | 2.36 |
| 17. 01/01/23 | 20:00 | Hapoel Hadera FC vs Maccabi Bney Reine | 2.40 | 3.15 | 3.00 |

# MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## IJUMAA - 30/12/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 11:45 | 3598 | Western United vs Brisbane Roar | 2.19 | 3.28 | 3.19 |
| 15:30 | 3254 | Singapore vs Vietnam | 11.61 | 6.00 | 1.18 |
| 15:30 | 3828 | Al Fateh (KSA) vs AL Faiha | 1.56 | 4.00 | 5.60 |
| 16:00 | 3834 | Singida BS FC vs Geita Gold FC | 2.10 | 2.81 | 3.74 |
| 16:00 | 5184 | Ahi Nazareth vs Maccabi Petach Tikva | 3.40 | 3.40 | 2.07 |
| 16:00 | 5260 | Nazareth Ilit vs Ironi Tiberias | 3.25 | 3.35 | 2.16 |
| 16:00 | 5425 | Hapoel Afula vs SC Kfar Qasem | 2.35 | 3.26 | 2.96 |
| 16:00 | 5596 | Hapoel Petah Tikva vs Maccabi Jaffa | 2.23 | 3.20 | 3.25 |
| 16:30 | 3831 | Mamelodi Sundowns vs Orlando Pirates | 1.71 | 3.52 | 4.76 |
| 18:00 | 2116 | Smouha Club vs Ghazl EL Mahallah | 2.31 | 2.84 | 3.44 |
| 18:00 | 4251 | US Monastir vs EO Sidi Bouzid | 1.27 | 4.56 | 10.67 |
| 18:00 | 4288 | Al Wehda vs AL Adalh | 1.83 | 3.31 | 4.51 |
| 18:15 | 1680 | Simba vs Tanzania Prisons | 1.11 | 5.07 | 11.77 |
| 18:30 | 1151 | Cape Town City vs Bloemfontein Celtic | 2.11 | 3.07 | 3.57 |
| 18:30 | 4668 | Stellenbosch vs Chippa Utd | 2.14 | 2.87 | 3.81 |
| 19:00 | 5335 | Bordeaux vs Sochaux | 2.12 | 3.27 | 3.32 |
| 19:00 | 5339 | Getafe vs Mallorca | 2.71 | 2.71 | 3.01 |
| 19:30 | 1437 | Generation Foot vs ASC Diambars | 2.50 | 2.70 | 3.35 |
| 19:30 | 3267 | ASC Jaraaf vs Teungueth | 2.48 | 2.75 | 3.30 |
| 20:00 | 1069 | National Bank vs Arab Contractors | 2.53 | 2.73 | 3.18 |
| 20:00 | 4368 | GD Chaves vs Famalicao | 2.37 | 3.14 | 2.99 |
| 20:15 | 4961 | Dodoma FC vs Kagera Sugar | 2.90 | 2.90 | 2.60 |
| 20:30 | 3860 | Maritzburg Utd vs TS Galaxy FC | 2.73 | 2.83 | 2.78 |
| 20:30 | 4406 | SuperSport Utd vs Marumo Gallants FC | 2.18 | 2.78 | 3.82 |
| 20:30 | 5453 | Al Shabab Riyadh vs Al-Ettifaq | 1.42 | 4.69 | 6.59 |
| 20:45 | 2909 | Newtown AFC vs Aberystwyth Town | 1.32 | 5.06 | 6.81 |
| 21:05 | 5412 | St Etienne vs Caen | 2.47 | 3.12 | 2.82 |
| 21:15 | 1311 | Celta Vigo vs Sevilla FC | 2.17 | 3.26 | 3.31 |
| 21:15 | 1795 | Cadiz CF vs Almeria | 2.32 | 3.10 | 3.15 |
| 22:00 | 2452 | FC Vizela vs Vitoria Guimaraes | 2.21 | 3.24 | 3.19 |
| 22:45 | 2008 | Newry City AFC vs Glenavon | 3.55 | 3.60 | 1.85 |
| 22:45 | 2263 | Cardiff Met Uni. vs Penybont | 1.91 | 3.40 | 3.55 |
| 22:45 | 2511 | Birmingham vs Hull City | 1.98 | 3.32 | 3.66 |
| 22:45 | 3152 | Lincoln vs Bolton | 3.22 | 3.32 | 2.14 |
| 22:45 | 3214 | Bala Town vs Caernarfon Town | 1.29 | 5.27 | 7.42 |
| 22:45 | 3751 | Norwich City vs Reading | 1.73 | 3.56 | 4.54 |
| 22:45 | 4637 | Derby vs Cambridge Utd | 1.50 | 3.98 | 6.16 |
| 22:45 | 4920 | Swansea vs Watford | 2.21 | 3.26 | 3.11 |
| 22:45 | 5223 | Stoke City vs Burnley | 3.02 | 3.27 | 2.26 |
| 22:45 | 5649 | West Ham vs Brentford | 2.00 | 3.43 | 3.48 |
| 23:00 | 1019 | Guingamp vs US Quevilly Rouen | 1.93 | 3.31 | 3.86 |
| 23:00 | 1108 | Bastia vs Valenciennes | 2.21 | 3.06 | 3.31 |
| 23:00 | 1972 | Rodez Aveyron vs Dijon | 3.06 | 3.01 | 2.38 |
| 23:00 | 2112 | Laval vs Amiens | 2.63 | 3.07 | 2.68 |
| 23:00 | 2186 | Liverpool vs Leicester | 1.26 | 5.73 | 8.70 |
| 23:00 | 3664 | Niort vs PAU FC | 2.42 | 3.08 | 2.93 |
| 23:00 | 4326 | Paris FC vs Le Havre | 2.74 | 2.98 | 2.64 |
| 23:00 | 4581 | Annecy FC vs Nimes | 2.34 | 3.12 | 3.02 |
| 23:00 | 5767 | Grenoble Foot vs Metz | 2.67 | 2.96 | 2.72 |
| 23:30 | 1873 | Valladolid vs Real Madrid | 5.80 | 4.60 | 1.47 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Ijumaa Desemba 30, 2022

Nipashe



UKURASA 29

Mbappe: Nguvu zote sasa nazielekeza PSG

# SIMBA, PRISONS HATUMWI MTOTO

## ...Mgunda awaahidi mashabiki wa Msimbazi watafunga mwaka kibabe...

**Na Saada Akida**

HUKU ikiendelea kukosa huduma ya nyota wake, Peter Banda na Moses Phiri, Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, amesema amejipanga kufunga mwaka kwa furaha pale atakapoikaribisha Prisons katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Mechi hiyo imepangwa kuchezwa kuanzia saa 12:15 jioni na Simba itashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 3-1, walioupata kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini, Mwanza dhidi ya KMC FC ya Dar es Salaam.

Katika mechi ya mzungumzo wa kwanza, Wekundu wa Msimbazi walipata ushindi wa bao 1-0, shukrani za pekee zikienda kwa kiungo, Jonas Mkude ambaye alifunga goli hilo.

Akizungumza jana jijini, Mgunda, alisema maandalizi yote kuelekea mchezo dhidi ya Maafande hao yamekamilika na yako vizuri.

Mgunda, kocha wa zamani wa Coastal Union alisema anafahamu wanakutana na moja ya timu nzuri na yenye ushindani lakini kikosi chake kitashuka dimbani kwa dhamira ya kuvuna pointi tatu muhimu.

Kocha huyo alisema anatambua mechi hiyo haitakuwa nyepesi kwa pande zote mbili kwa sababu wapinzani wao wanacheza soka la ushindani.

"Tunawaheshimu wapinzani wetu, timu yao ni nzuri na ina benchi la ufundi zuri, kikubwa tumejipanga vizuri katika mchezo wa kesho (leo) kuhakikisha tunavuna pointi tatu na hatimaye kuelekea kufikia malengo yetu.

Kuhusu kutumika kwa nyota wake mpya , Ntibazonkiza (Saido), yuko vizuri na muda wowote anaweza kuonekana ndani ya kikosi cha mchezo wa kesho (leo), kwa sababu tayari ni mali ya Simba," alisema Mgunda.

Aliongeza katika mchezo huo watashuka dimbani kwa tahadhari kutokana na rekodi ya timu hizo kila wanapokutana ingawa anaipa timu yake nafasi kubwa ya kushinda kwa sababu wanatumia uwanja waliouzoea zaidi.



Kiungo wa Simba, Mzamiru Yasin (kushoto), akijaribu kufanya shambulizi dhidi ya golikipa chaguo la tatu wa timu hiyo, Ally Salim kwa ajili ya kujiandaa na mechi mbalimbali zinazoendelea hapa nchini. **PICHA: SIMBA SC**

Naye mwakilishi wa wachezaji wa Simba, Gadiel Michael, alisema baada ya kumaliza mechi za Kanda ya Ziwa, kikosi chao kimerejea vizuri jijini na wako tayari kwa ajili ya kuwakabili Prisons iliyoahidiwa kupata Sh. milioni 30, endapo itashinda mchezo huo.

"Tumejipanga vizuri na tuko tayari kwa ajili ya mchezo wetu dhidi ya Tanzania Prisons, tunatambua ugumu ya wapinzani wetu lakini tumejipanga kuwapa furaha mashabiki wetu hasa kwa kipindi hiki cha kumaliza mwaka," alisema Gadiel.

Aliongeza kuna presha kubwa baada

INAENDELEA UK. 31

## Yanga, Azam FC na vita ya fedha

**Na Saada Akida**

AZAM FC imesema kwa sasa haijafikiria kuuza mchezaji wake yeyote na inawataka Yanga ambayo imewasilisha maombi ya kuhitaji huduma ya James Akaminko na Kipre Junior kuwa wavumilivu hadi pale bodi ya klabu hiyo itakapokutana na kutoa uamuzi rasmi.

Yanga kupitia Ofisa Mtendaji Mkuu, Endrew Ntime, ilipeleka maombi kwa Azam ikihitaji kufahamu ofa ya wachezaji hao kwa ajili ya kuimarisha kikosi chao.

Taarifa zilizopatikana jijini, Dar es Salaam zinasema ada ya kila mchezaji ambaye anatakiwa na Yanga ni Dola za Kimarekani 400,000.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam, Abdulkarim Amin 'Popat', alisema kwa sasa akili na nguvu yao wanaielekeza katika mchezo wao wa dhidi ya Mbeya City ambao ndio kipaumbele chao.

Popat alisema baada ya mechi hiyo kumalizika ndio bodi ya klabu yao itakutana kujadiliana na benchi la ufundi pamoja na wachezaji husika na kuwapatia majibu ya maombi yao.

"Tumewajibu wawe na subira kwa sababu Jumamosi tunamechi dhidi ya Mbeya City, baada ya vikao vya bodi na benchi la ufundi na wachezaji tutawasikiliza halafu tutaweka wazi, soka ni biashara.

Hatuna shida ya Yanga, maana tulifanya biashara nao mwaka 2017 kwa Gadiel Michael, kipindi ambacho yuko kwetu na hadi leo (jana), hao Yanga hawajatumalizia fedha zetu ambazo ni Sh. milioni 10," alisema Popat.

Aliongeza wanashangazwa na suala la Feisal Salum 'Fei Toto', kuhusishwa nao hali ya kuwa hawajawahi kufanya mazungumzo yoyote yanayoonyesha wanahitaji huduma ya kiungo huyo na wakitaka watafuata taratibu za kisheria.

"Azam FC tunatambua sheria na kanuni za mchezji mwenye mkataba, kama tukihitaji huduma ya Fei Toto basi tutafuata taratibu kwa klabu husika kufanikisha mipango yetu na sio inavyoelezwa kwa sasa," alisema Popat.

Ofisa Habari wa Yanga, Ally Kamwe, amekiri kupokea barua ya majibu kutoka Azam FC ikiwataka kusubiri hadi bodi ya timu hiyo itakapokutana.

Kamwe alisema baada ya kuridhishwa na viwango vya wachezaji hao, benchi la ufundi linaloongozwa na Nesreddine Nabi lilipendekeza kwenda

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >